

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

#### MKUTANO WA TATU

Kikao cha Hamsini na Tano – Tarehe 21 Juni, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

#### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali. Tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijiini, sasa aulize swalii lake.

Na. 455

**Kulipa Wastaafu Mafao Kwa Wakati**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia watumishi waliostaafu kupata mafao yao kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira na Vijana, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCAL P. KATAMBI) alijibu: -**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (*PSSSF*) ulianzishwa rasmi tarehe 1/8/2018 kwa Sheria Namba 2 ya Mwaka 2018. Mfuko huu ni matokeo ya kuunganisha mifuko minne ya awali (*LAPF, GEPF, PPF na PSPF*) ambayo ilikuwa ikihudumia watumishi mbalimbali wa Umma na kuufanya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kubaki ukihudumia sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati, mipango na utekelezaji wa Serikali katika kuhakikisha watumishi waliostaifu wanapata mafao yao kwa wakati ni kama ifuatayo: -

(i) Kutengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA ili kuweza kuwatambua wanachama wake na kulipa mafao stahiki pale wanapodai mafao;

(ii) Kulipa malimbikizo mbalimbali ya mafao ya wanachama yaliyopaswa kulipwa na mifuko iliyounganishwa na yale yaliyopokelewa kipindi ambacho mchakato wa kuunganisha mifuko huo ulikuwa unaendelea; na

(iii) Kuandaa ofisi mbalimbali nchini kote na kuweka misingi bora itakayowezesha utoaji wa huduma bora kwa wanachama wake ikiwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha wastaifu wanlipwa kwa wakati, waajiri wanakumbushwa kufuata kikamilifu utaratibu ulioainishwa katika Sheria namba 2 ya Mwaka 2018 ambapo inaelekeza ipasavyo maandalizi ya taarifa za wastaifu kabla ya malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifuko imeendelea kuboresha mifumo yake ambapo matarajio ni kuwa waajiri nao wafuate vizuri utaratibu ulioainishwa kisheria ili kupunguza ucheleweshaji wa kulipa mafao kwa wastaaifu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri yenyé mikakati ya Serikali juu ya watumishi wao, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Jimbo la Kibaha na majimbo mengi nchini kuna watumishi ambao wamechelewa kulipwa mafao yao kutokana na waajiri kutokupeleka michango yao kwa wakati. Je, Serikali inawasaidiaje watumishi hao, kwani waajiri wao wamefanya kinyume na utaratibu wa sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kuanzia mwaka 2016 mpaka 2020, kulikuwa na maelekezo mbalimbali ya Serikali juu ya upandishwaji wa vyeo, kuna watumishi ambao wamestaafu wakiwa na barua mkononi lakini wameshindwa kulipwa kutokana na barua zao walizo nazo. Lakini pia kuna watumishi walichelewa kupandishwa vyeo kwa sababu ya waajiri kuwasahau kwenye kuingiza kwenye mfumo.

Je, Serikali inawasaidiaje watumishi hao ili waweze kupigisha hesabu zao kulingana na haki na sheria ilivyo? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobas Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Costantino, kwa kufuatilia vizuri sana haki za wananchi wake katika Jimbo la Kibaha Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la kwanza ambalo ameuliza ni utaratibu gani tunaochukua kwa wale waajiri ambao wanachelewesha michango lakini pia wanaosababisha fedha zile zisiweze kulipwa kwa wakati, hasa hizi za pensheni. Tumekwisha kuchukua hatua mbalimbali kwa mameneja wa mikoa wa PSSSF, lakini pia hata kwa NSSF kwenye maeneo ambayo tunagundua kwamba kuna uzembe wa ukusanyaji wa michango. Tumekuwa tukichukua hatua kali kwa wakurugenzi wa PSSSF Mikoa, lakini pia *complying officers* ambao tumekuwa tukiwaagiza kwa wakati wote watoe taarifa ya wadaiwa sugu kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu waajiri wanapochelewesha michango ni pamoja na kukwepa kodi, kwa sababu kuna PAYE kwenye mshahara wa mfanyakazi, kuna fedha inayopaswa kuinia katika Mfuko wa WCF, kuna fedha inayopaswa kulipwa kama *Skills Development Levy*, lakini vilevile kuna fedha ambayo ni ya mafao ya mfanyakazi, anapomaliza wakati wake wa kazi itamsaidia kwenye maisha yake. Kwa hiyo tunachukua hatua kali, na sheria inaelekeza na tumekuwa tuna kesi mbalimbali ambazo zinaendeshwa kwenye mahakama mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuagiza kwamba mameneja wetu wa mikoa na *complying officers* wawewe kufuatilia michango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili kwa kifupi, ni kwamba swali hili liko Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma, kwa wafanyakazi ambao ni wa Serikali. Nikuombe Mheshimiwa Mbunge, mimi pamoja na weve tuweze kuiona ofisi ile na tuweze kufuatilia madai hayo ili wawewe kupata haki na stahiki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. tunakwenda Ofisi ya Rais, TAMISEMI; Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 456

**Kila Kata Kuwa na Shule ya Sekondari Nchini**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza: -

Je, ni lini ujenzi wa shule za sekondari utaanza katika kata zisizo na shule za sekondari nchini ili kuendana na mpango wa Serikali wa kuhakikisha kila kata inakuwa na shule ya sekondari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari itajenga shule mpya 1,000 za sekondari za kutwa nchini kwa kuanza na ujenzi wa shule za sekondari kwenye Kata zote ambazo hazina shule za sekondari. Mradi huo unatakelezwa kwa awamu, na katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi bilioni 220 kujenga shule 310 mpya za sekondari za kutwa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura, swali la nyongeza.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo

yanaonesha kwamba kazi inaendelea. Lakini niiombe Serikali, pamoja na kazi, kasi iendelee. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mtwara una Kata 191 na kati ya Kata hizo, 137 zina shule za sekondari na Kata 57 hazina shule za sekondari. Na jambo hili linasababisha wanafunzi kutembea umbali mrefu sana kufuata shule za sekondari, na matokeo yake ni upungufu mkubwa wa vyumba nya madarasa katika Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba, je, katika shule hizi 310 Mkoa wa Mtwara umetengewa shule ngapi katika kipindi hiki? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba shule ni walimu pamoja na mambo mengine yote. Sasa Mkoa wa Mtwara una upungufu wa walimu wa sayansi wa asilimia 41. Sasa nina wasiwasi kwamba kama hakutakuwa na maandalizi ya kutosha, kukamilika kwa madarasa au kwa shule hizi zitakazojengwa kutaongeza tena upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba baada tu ya kukamilika kwa shule kunakuwepo na walimu wa sayansi wa kutosha ili kupunguza tatizo la uhaba wa walimu wa sayansi? Ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali hayo mawili. Swali la kwanza kwa sababu linahitaji takwimu unaweza ukampatia baadaye, kwamba katika hizo shule 310 ngapi zinakwenda Mtwara. Jibu swali la pili la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari umeshanipa mwongozo kuhusu takwimu sahihi na mimi nitampatia takwimu sahihi katika mwaka huu wa fedha tutajenga shule ngapi. Lakini niwahakikishie wananchi wa Mtwara kwamba Kata zote zilizobaki 57 zitajengwa sekondari za Kata kwa sababu zipo katika mpango wetu kwa sababu idadi ya shule tulizonazo zinatosheleza Kata zote nchini ambazo hazina shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, anasema Mkoa wa Mtwara una upungufu wa walimu, hususan wa sayansi, na alitaka kujua mpango wa Serikali ni upi kuongeza. Ni kwamba Serikali itaendelea kuajiri kama ambavyo tulitangaza hizi ajira ambazo muda mfupi, ndani ya wiki mbili hizi tutakuwa tumeshatoa hayo majina. Lakini vilevile Serikali itaendelea kuajiri walimu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu kwamba tutaendelea kuangalia hivyo vigezo ambavyo amevitaja, wakiwemo walimu wa sayansi, na masomo mengine hatutayaacha kwa sababu yote yanahitajika katika elimu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, wakati unajibu hapo umesema fedha zinatosheleza kwenda kwenye kata zote ambazo hazina shule, na Mtwara wanazo 57. Hizo sole zote zitajengwa mwaka huu wa fedha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ambacho nilikuwa nakieleza kwa kifupi ni kwamba Mradi wetu wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari Nchini ni ujenzi wa shule za sekondari 1,000. Na awamu ya kwanza Mwaka huu wa Fedha ambao tunakwenda, 2021/22, tunaanza kujenga shule 310.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika hizi 310 ni kwa mwaka huu. Halafu mwakani tutakuwa na idadi nyingine

ya shule kwa Mwaka mwagine wa Fedha kwa maana ya 2022/2023, tutaleta fedha nyingine. Lakini mradi wetu unatosheleza kujenga shule zote kwa sababu tuna upungufu katika Kata kama 780 ambazo hazina sekondari za Kata hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo bado tutajenga na bado zile kata ambazo zina idadi kubwa ya wanafunzi tutapeleka vilevile sekondari nyingine, yaani kutakuwa na sekondari mbili katika Kata moja ili tuweze ku-*accommodate* idadi kubwa ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilichomwambia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba awe na uhakika kwamba Kata zote za Mtwara zitafikiwa. Lakini kwa mwaka huu nitampa idadi kamili ya shule ngapi tunajenga na mwakani tutajenga shule ngapi na mara ya mwisho tutamaliza kwa ngapi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema tatizo la upungufu wa walimu litaanza kupunguzwa kwa ajira 6,000 zilizotangazwa. Ninapenda kujua, kati ya hizo ajira 6,000 za walimu, ni walimu wangapi watakwenda kwenye masomo ya sayansi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Naibu Waziri, hilo nalo linahitaji takwimu, utampelekea idadi ya watakaokwenda kwenye kufundisha sayansi kwa sababu na mimi nawasubiri Mbeya hao wa sayansi.

Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 457

## **Ujenzi wa Barabara ya Redio Habari Maalum – Olturumet Hospital Arumeru**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa Barabara ya Redio Habari Maalum kwenda Hospitali ya Wilaya ya Olturumet kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA  
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Redio Habari Maalum hadi Hospitali ya Wilaya ya Olturumet iliyopo Arumeru Magharibi yenye urefu wa kilomita 2.5 ni mionganini mwa miradi nchini ambayo ni ahadi za Rais. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, na itatoa kipaumbele cha ujenzi pindi fedha za ujenzi zitakapopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuifanya matengenezo barabara hii kila mwaka wa fedha ili kuhakikisha inapitika majira yote ya mwaka. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 na 2020/2021 Serikali imetoa shilingi milioni 37.7 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 56.75 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Redio Habari Maalum hadi Hospitali ya Wilaya ya Olturumet.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Noah Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara hii iliahidiwa na Mheshimiwa Rais na umepita muda mrefu sana, na wananchi wamekuwa wakihoji, na katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri sijaona *commitment*. Je, ni lini hasa fedha zitapatikana kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa tunakwenda kuahirisha Bunge keshokutwa na wananchi wamekuwa wakiniuliza kila siku na kila saa kwa sababu hospitali hiyo inatumiwa na wagonjwa wengi sana kwenda kwenye hospitali ya wilaya. Ni nini nitakwenda kuwaambia wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibu nitakaporudi Jimboni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameuliza tu kwamba lini hasa fedha zitapatikana kwa sababu ahadi hii ni ya muda mrefu, na katika jibu letu la msingi tumeeleza hapa kwamba mara fedha zitakapopatikana basi barabara hii tutaiingiza katika mipango yetu ya kujengewa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kuwa Serikali ilisikia kelele ama maombi ya Wabunge ambayo waliyatoa katika Bunge lako Tukufu na kusababisha Serikali kutaka kuanzisha chanzo kipyaa cha fedha ili *TARURA* iweze kuongezewa,

ninaamini tutakavyopata ongezeko la fedha hiyo tutazingatia ombi la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ameuliza ni nini akawaambie wananchi. Akawaambie tu wananchi kwamba ahadi ambayo viongozi wetu wakubwa waliiota itatekelezwa mara hapo fedha itakapopatikana. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Maji. Mheshimiwa Stella Simon Fiya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 458

### **Tatizo la Maji – Tunduma**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Mradi mkubwa wa maji katika Mji wa Tunduma ili kutatua changamoto wanayoipata wakazi wa mji huo?

**NAIBU SPIKA:** Naona jirani yako anacheka hapo, soma Kanuni ya 49. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Tunduma unapata maji kutoka kwenye visima virefu tisa vilivyoko maeneo ya lkulu, Sogea, Mamboleo, Tazara, Maporomoko, Mahakamani, Majengo, Msongwa na Makambini. Visima hivyo vinazalisha maji lita 2,072,000 kwa siku wakati mahitaji ya maji kwa Mji huo ni lita 4,413,000 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha huduma ya maji safi na salama katika Mji wa Tunduma, Serikali

inatekeleza mipango ya muda mfupi na muda mrefu, ambapo katika mpango wa muda mfupi mwaka 2020/21, Serikali kuititia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji (RUWASA), imechimba visima virefu sita vyenye uwezo wa kuzalisha maji lita 600,000 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji ya visima hivyo utafanyika kuanzia mwezi Julai, 2021, na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Septemba, 2021. Vilevile, Serikali itafanya upanuzi wa mtandao wa maji katika maeneo mengine ya Mji wa Tunduma ikiwemo maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa muda mrefu wa kuboresha huduma ya maji safi na salama na yenye kutosheleza katika Mji wa Tunduma, Serikali imepanga kujenga mradi kuititia chanzo cha maji cha Mto Bupigu uliopo Wilaya ya Ileje wenye uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha lita milioni 73 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina (*detailed design*) wa mradi huo anatarajiwa kupatikana katika robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, Serikali itaendelea kufanya utafiti wa vyanzo vya maji juu na chini ya ardhi ili kupata maji yenye kutosheleza katika Mji wa Tunduma na miji mengine hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza mradi wa kutoka Ileje Mto Songwe kuja Tunduma ulifanyiwa upembuzi yakinifu kutoka mwaka elfu 2013 na kampuni ya *networkers* kutoka Marekani. Mradi huu ulikuwa unaghanimu kiasi cha Shilingi bilioni tatu. Sasa nataka kujua;

Je, ni lini mradi huu utakamilika ili wananchi wa Tunduma waweze kunufaika na maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuwa wananchi wa Kata ya Mpemba na Kata ya Katete wamekuwa waktegemea mradi wa maji kutoka katika Wilaya ya Mbozi maeneo ya Ukwile, lakini mradi huu umekuwa ukisumbua sana kutokana na miundombinu kuwa mibovu, miundombinu iliyopo ilitengenezwa kutoka mwaka 1971 sasa nataka kujua;

Je, ni lini Serikali itawenza kuboresha miundombinu hii ili wananchi wa Kata ya Katete na Kata ya Mpemba waweze kupata maji kwa ukamilifu kabisa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Fiyao kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu wa maji kutoka lleje kwenye Mto Bupigu ni mradi mkubwa. Kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi mwaka ujao wa fedha 2021/2022 mhandisi anatarajiwa kuja kwa ajili ya usanifu wa kina, na tunaratajia mwaka ujao wa fedha usanifu wa kina utakamilika. Kwa hiyo, kadri tutakavyokuwa tukipata fedha mradi huu utatekelezwa kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni kutokana na maeneo ya Mpemba na Katete kupata maji kwa kusumbua sumbua. Binafsi nimeshafika pale kwenye mradi ule, nilikwenda nikiwa na Mbunge wa Jimbo na tulifanya kazi vizuri sana na niliacha maagizo ya kujitosheleza. Na yule meneja ambaye alikuwa pale ambaye kidogo alisusua tulimbadilishia kazi, tulimwondoa pale na sasa hivi anakuja meneja mwingine mwenye maagizo kamili ili miradi hii yote iweze kutekelezwa kwa kina.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Theonest swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Licha ya kutengwa bajeti katika maeneo mbalimbali katika Wilaya ya Kyerwa katika Kata ya Kikukuru haikutengwa hata Shilingi moja; kata hiyo ina vijiji vitatu ambavyo hakuna hata kijiji kimoja chenye maji na wananchi wanatembea umbali wa muda mrefu kutafuta maji.

Sasa nataka kujua ni mpango gani mahususi wa kusaidia hiyo kata ili waweze kujkwamua na wao kupata maji? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji Mhandisi Mahundi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata hizi alizozitaja katika Jimbo la Kerwa nazo pia zimepewa jicho la kipekee kabisa. Unaweza ukaona kwenye bajeti yetu huku haikupangiwa, lakini kipekee nipende kumshukuru Mheshimiwa Rais ambaye ameweeka mkazo katika kuona miradi yote ya maji nchini itafanyiwa kazi. Kama mlivyomsikia, mama yetu ametuahidi kutoungezea fedha zaidi ili miradi yote iweze kutekelezwa. Hivyo nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge, mradi huu pia tutakuu kuutekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hhyuma swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi.

Naomba kufahamu, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji wa Ziwa Basutwa ambao utasambaza maji kwa vijiji tisa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Hhayuma Mbunge wa Hanan'g kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote ambayo inapatikana kuitia maziwa makuu, mito na vyanzo vikubwa vya maji vyote vimepewa kipaumbele na Wizara. Na kama tulivyowahi kumsikia hapa ndani Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe ameshaji-*commitee* kwa Serikali, kwamba lazima tutajitahidi kutatafuta fedha ili tuweze kuona maziwa makuu na vyanzo vikubwa vya maji vyote tunakwenda kuvitumia kadri fedha tutakakuwa tunazipata.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swalii lake.

Na. 459

#### **Matibabu kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaandaa utaratibu mzuri wa matibabu kwa watu wenye ulemavu wakati ikisubiri Bima ya Afya kwa wote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL).** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba

kujibu swalii la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka utaratibu wa kuwatambua watu wenye ulemavu kuitia Kamati za Watu Wenye Ulemavu kuanzia ngazi ya kijiji na kuwaunganisha kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma za afya kulingana na mahitaji yao. Aidha, kuitia mipango kabambe ya afya ya halmashauri Serikali imeendelea kuwatengea rasilimali kulingana na mahitaji yao. Mfano kwa walemovu wa ngozi wanawezeshwa mafuta ya kuzuia juu (*Sun Cream*) ambayo kwa sasa hutengenezwa katika Hospitali ya Kanda ya *KCMC*, na bidhaa hii imeingizwa kwenye orodha ya bidhaa za afya zinazosambazwa na Bohari ya Dawa (*MSD*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoea miongozo ya miundombini ya kutolea huduma kwa kuzingatia haki za watu wenye ulemavu. Pia, Wizara imeendelea kutengeneza miongozo na mafunzo kwa watoa huduma ili kuwezesha na kuboresha utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mswada wa Bima ya Afya kwa Wote unakuja, hii ni fursa muhimu sana kwa sisi Wabunge kutengeneza sheria nzuri zitakazolinda haki za watu wenye ulemavu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, swalii la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri; nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ugonjwa hautasubiri mpaka mpango huu mzuri wa bima ya afya kwa wote ukamilike, na kwa kuwa miongozo ambayo inatolewa na Serikali kiuhalisia haizingatii na watendaji; ni nini kauli ya Serikali kwa watendaji hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ikumbukwe kwamba wakati wa Bajeti ya Wizara hii ya Afya, Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha hotuba ya bajeti yake alisema kwamba Serikali imeandaa utaratibu mzuri wa matibabu kwa wazee, ambapo alisema kwamba zitaandaliwa tisheti nzuri ambazo zitahamasisha utoaji wa huduma bora kwa wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali inaonaje mpango huu mzuri ukawajumuisha na watu wenye ulemavu?

Kwa mfano kama tisheti hizi zitaandikwa mzee kwanza, basi iwe mzee kwanza na mtu mwenye ulemavu, lakini pia kama itaandikwa kwamba tuwajali wazee basi tuwajali wazee na watu wenye ulemavu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL).** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kusema kwamba ni kweli kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema, kwamba ugonjwa na matatizo hayasubiri mswada kutengenezwa. Lakini kama ambavyo unajua kwamba kwa sasa kwenye hospitali zetu; na kwenye eneo hilo anachotaka kujua Mheshimiwa Mbunge ni tamko gani linatolewa. Kwa sababu kwa kweli pamoja na kuwepo na sheria na vitu, vingine inawezekana kuna maeneo ambayo haizingatiwi maelekezo ya Serikali kwa mambo ambayo kwa sasa yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi niseme na nitoe ari kwamba, kwanza agizo, Waganga Wakuu wa Mikoa na Ma-*DMO* wanapokuwa wanazunguka; cha kwanza kwenye CCP zetu na kwenye *supervision* zao wahakikisha kwamba wamekagua na kuhakikisha kwamba hizi haki zimezingatiwa. Pia kuwaomba kupitia TAMISEMI Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala kusimamia suala hilo ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni kuhusu suala la kuunganisha huduma za watu wenye ulemavu pamoja na huduma za wazee. Kama ambavyo tayari Mheshimiwa Waziri ameshazindua hili suala la tisheti na kuzindua huo mkakati wa kuweza kuboresha huduma za wazee kama ambavyo mmeona kwenye vyomba vya Habari; tunachukuwa wazo lake kwamba hilo suala liende kuunganishwa pamoja na suala la watu wenye ulemavu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Flatei Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 460

### **Ujenzi wa Barabara ya Haydom - Singida**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mbulu – Haydom – Singida kwa lami, ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais tangu mwaka 2015?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tena matumizi ya kanuni ya 49. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mhandisi Msongwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mbulu - Hydom hadi Singida yenye urefu wa kilometra 160.5 inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*). Barabara hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili za Mbulu – Haydom urefu wa kilometra 70.5 na Haydom – Singida urefu wa kilometra 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya pili ya Mbulu – Haydom imetangazwa kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi kwa kuanza na kilometra 25 na sehemu zingine zilizobaki zitaendelea kuongezwa wakati sehemu ya kwanza ya kilometra 25 ikiendelea. Sehemu iliyobaki ya Haydom – Singida ipo katika hatua ya manunuzi ili kumpata mhandisi mshauri atakayefanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kabla ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo ile barabara ambayo nilitaka kuruka *somersault* humu ndani. Kwanza niishukuru Serikali kwa kutangaza hizi kilometra 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kwenye bajeti ya Serikali ziko kilometra 50;

Je, ni lini unatangaza tena *slot* iliyobaki ya kilometra 25?

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kuwa amesema barabara hii ina kilometra 70,

Je, kilometra 20 zinazobaki point tano atatangaza lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mhandisi Msongwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Flatei Grerory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini, kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru kwanza leo hajataka kuruka sarakasi. Na kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri wakati wa bajeti kwamba barabara hizi zitatangazwa ni kweli zimetangazwa, na hizo kilomita 25 zinaanza kujengwa kwa bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti ya mwaka tutakayoanza Julai pia kuna fedha imetengwa. Kwa hiyo tutaendelea na ujenzi kadri fedha itakapopatikana, lakini kwenye bajeti pia tumetenga. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kadri fedha itakapopatikana kilomita zote na barabara yote hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Sibiti hadi Hydom kwa kiwango cha lami kwa sababu tayari ipo kwenye bajeti? Ahsante (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyouliza Mheshimiwa Flatei ndio mwendelezo wa barabara kutoka Hydom kwenda Daraja la Sibiti. Ni barabara ambayo inafanya kama kilomita 300 na kitu ambayo inaanzia Kolandoto, Lalago, Sibiti, Hydom, Mbulu hadi Karatu. Tayari tumeshaanza ujenzi, kwa maana ya daraja na kilomita zake takriban 25; na kwa hiyo kadri tutakavyoendelea kupata hela

barabara hii tutaiunganisha yote kuwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 461

**Ujenzi Wa Barabara ya Kutoka Manyoni – Dodoma  
kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa barabara ya kutoka Manyoni - Sanza - Chipanga - Bahi hadi Dodoma kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG.  
GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu Swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Manyoni East – Heka - Iseke - Sanza - Chipanga katika Wilaya ya Bahi; Chidilo Juction – Bihawana Juction Dodoma yenye urefu wa kilometra 194 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *TANROADS* ambapo ni Mkoa wa Singida na Dodoma. Kati ya hizo kilometra 126 zinasimamiwa na *TANROADS* Mkoa wa Singida na kilometra 68 ni Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii kiuchumi, Serikali imeanza na hatua ya

kwanza ya ujenzi wa daraja la Sanza ambapo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja lenye urefu wa mita 75 na barabara unganishi zenyé jumla ya urefu wa kilometra 14.5 kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya Shilingi milioni 1,500, sawa na bilioni 1.5 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Daraja la Sanza ambalo ni kiungo muhimu kwa barabara hii inayounganisha Mkoa wa Singida na Dodoma. Aidha, mipango ya ujenzi wa sehemu ya barabara inayobaki kwa kiwango cha lami itaendelea kufanyika kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulishafanyika wa daraja la Sanza.

Je, nini *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba inaanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa kipande cha barabara ambacho kitaunganisha daraja hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, ni lini Serikali itawamalizia kuwalipa fidia wananchi wa vijiji vya Sanza Chicheho na Ikasi ili ujenzi wa daraja uweze kuanza? Ahsante sana (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mhandisi Msongwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Pius

Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi, ni kwamba tayari tumeshakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja na ujenzi huo utaanza mara moja, ikiwa ni pamoja na *approach roads* zenye urefu wa kilometra tisa upande wa Singida na kilometra tano nukta kadhaa upande wa Dodoma kwa ajili ya kuondoa changamoto iliyokuwepo kwa sababu hilo daraja liko chini. Kwa hiyo ujenzi utaanza mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la fidia; daraja hili limehamishwa mahali lilipokuwa na barabara inajengwa upya sehemu ya hilo daraja. Tayari fidia, atakubaliana nami Mheshimiwa Mbunge, Wizara na Serikali tumeshalipa zaidi ya milioni 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya wananchi kulalamika tumefanya tathmini upya na kuona kwamba zinahitajika si zaidi ya milioni 65. Tayari mchakato wa kupata hizo fedha unaendelea ili kabla ya kuanza ujenzi tumalize kwanza kuwalipa wananchi fidia halafu tutaanza ujenzi wa daraja hilo. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Manyoni kwamba fidia tayari tumeshafanya tathmini upya, tutawalipa, halafu tutaanza ujenzi wa hilo daraja na hizo barabara zake. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwanza, naomba niipongeze Serikali kwa kutangaza barabara ambayo nilikuwa naipigania hapa Bungeni kwa muda mrefu ya kipande cha kilometra 25 kutoka Itigi kuelekea Noranga. Sasa, je, Serikali iko tayari kuongeza kipande kingine katika bajeti ijayo ya 2021/2022 angalau kufanya urefu uwe wa kutoshatosha? Barabara hii ni ndefu, ina kilometra 219.

**NAIBU SPIKA:** Unamaanisha bajeti ya 2022/2023 au? Kwa sababu hii si ndiyo tumetoka kuijadili sasa hivi?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapana, namaanisha bajeti iliyo tangazwa ni hii ambayo inaishia Juni. Je, kuanzia Julai 2021/2022, Serikali iko tayari kuongeza kipande kingine ili barabara hii iweze kufanya vizuri zaidi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, msaidie kama hiyo bajeti ipo kwenye bajeti yenu au haipo. Inaonekana Mheshimiwa Massare hajaipitia hiyo bajeti, kwa hiyo hajui kama ipo ama haipo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahaya Massare kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zilizotangazwa zimetangazwa kwa bajeti ambayo tunaendelea kuitekeleza kabla ya tarehe 30 Juni na barabara anayoisema pia tumeitengea fedha kwa bajeti tutakayoanza kutekeleza Julai. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea na ujenzi kwa kipande kinachoendelea mpaka barabara itakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo bajeti tuliyotangaza ni kwa mwaka huu tunaoendelea nao kabla ya Juni, 30, lakini tumetenga pia fedha kwa ajili ya bajeti tunayoanza 2021/2022. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. nadhani majibu yanamtia moyo kwamba fedha zipo kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 462

**Ujenzi wa Barabara ya *Bypass* – Maswa**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya *Bypass* ya Mji wa Maswa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa kazi ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya mchepuo katika mji wa Maswa (*Maswa Bypass*) yenye urefu wa kilometra 11.3 ulisainiwa tarehe Mosi Juni, 2021 kati ya Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) na Kampuni ya *M/S CHICO* ya China kwa gharama ya shilingi 13,446,688,420.00 na muda wa ujenzi ni mlezi 15 ambapo ujenzi wa barabara hii unatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwezi Julai, 2021. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swalii la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza niishukuru sana Serikali kwa kuingia mkataba na mkandarasi huyu ili ujenzi uanze tarehe Mosi, Julai, kwa hilo kwanza napongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ili niweze kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza, ni kwamba swalii la kwanza; mikataba mingi ya ujenzi inasainiwa, lakini ujenzi

unapopita maeneo yao, watu wanakuwa hawajalipwa *compensation* ili ujenzi ule uanze. Je, Serikali imekwishalipa *compensation* kwa wale watu wa sehemu ambako mradi huo unapita ili mradi huo uanze?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mkandarasi huyu waliyepatiwa wa *CHICO Construction* ndio huyu huyu aliyejenga barabara ya kilometra 50 kutoka Mwigumbi kwenda Maswa. Barabara hii hata kabla haijakabidhiwa ilikuwa tayari imekwishaanza kupata mashimo na kuharibika. Mkandarasi huyo sasa hivi anafanya *mobilization* ku-*bypass* ili aanze kukarabati barabara ambayo hata bado hajaikabidhi. Je, Serikali ina uhakika gani kwamba baada ya kumpa mkandarasi huyu kazi hiyo ya *bypass* atajenga kwa kiwango kinachostahilli? Ahsante sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Waitara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyongo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, utaratibu wa Serikali ni kwamba barabara haiwezi kuanza kujengwa kama wananchi hawajalipwa fidia katika eneo hilo. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kabla barabara haijaanza kujengwa, wananchi watalipwa fidia na baada ya hapo ndiyo ujenzi utaendelea; hilo namuondolea wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, anauliza mkandarasi ambaye amepewa barabara hii, *M/S CHICO*, kwamba alijenga barabara kutoka Mwigumbi kwenda Maswa na imeharibika. Bahati nzuri mwenyewe Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba barabara hii haijakabidhiwa, utaratibu ni kwamba ukipata kazi, unafanya kazi yako, kabla hujakabidhi kuna muda wa matazamio na lolote likitokea, kama kuna sehemu imeharibika, unapaswa kutengeneza

kwa gharama zako. Ameshaelekezwa maeneo yote ambayo yameharibika ayarekebishe ili aendelee na kazi nyine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, kwamba huyu tutamfuatilia na kumsimamia kwa ukaribu, kazi lazima ikamilike. Kama kuna mahali kuna shida tutawasiliana mara kwa mara na Mheshimiwa Mbunge ambaye yuko karibu na wananchi wake, ili fedha ya Serikali ifanye kazi ambayo imekusudiwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili kuuliza swali. Napenda kuuliza swali; ni lini Serikali itanza ujenzi wa barabara ya kutoka Igawa, Mbeya mpaka Tunduma, zikiwemo njia nne za Mbeya Bypass kwa ajili ya kupunguza msongamano uliopo pale Mbeya? Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu kwa swali hilo muhimu sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwenisongole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja ni barabara muhimu sana na kwako Mbeya Mjini ni shida. Bahati nzuri mwezi uliopita tulikwenda kule Mbeya, kulikuwa na mgomo wa bajaji, pikipiki na daladala, shida ni kwamba kuna msongamano mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mpango mkubwa wa Serikali wa kujenga barabara ya njia nne. Tunafanya mpango na majadiliano na Benki ya Dunia, tukipata fedha hiyo wakati wowote kuanzia sasa, barabara hii itajengwa ili kuweza

kupunguza msongamano katika Mji wa Mbeya na maeneo ya jirani. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 463

**Mapato Yatokanayo na Uvuvi wa Bahari Kuu**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza: -

(a) Je, ni asilimia ngapi ya mapato yatokanayo na Uvuvi wa Bahari Kuu yanaenda upande wa Zanzibar?

(b) Je, kwa miaka mitano iliyopita Zanzibar imepata kiasi gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa mapato yatokanayo na uvuvi wa Bahari Kuu unafanyaika kwa mujibu wa Sheria ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 5 ya mwaka 2020, Kifungu cha 79, ambayo inaelekeza mgawanyo wa mapato yanayokusanya na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu kwa utaratibu ufuatao, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar asilimia 20; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania asilimia 30; na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu asilimia 50.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Mamlaka ya Kusimamia Uvubi wa Bahari Kuu ilikusanya jumla ya Dola za Kimarekani 1,352,107.50 sawa na Sh.3,091,837,178.10. Kutokana na makusanyo hayo na kwa kuzingatia maelezo yangu katika kipengele (a), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufikia mwezi Machi, 2021 imepata mgao wa Sh.618,367,435.62.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Maelembeka, swalii la nyongeza.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Nimshukuru pia kaka yangu, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri yanayoridhisha na kutia moyo. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza; kwa kuwa kipato hicho ni kidogo, Serikali ina mpango gani wa kuongeza pato hili kwa pande zote mbili za Muungano na kuwasaidia wavuvi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii langu la pili; kwa kuwa mgawanyo wa mapato ni wa kisheria, je, Wizara inawasaidiaje wavuvi kutoka Zanzibar wanaoleta samaki bara na wale wanaopeleka mifugo Zanzibar ili kuondoa kero na usumbufu unaowapata? Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jitihada gani za Serikali zinafanywa kuongeza pato hili kwa kuwa pato hili ni dogo. Kwanza naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge na

Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla, natoa shukrani nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Mama Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nane, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuridhia mabadiliko ya sheria na kanuni ambazo zimekwenda sasa kufungua mwanya wa uwekezaji zaidi katika uvuvi wa bahari kuu. Hivi ninavyozungumza, tayari makampuni takribani 20 yameshakata leseni na kuingiza pato la zaidi ya shilingi bilioni moja kwa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu; ni jitihada kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada nyengine ambayo Serikali hizi mbili zimefanya ni kuhakikisha kwamba tunaweka kipengele ya uvutiaji kwa maana ya *incentive*. Tumeshatoa maelekezo kwa Mamlaka yetu ya Uvuvi wa Bahari Kuu kuitisha kikao ambacho kitatusaidia kuwaunganisha wadau wote kwa lengo la kwamba tuvitambue sasa vile vivutio ambapo tutawapa Waheshimiwa Mawaziri wawilli; wa Jamhuri na yule wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, waweze kuvitangaza hadharani ili wawekezaji wajue iko fursa gani ya kuweza kuwekeza zaidi katika uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, baada ya hili la kuongeza kipato, ni nini tunafanya kuondoa vikwazo. Mambo makubwa mawili yanafanyika; hivi sasa timu zetu za wataalam kutoka Zanzibar na kutoka Bara zinakaa pamoja kujadili mambo makubwa mawili; la kwanza, ni leseni za wavuvi wa Zanzibar ziweze kufanya kazi hata huku Bara pia, lakini la pili ni kuondoa kikwazo kile cha mifugo inayotoka Bara kwenda Zanzibar na kulipiwa ushuru mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tupo katika hatua nzuri baada ya Wakurugenzi hawa kumaliza, watakaa Makatibu Wakuu na baadaye watakaa Waheshimiwa Mawaziri ili kufanya *harmonization* ya sheria hizi na hatimaye Watanzania wote wa Bara na Visiwani, waweze ku-enjoyrasilimali za Taifa letu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, sasa aulize swalii lake.

Na. 464

## **Serikali Kuzalisha Mbegu za Mninga**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itazalisha mbegu za mti wa mninga ili wananchi waweze kupanda na kuzalisha miti hiyo kibiashara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umaarufu wa mti wa mninga katika matumizi ya shughuli za ujenzi na utengenezaji wa samani. Kutokana na umuhimu huo, Wizara kuititia *TFSimeandaa mpango wa miaka mitano wa kuendeleza mti huo na miti mingine kibiashara kwa kuipanda kama ilivyo miti ya kigeni*. Mpango huo unahusisha aina 56 za miti ya asili ikiwemo mninga ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara imetenga shilingi 60,000,000 kwa ajili ya kuzalisha mbegu za miti hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Wizara ni kuongeza kasi ya uzalishaji wa mbegu za miti ya asili ili wananchi waweze kuzipata kwa urahisi kuititia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania zilizopo kwenye kanda mbalimbali hapa nchini. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha elimu ya upandaji wa mti wa mninga ili kuleta hamasa ya kupanda na kutunza miti hiyo. Serikali itahakikisha elimu ya utunzaji na uendelezaji wa miti ya mninga iliyopo katika maeneo ya mashamba ya wananchi inatolewa ili miti hiyo itunzwe kwa ajili ya kuzalisha mbegu ili kuwezesha wananchi kupanda miti ya mninga kibiashara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naipongeza Serikali kwa majibu mazuri sana ambayo wameyatoa hapa mbele ya Bunge, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza; miti hii inapatikana kwenye maeneo yaliyohifadhiwa na maeneo ambayo hayajahifadhiwa, yakiwemo mashamba ya watu binafsi na ardhi ambayo inamiliikiwa na watu binafsi. Sasa swali langu; kwa nini Serikali isitoe ruhusa maalum itakayosimamiwa na Serikali za vijiji kwenye maeneo hayo ambayo hayajahifadhiwa ili watu waruhusiwe kuvuna miti wanayoimiliki kihalali kwa ajili ya matumizi ya ujenzi wa nyumba za asili pamoja na nyumba za kisasa bila kwanza kupata vibali vile vya maliasili kwa sababu maeneo hayo hayahusiani na maliasili? Kwa sababu matumizi yale siyo ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; kuhusu uvunaji wa miti kwenye maeneo yaliyohifadhiwa; kwa nini Serikali isitoe elimu kwanza kuitia mikutano ya hadhara na njia nyingine za mawasiliano ili wananchi wapate ufahamu wa kutosha wa namna ya kuomba vibali ili wasiingie migogoro mara kwa mara ya kuvunja sheria za nchi? Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimtoe wasiwaso Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali ipo kwa ngazi zote. Kuhusu swali lake linalosema kwa nini Serikali isitoe ruhusa kwenye maeneo yasiyohifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yote ambayo yana rasilimali za misitu yanahifadhiwa na Serikali ikiwemo Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini kwenye ngazi za vijiji na maeneo ya wilaya, zinahifadhiwa na Serikali za Mitaa, zikiwemo halmashauri za wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo haya ambayo vibali vyake vinatolewa na Maliasili ni yale maeneo ambayo yanahifadhiwa na Wizara. Hata hivyo, kuna yale ambayo yanahifadhiwa na Serikali za Mitaa, vibali vyote huwa vinatolewa kwenye /level ya vijiji na wilaya. Kwa hiyo wale wote ambaao wanahitaji kupata vibali basi wawe wanakwenda kwenye maeneo hayo na pia watapata hivyo vibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe tu kwamba maeneo yote yanahifadhiwa, siyo kwa ajili ya kutunzwa peke yake, lakini pia na uhifadhi wa mazingira pamoja na utunzaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, ameuliza kuhusu elimu; ni kweli kwamba Serikali imeendelea kutoa elimu mbalimbali kwa wananchi ili watambue umuhimu wa utunzaji wa miti. Nimpangidhishwa tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango wa bajeti na fedha zilizoidhinishwa kipindi hiki tumeweka eneo la elimu ambalo tutapita kila maeneo ambayo yanazunguka hifadhi kuhakikisha kwamba wananchi wanapata elimu ya kutosha na namna ya kuomba hivi vibali vya ukataji miti. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Robert Maboto, swalii la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Wananchi wangu wa Jimbo la Bunda Mjini, Alhamisi ya wiki iliyopita tembo wamekula mazao yao, hasa Kata za Bunda Stoo, Balili na Kunzugu. Wapo baadhi ambaao wamefanyiwa tathmini ya mazao yao, je, ni lini Serikali itawalipa fidia yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, labda kama unayo majibu, lakini kama huna nitakupa muda ukafuatilie hilo jambo ndiyo utoe majibu; uamuzi ni wa kwako.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Robert Maboto, Mbunge wa Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza kulipa malipo haya ya kifuta jasho na kifuta machozi na kulikuwa kuna malipo ya kipindi cha nyuma ambayo walikuwa wanadai na niliahidi hata kwa Mbunge mwenzie Mheshimiwa Esther Bulaya, kwamba nitafunga safari niende kwenye maeneo husika tukaangalie ni madai gani ambayo wanadai kisha Serikali iweze kuyalipa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali. Nilita kwenu matangazo tuliyonayo; kwanza ni matangazo ya wageni waliopo hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na wageni 6, wageni wangu ambao wapo Jukwaa la Mheshimiwa Spika kutoka Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Ndugu Jeddah Hasabubaba. Karibuni sana wageni wangu kutoka Dar es Salaam. Hawa ni wageni wanatoka Kampuni ya *Pinetech*, nadhani watakapokuja hapa Dodoma tutawasikia zaidi. (*Makofii*)

Wapo pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, huyu ni mtumishi wa Mungu kutoka Kanisa Katoliki Jimbo la Tanga ambaye ni Padre Gasper Shekigenda. Karibu sana, tunakutakia kila la heri Padri Gasper Shekigenda maana jana tumemwona Mhashamu Pengo akisheherekeea miaka 50 tangu apate Upadri. Kwa hiyo, tunakuombea na wewe Mungu akujaalie uishi maisha marefu. (*Makofii*)

Tunao wageni 24 wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel ambaye ni Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao ni waandaji wa mbio za Siha Afya Marathon wakiongozwa na Ndugu Selina Mkonu. Haya, nadhani hawakupata nafasi. (*Makofii*)

Vile vile wapo wageni nane wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, ambao ni Chama cha Wahasibu Tanzania (*TAA*) wakiongozwa na Ndugu Peter Mwabuja. Sijui na wenyewe hawajapata nafasi! (*Makofii*)

Wapo wageni 78 wa Mheshimiwa Flatei Massay, ambao ni Madiwani na Kwaya ya Umoja wa Kanisa la KKKT Mbulu Vijijiini Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Ndugu Malkiadi Nari. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Flatei Massay, tumesikia na Madiwani wapo hapo, karibuni sana. (*Makofii*)

Wapo wageni 12 wa Mheshimiwa Noah Lemburis, ambao ni viongozi wa dini ya Kikristo na Kiislamu kutoka Arumeru Mkoani Arusha wakiongozwa na Mchungaji Osupat Daud na Shehe Hussein Said. Karibuni sana viongozi wetu, tunawashukuru kwa maombi yenu kwa Taifa hili. (*Makofii*)

Pia wapo wageni watano wa Mheshimiwa *Eng.* Samwel Hhayuma, ambao ni wafanyabiashara kutoka Hanang, Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Clementini Fisoo. Nadhani hawajapata nafasi ya kuingia. (*Makofii*)

Tunao wageni 34 wa Mheshimiwa Saasisha Mafuwe, ambao ni Kwaya ya Waadvestista Wasabato kutoka Hai Mkoani Kilimanjaro, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Ndugu Wang'uba Maganda. Haya nao nadhani hawajapa fursa ya kuingia humu ndani. (*Makofii*)

Wapo wageni nane wa Mheshimiwa Jumanne Sagini, ambao ni Makada wa CCM kutoka Jimbo la Butiama Mkoani Mara wakiongozwa na Ndugu Hamidu Machage, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni 25 wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Lushoto Mkoani Tanga wakiongozwa na Ndugu Abedia Hassan. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 38 wa Mheshimiwa Anatropia Theonest, ambao ni wanakwaya wa Mtakatifu Bakanja kutoka Tabata Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Jonathan Mgogo. Karibuni sana. Eh, naona huku kwenye kwaya wamekuja na Watoto, sasa hao watoto sijatajija majina hapa, lakini niwapongeze akina mama ambao wamekuja na watoto. Jana ilikuwa siku ya akina baba na nimewona baba mmoja ambaye amebeba mtoto, kwa hiyo, naye tumpongeze. (*Kicheko/Makofi/Vigelegele*)

Haya ahsante sana. Huyo amewawakilisha akina baba wote wanaowajali watoto wao. (*Makofi/Vigelegele*)

Tunao pia wageni 26 wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde ambao ni wanachama wa Timu ya Dodoma Jiji, wakiongozwa na Ndugu Mohamed Bakary. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Joseph Kamoga, ambao ni wapigakura wake kutoka Ludewa Mkoani Njombe ambao wameongozwa na Ndugu Alexander Mhagama. Karibu sana; kumbe huyu siyo sehemu ya kwaya. Haya, sawa; huyu baba aliyejukua na mtoto anatoka Njombe. Nampongeza sana.

Sasa changamoto ni kwamba hatujajua kama kaongozana na mama lakini amebeba mtoto au mtoto kaja naye yeye mwenyewe. Sasa hizo taarifa kwa sababu sina, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi mlizompa kwa Makofi. (*Makofi*)

Wapo wageni tisa wa Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Saint John's cha Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Emmanuel John. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Zaytun Swai, kutoka Jijini Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Alina Lungaisa na Ndugu Rukia Iddi. Aah karibu sana, nimewaona, karibuni sana. (*Makofi*)

Pia wapo wageni tisa wa Mheshimiwa George Malima ambaao ni wanawake kutoka Kanisa la Anglicana nchini wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Ndugu Josephine Ndabagoye, karibuni sana akina mama. (*Makofi*)

Vile vile tunao wageni watano wa Mheshimiwa Kenneth Nollo ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (*SUA*) wakiongozwa na Ndugu Peace Faraja. Nadhani hawakupata nafasi. (*Makofi*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Esther Matiko, ambaye ni Msanifu Majengo kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi, huyu ni Ndugu Alex Mariba. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi, ambaao ni dada zake kutoka Mkoani Iringa na hawa ni Benadhetha Mgungusi na Ndugu Norga Komba. Karibuni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mgungusi anao wageni wengine sita ambaao ni Wenyeviti wa UVCCM wa Wilaya zote za Morogoro wakiongozwa na Ndugu Joseph Mhalule. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 80 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi El-Shadai ya Jijini Dodoma ambaao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi, wakiongozwa na Mwalimu Isaack Luhinda. Karibuni sana walimu na watoto wetu, tunawashukuru kwa malezi mazuri. (*Makofi*)

Nami nawapongeza hii Shule ya El-Shadai kwa kuitikia wito wa Mheshimiwa Spika kwamba watoto wawe wanaletwa huku Bungeni kujifunza namna ambavyo chombo chao cha uwakilishi kinafanya kazi.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Saashisha anasema wageni wake wapo upande wa kulia, sasa kulia kwake siyo kulia kwangu, sasa sjui wamekaa upande gani? Aaah, naambiwa wamekaa humo ndani, haya. Karibuni sana wageni kutoka Hai. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyokuwa nayo hapa mezani, tutaendelea na ratiba yetu. Kuna tangazo la michezo hapa, Wabunge wachezaji wasije wakaona sasa mambo yameenda viipi? (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa matokeo ya mechii zilizochezwa siku ya Jumamosi na Jumapili kama ifuatavyo:-

Siku ya Jumamosi tarehe 19 Juni, 2021, kulikuwa na mpira wa miguu (*Football Bunge Sports Club*) ilikubali kipigo cha mabao matano kwa moja dhidi ya Chama cha Waandishi wa Habari. Kwa hiyo, wale TASWA walitangazwa humu ndani halafu wakawaangalia Wabunge wakaona hawatoshi kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, waliotuwakilisha kwa upande wa *football* hiyo siku, naona hadi sura zao wameinama hawataki hata nimtaje mmojawapo. Basi sitawataja, lakini kwa kweli haya mabao mlibugia mengi, tukubaliane na hali. Tunaamini mechii ya Jumamosi mtafanya yale mambo yetu ya “*Hatoki Mtu Jamhuri.*” (*Makofi/Kicheko*)

Haya Ppira wa Pete (*Netball*), *Bunge Queens* ilijibu shambulio hilo kwa kuwafunga Waandishi wa Habari magoli 32 kwa 12. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mliwakilishwa vizuri; na mkiona magoli yalikuwa yanaingia kidogo, mjue hapo kulikuwa na watu wanaokinga yale magoli, wakiongozwa na *Captain* wa Timu Halima Mdee, nami hapa jamani ndio *goalkeeper* mwenyewe. Tuwapongeze sana *Bunge Queens* kwa kazi nzuri. Siku ya Jumapili tarehe 20 Juni, 2021 *Bunge Queens* waliwanywesha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam magoli 40 kwa 30. Kwa hiyo, *Bunge Queens* wanatutoa kimasomaso. (*Makofi/Vigelegele/Kicheko*)

Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawapongeza Wabunge wote. Nami namwomba Mwenyekiti wetu, tunapocheza kule, uwe unakujakuja, unajua pale uwanjani kuna vitu vidogo vidogo huwa vinauzwa, nasi tunatamani tuwe tunanunuliwa na Mwenyekiti wa *Bunge Sport Club* ili tuwe tunakutoa kimasomaso. Kwa hiyo, uwe unatutembelea tembelea uwanjani. (*Makofi/ Kicheko*)

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano. Nimeshaletewa majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Janeth Mahawanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay na Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rwekiza, ajandae.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami kuchangia bajeti hii. Kwanza naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa bajeti hii nzuri kwa Serikali ya Awamu ya Sita maana ni bajeti ya kwanza. Vile vile, nampongeza Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu wake pamoja na timu nzima kwa bajeti hii nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii inatia matumaini na faraja kwa Watanzania kwani ni bajeti ambayo imekidhi changamoto zote za jamii yetu kwa kuweka vipaumbele

ambavyo Wabunge wengi walichangia katika Wizara mbalimbali. Vile vile, bajeti hii inakwenda kukamilisha mahitaji yote hususan kwenye masuala ya afya na miundombinu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napongeza kuhusiana na kipengele cha kodi ya *line* za simu. Tija ya kodi hii ni nzuri, kama ambavyo bajeti imeonyesha Shilingi za Kitanzania bilioni 360 zinakwenda kupatikana ambapo zitakwenda kujenga zahanati na mahospitali. Naiomba Serikali, fedha hizi kama zitakwenda kutekeleza haya, basi kiu kubwa na changamoto ya masuala ya afya katika jamii yetu itakwenda kukamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naipongeza bajeti hii kwenye kodi ya shilingi mia katika kila lita ya mafuta. Fedha hii itakapopatikana itapelekwa *TARURA* kama ambavyo imeonyeshwa, ni kitu kizuri sababu fedha hizi zitakapokwenda kutoa changamoto ya miundombinu, uchumi wetu utakwenda kuimarika hususan kwenye jamii yetu hasa vijijini, kwani uchumi wa nchi unategemea sana suala la miundombinu. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuliona hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile bajeti hii imekwenda kugusa masuala ya vikundi vya akina mama na vijana, hasa katika kutoa mikopo. Ukiangalia hata Mheshimiwa Rais alipoongea na akina mama *ali-insist* sana suala la vikundi vya akina mama kujiunga ili wapate mikopo ambayo itasaidia kutoa ajira na kufanya biashara zenye tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuitia bajeti hii, wakaangalie katika suala la Sheria ya Fedha Mwaka 2018, kwani limekuwa ni mzigo hasa kwenye vikundi vya akina mama. Naiomba Wizara ikatumie wataalamu wa *BoT*katika kutoa elimu, maana vikundi vingi vimeshahamasishwa kujiunga, Iakini kuitia sheria hii wengine wanafunga, hawaelewi sheria ile inataka nini hususan kwenye kutumia teknolojia ya TEHAMA. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara itumie wataalamu wao wa *BoTambao* wanaweza kufafanua sheria hizi wapite kwenye Wilaya wakutane na Madiwani na Bibi Maendeleo, watoe miongozo ya sheria hii hasa katika vikundi vyta akina mama na vijana ili nao watakaposhuka chini kwenye makato wakikutana na akina mama waweze kufafanua sheria hizi ili vikundi viende kuwa imara vikatumie fursa hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kupitia bajeti hii ikaangalie masuala ya sheria za fedha, lakini zaidi sana ikaangalie kwenye kipengele cha mabenki, kwani mabenki yatakaposhirikiana na Serikali katika kuongeza tija kwenye mikopo ya wafanyabiashara, itasaidia sana, maana mikopo ya asilimia 10 bado haitoshelezi. Kwa mfano, Mkoa wa Dar es Salaam, kazi za usafi wa barabara ambazo zilikuwa zikifanywa na akina mama wengi sasa hivi zile kazi zimeamishwa kwa *SUMA JKT*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna kundi kubwa la akina mama ambalo limepoteza ajira na kupitia ajira zile walikuwa wakilea familia, wakisomesha watoto na kujikimu kwa mahitaji yao ya kila siku. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie sana taasisi za kifedha hususan mabenki, kuangalia ni jinsi gani ambavyo mabenki haya yataweza kuongeza mikopo kwa akina mama na vijana lakini mikopo hiyo itoke kwa riba nafuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naishauri Serikali iwekeze kwenye mfumo thabitu ulioungana (*complete and consolidated system*) ambayo watakuwa na utambulisho utakaokuwa na kanzidata ya taarifa za wafanyabiashara. Taarifa hizo zikiwa zinahusisha biashara zao, mali zao anuani za makazi ambazo zitawenza kusaidia mabenki kuwatambua hawa watu na kutoa mikopo kwa gharama nafuu, lakini kwa kutumia mfumo huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali iangalie kwa jicho la pili kuwekeza katika mabenki yote kuhakikisha kwamba gharama za uendeshaji wa mabenki, zisizidi asilimia

55 ya mapato. Ni kwamba inasema ikizidi benki hairuhusiwi kupata *dividend* ambayo ni kutoa faida. Kanuni hii imefanya mazingira ya uwekezaji wa mabenki kuwa ngumu. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie sana katika hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwa kupitia bajeti hii, naiomba Serikali ijikite zaidi katika mapato na mwenendo wa uchumi hususan kwenye ukuaji wa pato la Taifa, kwenye mapato na matumizi ya Serikali, kwenye deni la Taifa, Serikali ijikite sana kuangalia ukopaji na ulipaji wa madeni ili Taifa letu lisije likaingia kwenye adha ya kutokopesheka. Zaidi Serikali iboreshe tena kwenye sekta ya fedha; Serikali irejeshe mifumo iliyokuwa inasaidia benki kutoa mikopo kwa wingi (*Guarantee Credit Schemes*). Benki hizi zilikua kwa kutumia mifuko hii; mifuko ilikuwa inachochea sana utoaji wa mikopo. Kwa hiyo, Serikali ijitahidi kurudisha hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile uendeshaji wa sekta binafsi. Kama tulivyoona Serikali imeweka mazingira mazuri hususan kwenye Mfumo wa Sera na sheria za kodi ambazo zimekuwa ni kivutio kwa wawekezaji wetu. Mwisho, ijjizatiti katika tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Mwaka 2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naipongeza Serikali kwa bajeti hii nzuri na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, atafuatiwa na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, ajiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza namshukuru sana Mungu kwa kunijalia nafasi ya kuwepo hapa. Pamoja na hayo yote, naomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa bajeti hii ya kwanza na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na msaidizi wake Mheshimiwa Masauni kwa bajeti yenu ya

kwanza hii. Nina ushauri na kwa sababu muda ni mfupi, naomba niende haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunakuja huku mara nyingi kuwawakilisha wenzetu hasa Madiwani; kwenye maeneo mengi ya mafao yao/posho zao; sasa kwa sababu Madiwani wengi mara nyingi wamekuwa *waki-suffer* kutokana na namna ambayo wanalipwa, kwanza nawapongeza kwa sababu Serikali imekubali zile hoja za Wabunge ambazo zilikuwa zinaletwa humu, nawe Mheshimiwa Naibu Spika aliletu hoja hapa ili walau Madiwani walipwe kwenye *accounts* zao kama Serikali ilivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri mwiningine ambao sasa kwa kuwa Madiwani hao wana wigo mkubwa na ziko kata nyingine kwa mfano kule Mbulu Vijijini ni kubwa na ni pana, hawana uwezo wa kuizunguka kwa mara moja. Sasa naomba Serikali iangalie kwenye bajeti hii waweze nao kupewa mikopo kama tunayopewa Wabunge ili mikopo hii basi ikawasaidie. Aidha, wapewe usafiri na iandikwe kabisa na ziwe katika *principal* ambazo wao wenyewe wanaweza kulipa kutokana na fedha ambazo watapewa na kuongezewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiinua mgongo cha Mheshimiwa Diwani ni kidogo sana, lakini posho ile ikiongezwa ni wazi kwamba unaweza kuangalia katika mafao haya anaweza kukopeshwa nini? Aidha, kama ni gari dogo au pikipiki. Kwani hawa ni wawakilishi wetu wa kutosha katika maeneo ya kata zetu, kwa hiyo, naomba hili lizingatiwe sana. Kwa sababu hii basi, wataweza kusimamia miradi, maana miradi mingi katika maeneo yetu wanapaswa kusimamia kwa ukaribu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati ambayo inaweza kusimamia miradi ni Kamati ya Fedha kwa mujibu wa sheria na inapata nafasi ya kuzunguka mara nyingi katika maeneo ya Halmashauri. Kwa hiyo, unapompa na kumwezesha Diwani akaweza kuzunguka maeneo haya ni wazi kabisa miradi itasimamiwa kwa karibu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwa kuwa sasa Halmashauri imeshaondolewa mzigo wa ulipaji wa hii posho na mishahara ya Madiwani, napendekeza, tuna Wenyeviti wa Vijiji ambao bado hawajakumbukwa, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie na Serikali ione, Wenyeviti wa vijiji asilimia 20 inayotajwa kwenye kanuni zetu haziwafikii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kwa sababu mshahara ule wa Madiwani umeshaondolewa kwenye Halmashauri kwa kupitia mapato ya ndani, kwa nini fedha hizi zisiende basi tukawapatie Wenyeviti wa Vijiji hata *allowance* kidogo tu? Hata kama siyo mshahara, basi posho ya mwezi kidogo tu ili Mwenyekiti wa Kijiji aone kwamba aah; awe na utaratibu, maana ukiangalia katika mtindo wa sasa hivi, Mtendaji wa Kijiji analipwa fedha. Kwa hiyo, inaonekana Mtendaji wa Kijiji ni bosi wa Mwenyekiti kumbe kwa kawaida kabisa Mwenyekiti wa Kijiji ni bosi na ana Serikali yake ya Kijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Serikali zote ambazo zimeachwa kidogo, ni Serikali ya Kijiji. Kwa hiyo, namwombwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Serikali kwa Wizara ya Fedha ione ni namna gani, kama siyo bajeti hii, basi bajeti ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wenyeviti wa Vitongoji ni wa msingi sana kwa sababu wao ndio wanaotoa habari, wanaotoa taarifa na ndio wanaoandaa mikutano, ndio wanaotekeleza sera zote na ndio wakusanya michango. Kwa hiyo, hata hao wanapokusanya michango waonekane basi. Serikali ipange utaratibu wa namna fulani, hata wao fedha chache ziwe zinawafikia. Hata wao isiwe kama bakshishi, iende kwenye *account*. Maana siku hizi kila mtu ana *account*, waelekezwe hao wapate na fedha kidogo hata kama fedha zenyewe ni chache, lakini ajue kwamba anapata kiwango fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini wakishapata utaongeza *morality* katika Serikali kutoka kwenye ngazi ya Taifa hasa hadi kwenye vitongoji maana hao wote ni Serikali. Ukifanya hivi, Serikali hii itakuwa

imejiwekeea *legacy*; na Mheshimiwa Mwigulu utakuwa umeweweza kufanya hii ya kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji na Madiwani sasa wanaenda kufaidika. Kwa hiyo, naomba hivi vyeo viwili visisahaulike, maana ni vyeo vya msingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye miundombinu na hasa ya barabara. Duniani kote, uchumi hauwezi kwenda vizuri kama miundombinu iko vibaya na hasa miundombinu ya barabara. Naomba Serikali ione, mmeelekeza fedha kwenye barabara nimeona, lakini siyo kubwa sana, ni kidogo. Kwa hiyo, naomba elekeza maeneo haya kwa sababu wakulima wanapotoa mazao, wanapopeleka viwandani na uzalishaji unakuwa mkubwa, Serikali ni rahisi na kupata kodi na kkusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko barabara ambayo kwa kweli nisipoisema naona kama sjafikisha ujumbe, ni barabara yetu moja ya Karatu – Hydom – Sibiti. Nashukuru kwanza Waziri amejibu swalilangu leo na kwa kweli amesema inatangazwa kilometra 25. Kwa ajili hiyo nilishawahi siku moja kuomba hapa nipige sarakasi, hilo na-*withdraw*, leo sipigi hiyo, kwa sababu nimeona kwanza Serikali imekubali na inataka kujenga barabara hiyo. Ni vizuri kushukuru hata kwa kidogo, ni 25 zimetangazwa, nimeziona na imesemwa imetangazwa na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, mmetangaza kilometra 25. Sasa kilometra 25 ni kipande kidogo sana. Kwa bahati nzuri hiyo barabara iko kwenye bajeti inaonyesha kilometra 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe basi, kwa sababu inaonyesha kilometra 50 na hii ni ahadi ya Rais, ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Tano na sasa ni ahadi ya Rais wa Awamu hii ya Sita, mama Samia Suluhu Hassan, alikuja akaisema barabara hii akiwa Dongobesh akiwa pia Haydom. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa itakuwa si vyema sana na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwa sababu ni Waziri wa Fedha

wewe barabara hii, lazima niseme tu ukweli kwa namna fulani ni mdau. Sasa niombe najua bajeti ni kidogo yaani rasilimali ni kidogo, lakini naomba mwakani uiwekee fedha ili walau basi isiwe katika ile hali imesemwa kwamba 25 kwa sababu barabara hii inapita Majimbo tisa; Jimbo la Karatu, Mbulu Mjini, Jimbo la kwangu la Mbulu Vijijini, Jimbo la Mkalama na inakuja mpaka Iramba na inakwenda mpaka Sibiti. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo basi barabara hii itakapofunguliwa itakuwa imekidhi maeneo mengi sana kwa kuwapatia watu hawa huduma. Na unajua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu barabara hii inaleta watu wa kwako wa jimboni kwako kuja katika eneo la Haydom Hospitali. Ni hospitali kubwa sana ya Kanda ambayo iko pale, naomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ajue, anapoanza kujenga hiyo barabara aangalie kwa sababu pale hizi kilometra 25 sijui utaanzia wapi? Na sio suala langu linakuwa la Mkandarasi, lakini angalia eneo hili la Haydom kwa sababu eneo hili ni oevu na pale kuna maeneo ambako hayafiki na hayafikiki. Basi uone ni namna gani ya kuanza kilometra 25, sikupangii uanze wapi lakini angalia eneo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ukiangalia, katika mpango huu wa bajeti, ninaifurahia sana. Lakini nitashukuru kuona kwamba, bajeti ya mwaka huu nimeona pia ipo kilometra zingine 25. Sasa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu wewe ni mtani wangu, unajua kabisa na yupo Mheshimiwa Msaidizi wako anayeitwa *Comrade Masauni* na nyinyi ni vijana wenzangu. Tumekuwa wote Jumuiya ya Vijana hebu wekeni kilometra hii 25 ijayo, ili zifike 50 na hii barabara ikamilike. Weka hiyo *legacy*basi bwana usitake nikaanza kuruka sarakasi huku na unajua hataniruhusu. Sasa kama haniruhusu rafiki yangu si uweke tu fedha mambo yaende vizuri. Kwa nini tuanze kuvunja Kanuni za Kibunge wakati wewe ni Mbwanee na Mbwanee ni Saitaa na Saitaa mambo yote mazuri. *Brother* weka hii fedha ili baadaye kule mzee tuzekee tukiwa tuna barabara. Sasa hivi ni vijana *brother* na barabara hii inapita jimboni kwako, inakwenda mpaka Mkalama, inakutana kule kwa nini usiweke hii fedha? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jamaa ameishia hapo kilometra 25, bajeti hii ya kwako hii. Bajeti ya Mama Samia Suluhu Hassan ya 2022 kwenda 2023 na wewe Mheshimiwa *EngineerMasauni* hapo wekeni barabara hii na Mheshimiwa Naibu Spika uko hapa na najua mtaweka barabara hii na Mungu atawabariki. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapa kwa sababu kengele imelia. Lakini nikushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi hii na Mungu akubariki sana ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, Mheshimiwa Bahati Kenneth Ndingo, ajiandae.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika bajeti ya Serikali, kama ilivyowasilishwa juzi hapa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Nipende kupongeza sana bajeti hii nzuri, ambayo Serikali imeiwasilisha hapa kwetu. Nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa bajeti nzuri ya kwanza. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa bajeti nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya bajeti hii ni mazuri sana na hasa hasa ambaye imenigusa sana ni ile ya *TARURA*. Kuongeza fedha kwenye mamlaka hii au Wakala huu wa barabara vijijiini, ili iweze kupata uwezo mkubwa wa kuboresha barabara za vijijiini. Tunafahamu wote kwamba, vijijiini ndio kuna uchumi, ndio kuna kilimo, kunapelekwa pembejeo, kuna huduma za afya kwenda kwenye zahanati na vituo vya afya, bila barabara huwezi kuzifikia huduma hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule kwa hiyo, kwa kuwa na fedha zaidi kwenye mfuko wa *TARURA*, ina maana huduma hizi zinakwenda kuboreshwa na kuonekana na kufikiwa na wananchi kirahisi zaidi. Lakini na mambo mengi mengi sio tu *TARURA* peke yake, ambayo bajeti imeyagusia na kuyazingatia. Nnaipongeza sana Serikali ya CCM kwa

kuwa siku na kwa kuwa inaboresha maendeleo ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo napenda nizungumzie suala la elimu kwa sababu, tunapoongelea bajeti hapa tunaongelea uchumi na huwezi kupanga uchumi kama huna elimu nzuri. Elimu ndio ufunguo wa maisha na ndio ufunguo. Sasa, kwa hiyo bila elimu nzuri huwezi kuwa na uchumi mzuri na elimu yetu bado ni ya mitihani. Mtoto akitaka asonge mbele ni lazima afanye mitihani, afaulu, aende hatua nyingine, hatua nyingine, mpaka vyuoni huko aweze kuhitimu, akifeli mitihani hawezi kwenda huko. Nchi nyingine hawatumii utaratibu huo, kama Ujerumanii na nchi nyingine wana *system* tofauti ya vitendo sisi ni ya mitihani kwa hiyo, lazima mtoto afaulu mitihani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wiki iliyopita nilikwenda Jimboni, najitahidi mara kwa mara nakwenda jimboni, natembelea wapiga kura na safari hii nilitembelea shule. Na nawashauri Wabunge wenzangu mnapokwenda Majimboni, msisahau shule, mtembelee shule, shule za sekondari na za msingi. Kwa sababu, kama shule ina wanafunzi 500 ukaenda pale kusalimia wanafunzi 500, umesalimia jimbo zima karibu kwa sababu, ni kama watu 5,000. Kwa hiyo, nilifika pale nikaona shule zinavyoendelea, nikakuta shule zimefungwa kama ilivyo kawaida sasa hivi ni wakati wa likizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini baadhi ya shule nilizozitembelea nikakuta vijana wa *Form Four* wamebaki. Shule za Kata wamebaki kwa mpango maalum wa kusoma ili waweze kufaulu mitihani. Nilitembelea shule ya Butura ni Sekondari, Shule ya Kaja Sekondari, Katoro Sekondari, Bujuko Sekondari na nyingine nyingi. Hizi zilikuwa na wanafunzi wapo wa Kidato cha Nne wanajisomea, kwa mpango wa kujaribu kufaulu mitihani ya Taifa ya mwezi wa kumi na moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na wanafunzi hawa wana shida nyingi sana. Mtoto anaweza akawa anaumwa hajahudhuria shule au amechelewa kwa sababu mbali mbali, hana *uniform* hajaenda shule, uwezo wa wazazi ni mdogo.

Kwa hiyo, wanaamua kubaki ili waongeze muda wa kujisomea au walimu hawatoshi, kama tulivyosikia humu ndani kila siku walimu wa sayansi na wewe umesema kule kwako walimu wa sayansi ni pungufu. Kwa hiyo, walimu wanaamua kujitolea muda wa ziada, waweze kutoa elimu hii ambayo wanafunzi wameikosa huko nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, ikatokea mtu mmoja Wizarani pale amezuia utaratibu huu. Kaandika waraka kwamba, shule zikifungwa zifungwe hakuna kubaki shule, nikashangaa sana! Hawa vijana wanaobaki shulenii, wanabaki ili wajiandae na mitihani na hawana uwezo wa kufaulu bila kubaki. Na sio kwamba, wana fedha nydingi wanabaki pale wanajitolea na wanakaa mabweni shule za kutwa zile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaingia kwenye madarasa mle, hawana magodoro, wanaweka nyasi chini wanalala, ili wasome waweze kuongeza ufaulu. Walimu wanajitolea kufundisha bure bila malipo, wazazi wanachangia mihogo, ndizi, maharage, ili watoto wale usiku na mchana, wasome waendelee waweze kufaulu. Huyu mtu mmoja Kamishina wa Elimu amezuia utaratibu huo lengo lake silifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachelea kusema ana lengo la kuharibu elimu ya nchi hii na hivyo ana lengo la kuua uchumi wa nchi hii. Watoto wanajitolea, wazazi wanajitolea, walimu wanajitolea. Mtu mmoja anakaa pale Wizarani anaandika waraka anasema hii hairuhusiwi, Serikali, haichangii. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kamishina wa Elimu hachangii. Sasa inashangaza kweli kwa nini anazuia, inamuhusu nini yeye. Kuna mtu mmoja aliwahi kusema kwamba ukitaka kuua Taifa wala usipeleke

sumu kwenye wananchi wale au kuharibu madaraja na barabara wewe ua elimu tu. (*Makof*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ua elimu na utakuwa umefanikiwa kuua Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Ndalichako.

## TAARIFA

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mchangaji kwamba, Wizara jukumu lake pia ni kuwalinda watoto. Kwa hiyo, Serikali haiwezi ikaruhusu mtu sehemu ambayo sio bweni tena amesema watoto wanaweka nyasi, wanalala mazingira yanakuwa ni hatarishi, miundombinu haiko salama kwenda pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimpe taarifa tu kwamba, shule ambazo sisi tumezua ni zile ambazo wanalamisha wazazi kuchanga fedha. Kwa hiyo, suala la kwamba watu wanajitolea sio kweli, wanalamisha na ni kinyume na maelekezo ya Serikali ya elimu bila malipo. Kwa hiyo, nilikuwa nataka tu nimpe taarifa hiyo, ili labda anapochangia aweze kutupatia maeneo mahususi ambayo anayalalamikia, ili Serikali iweze kufanyia kazi vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jasson Rweikiza, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza ulinde muda wangu. Lakini ninachosema ni kwamba, nchi hii inatumia utaratibu wa mitihani, mtu akifeli, amefeli, ameishia hapo ndio mwisho. Kwa hiyo, wazazi na watoto na walimu wanajitolea kusoma

wala hakuna anayelazimisha michango. Niko kwenye sekta ya elimu yaani elimu ndio *system* yangu nafahamu utaratibu wa elimu. Sikutangaza maslahi kwa sababu haina masilahi yangu kifedha, lakini nikoo kwenye sekta ya elimu na ninaelewa vizuri ninachokisema. Serikali inaharibu elimu, Wizara ya Elimu inaharibu elimu kwa hiyo, taarifa hiyo siikubali, naikataa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nasema kwamba, kuna mtu aliwahi kusema, mtaalam wa elimu, mtaalam wa uchumi, mtaalam wa utawala kwamba, ukitaka kuua Taifa, ua elimu. Usihangaike na mambo mengine ua elimu. Huyu Kamishina wa Elimu amekusudia kuua elimu ya nchi hii, haiwezekaniuzuie watu kusoma, watafaulujebila kusoma? Watashindwa mitihani, watapotea, wataishia darasa la saba, wataishia *Form Four* na ndio mwisho wao na watakuwa wanapata zero.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajitahidi watoto wasome, waende mbele, wafike vyuo vikuu na vyuo vingine, wapate stadi mbalimbali vyuo vya ufundi. Lakini hawawezi kufika huko bila kufaulu mitihani yao ya ngazi mbalimbali, ambayo lengo la kufanya hiso kambi na halikuanza leo, tangu enzi hiso. Yeye mwenyewe Waziri ni Profesa asingefikia U-Profesa kama asingefanya hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, amesoma kwa bidii za wazazi, za walimu, za shule mbalimbali, za vyuo mbalimbali. Sasa kwa nini anazuia utaratibu huu ambao ni mzuri, nasema ni mzuri. Kule vijijini hawalipi fedha kwa sababu ya kulazimishwa, wanalipa fedha hiso ndogondogo mihogo hiyo, kwa sababu ya kupenda wenyewe na ndio walioomba. Ni Mbunge wa Jimbo nashiriki kwenye mikutano hiyo, watoto wanaomba, wazazi wanaomba. Wanazuiwa kufanya huu utaratibu ambao nafikiri ni kuua elimu.

Kwa hiyo, tujitahidi na yeye akiwa ndio Waziri wa Elimu, azuie utaratibu huo wa kuua elimu asimamie, ili elimu iwe bora na tuweze kufanikiwa katika mipango yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naomba kuishia hapo. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Prof. Patrick Aloyce Ndakidemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Bahati Ndingo, Mheshimiwa Magreth Simwanza Sitta, ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii, kuchangia kwenye bajeti hii ya Serikali ambayo imeongezeka kutoka triliioni 34.88 hadi triliioni 36.33, ikiwa ni ongezeko la asilimia nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Waziri na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, kwa kuwasilisha vizuri sana hii bajeti yao na ninaomba kabisa nikiri kwamba, bajeti hii imeandaliiwa vizuri sana kimkakati. Na inaleta matumaini makubwa sana kwa watanzania kwenye makundi mbalimbali ambao niseme, wafanyakazi, wafanyabiashara, wakulima, wakinamama, vijana, walemavu, watu wa viwanda, bodaboda na hata wastaaifu wameipokea vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ilioletwa ni nzuri na kusema ukweli inategemea kwenda kulegeza vyuma. Kule mitaani watu walikuwa wanasema kwamba, vyuma vimekaza. Bajeti hii nategemea kwamba, itakwenda kulegeza vyuma na itatupeleka mbele kiuchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii inategemea kuongeza pato la Taifa kutoka asilimia 4.8 hadi asilimia 5.6, inategemea kudhibiti mfumko wa bei ibakie katika asilimia 3 na asilimia 5. Inategemea mapato ya ndani yatafikia asilimia 15.9 ya pato la Taifa na makusanyo ya kodi yanategemea kuongezeka kutoka asilimia 12.9 hadi asilimia 13.5 ya pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii pia, inategemea kama tutaipitisha Waheshimiwa Wabunge, naomba wote tuiunge mkono inategemea kuwa na akiba ya fedha za

kigeni za kutusaidia kuagiza bidhaa za nje kwa miezi minne.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina kila sababu ya kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri wanayofanya. Nianze kwa zile shilingi milioni 500 ambazo mama yetu ametupatia/Rais wetu, kwangu ni fursa kubwa sana. Kwamba, barabara zinakwenda kurekebishwa nchi nzima na niwapi tumeshaona tu Rais anaingia tu na kutupa zawadi kubwa kama hii?  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo langu, hii fedha inakwenda kusaidia sana kwenye ujenzi wa barabara ya TPC, Mabogini mpaka Chekereni. Na kuna fedha ya ujenzi wa shule za Sekondari za Kata nina hakika wananchi wangu kule Moshi, Kata ya Kindi, Kijiji cha Chekereni, Weruweru tunakwenda kujenga shule pale kwa hiyo, ni jambo lenye heri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii pia, inakwenda kupunguza mzigo kwa mfanyakazi, ambapo kodi ya ajira inakwenda kupungua kutoka asilimia 9 mpaka asilimia 8 na hii itaongeza maslahi ya wafanyakazi na pia, kwa wafanyakazi pia kuna bilioni 449 inayokwenda kupandisha watu karibu 92,000 madaraja. Pia niipongeze Serikali kwa kupunguza faini kwa watu wa bodaboda, kutoka shilingi 30,000 hadi shilingi 10,000 ni kitu kizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na pia Serikali inakwenda kubadilisha mabadiliko ya Kanuni ya Sheria ya Bajeti, ambapo kama tutapitisha hakuna tena kurudisha fedha Hazina zitakuwa zinabakia kule na hii ni kitu kizuri. Kuna mambo mengi sana ambayo kutohana na muda sitawenza kuyasema nitawasilisha kwa maandishi. Lakini Serikali vilevile imepania kikamilifu kulinda viwanda vya ndani kwa kuondoa tozo za ushuru wa forodha, katika malighafi za aina mbalimbali ambazo zitaingizwa na zitasaidia kuboresha viwanda vya ndani. Kwa mfano, kwenye kilimo vile vifungashio vya maziwa, mbegu, kahawa, korosho, pamba wameondoa ushuru wa

forodha na hii itachochea watu kufungua viwanda na kufanya biashara hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nina ushauri kwa Serikali. Ushauri wangu wa kwanza ni kwamba, katika bajeti ya Taifa ya trillioni 36.3 asilimia 29.3, ambayo ni sawa na shilingi trillioni 10.66 zitatumika kulipa deni la Taifa. Hizi ni fedha nyingi karibia *one third* itatumika kulipa deni la Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ikiwezekana tutafute vyanzo vingine vya fedha, ili tukusanye fedha nyingi na zitumike kwenye kudhamini miradi mbalimbali. Vile vile ninaishauri Serikali ibuni mbinu mbalimbali za kukusanya kodi kwenye biashara ndogo ndogo. Hizi biashara ndogo zimepanuka sana ni wengi lakini wengi wao hawalipi kodi. Kwa hiyo, mijipange muangalle namna ya kuwakata kodi hawa wafanyabiashara wadogo wadogo, ambao wanaweza wakachangia sana katika pato la Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaishauri Serikali iendelee kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje. Ii tupanue wigo wa kuwaajiri watu wengi zaidi na tukishapanua wigo wa kuajiri watu wengi vile vile tutapata kodi na tutaongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inategemea kukopa ili *ku-support* miradi ya maendeleo na inategemea kukopa shilingi trillioni 7.34 ili kugharamia miradi ya maendeleo. Katika hizi shilingi trillioni 4.99, zitatoka kwenye Taasisi za ndani kwenye Mabenki ya ndani au Taasisi nyingine za ndani na shilingi trillioni 2.35 zitatoka nje.

Nilifikiri ilitakiwa iwe *the opposite* kwamba, nyingi tukope kutoka nje na kidogo tukope ndani, Ili tuwaachie wafanyabiashara wa ndani waweze kukopa kutoka kwenye Mabenki yetu. Kwa sababu tunawaminya wafanyabiashara wa ndani hawana mahali pa kukopa na hiyo inasababisha wasiweze kuwekeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili, ni kuhusu ushirikishaji wa sekta binafsi katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo. Kwenye ule Mpango wa Pili, ni ukweli usiopingika kwamba, Serikali haikuishirikisha sekta binafsi sana kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo. Kazi nydingi zilikuwa zinafanywa na Serikali, Taasisi za Serikali kwa mfano, mikutano ya Kiserikali tulikuwa tunaambiwa twende *VETA* tusiende kwenye hoteli nydingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya aina mbalimbali walikuwa wanafanya Taasisi za Serikali. Kwa hiyo, sekta binafsi ilipwaya sana walikuwa hawaajiri. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali kwenye Mpango wa Tatu huu, sekta binafsi wameshajifunza kwamba, kama kuna kitu walifanya makosa sasa hivi watarekebisha na tuwashirikishe ili waweze nao kushiriki kwenye ujenzi wa Taifa lao na kulipa kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwisho na ushauri wangu wa mwisho kwa Serikali ni kwenye sekta ya kilimo. Wabunge wengi hapa walilia sana kwamba, kilimo hakijatendewa haki. Lakini mawazo mengi yalichukuliwa ila la kilimo pamoja na kwamba, karibu kila Mbunge alisema bajeti ya kilimo ni ndogo halikubebwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri, ikiwezekana kwenye ile bajeti ijayo tunajua hili hatuwezi kulifanya kitu kikubwa lakini kwenye ile bajeti ijayo tujitahidi kilimo, mifugo, wapate fedha za kutosha kwa sababu sehemu kubwa ya watanzania ni wakulima na wanahitaji kusaidiwa. Tukishapanua kilimo tunauhakika kabisa kwamba tuta-*improve productivity*na watu watapata kipato cha kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bahati Kenneth Ndingo, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kupata fursa nami niungane na Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuipongeza Serikali ya Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa bajeti yake hii ya kwanza, nzuri kabisa ambayo imepokelewa kwa bashasha kubwa huko mtaani. Lakini pia niendelee kuipongeza Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kutuletea bajeti ambayo inakuwa ni chachu ya maendeleo kwa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kuongeza vyanzo vya mapato ya ndani. Tunaona bajeti hii inayokwenda kuisha tarehe 30 Juni, tulikuwa na vyanzo vya mapato ya ndani kwa asilimia 69, sasa kwenye bajeti hii tunatarajia kuwa na vyanzo vya mapato asilimia 72. Kwa hiyo ina maana tunakwenda kupunguza utegemezi wa bajeti na mikopo ya nje na wahisani kwa asilimia tatu. Siyo kazi ndogo niwapongeze sana kwa ubunifu wa kuibua vyanzo vipyta vya mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakubalina na mimi na Waheshimiwa Wabunge ni kwamba kwa takribani miaka mitano iliyopita kuanzia 2014 mpaka 20219 Halmashauri zetu bado zimekuwa na changamoto ya kuweza kupata mapato ya kutosha. Kwa hiyo tumekuwa tukiipa Serikali Kuu mzigo mkubwa kwenye Halmashauri zetu. Tumeona kwamba kwa takriban kuanzia mwaka 2014 mpaka 2019 zaidi ya asilimia 85 ya Halmashauri zilishindwa kujigharamia matumizi yake ya kawaida. Hivyo zilipelekea kwamba Serikali Kuu iendelee kuzisaidia hizi Halmashauri. Kwa hiyo, utaona kwamba bado Serikali Kuu ina mzigo mkubwa ambao ni lazima kama Taifa tuje na mbinu mbadala za kuendelea kutafuta vyanzo vya mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kuishauri Serikali, niliona katika Mpango wa Pili wa Serikali mliongelea Hati Fungani za Manispaa (*Municipal Bonds*) lakini pia niliona katika bajeti ya mwaka 2018/2019 Mheshimiwa Waziri wa Fedha kipindi hicho ni Makamu Rais sasa, alisisitiza kuendeleza Mpango ule wa kuanzishwa kwa Hati Fungani za Manispaa,

ilielezwa Bunge lako Tukufu kwamba mmekwenda kufanya *training* karibia Manispaa ya Mwanza, Arusha na nyaginezo na Tanga. Sasa, naona hili jambo pia limekuwa kama linasinzia. Hii nchi ni kubwa lazima tubuni halmashauri hizi zijiendeshe kibiashara. Tukisema halmashauri zote nchini ziweze kujiendesha kwa kutegemea Serikali Kuu tutakuwa tunajidanganya. Kwa hiyo niombe sana Serikali iweke mkazo kwenye kuhakikisha wanamalizia uanzishwaji wa hizi Hati Fungani za Manispaa au *Municipal Bonds*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana, kwenye bajeti tukatoe kipaumbele kwenye miradi ambayo itakwenda kuchochaea uchumi kwa haraka. Leo hii tuna mradi mkubwa unakwenda kuanza wa Liganga na Mchuchuma lakini kama Serikali imeandaa mazingira ambayo yatakuwa wezeshi kwa mradi huu kutopatikana kwa vikwazo. Barabara zipo, miundombinu rafiki kwa ajili ya mradi huu ipo? Ni vitu ambavyo kama Serikali lazima tuhakikishe tunatoa vipaumbele kwenda kutekeleza bajeti yetu kwenye vyanzo ambavyo vitakwenda kuchochaea uchumi wa Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukienda kule kwenye barabara za huko vijijiini utaona jinsi kuna uwekezaji mkubwa kwa mfano, kuna uwekezaji mkubwa ulifanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu kule kwetu Madibila, Mbarali. Waliwekeza zaidi ya bilioni 28 lakini leo hii hata barabara kufika kwenye yale mashamba hakuna. Ni jinsi gani Serikali inapoteza mapato kule kwa kukosekana tu barabara ile barabara ipo tangu Serikali ya Awamu ya Tatu imeahidiwa kwa wananchi kilomita 151 kutoka Rujewa, Madibila mpaka Mafinga kule kuna wakulima wa mbaو, kuna uwekezaji mkubwa Serikali imetengeneza skimu za umwagiliaji kubwa lakini hakuna barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana Serikali, leo hii langoo kubwa la biashara kwenye nchi za *Southern Africa*, Kusini mwa Afrika, (*SADC*) leo hii langoo kubwa la biashara ni kule, barabara ile haifai kutoka pale Igawa mpaka Tunduma ni shida. Kwa hiyo, ni lazima kama Serikali

tutoe vipaumbele kwenye maeneo ambayo yataweza kuchochea uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze TAMISEMI kwa kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge katika miradi mbalimbali inayoendelea. Niombe sana na Wizara nyingine zifanye hivyo kama Wizara ya Ujenzi wakae na Waheshimiwa Wabunge, Wabunge hawa wanajua barabara ambazo zitakwenda kuchochea uchumi kwenye Majimbo yao. Kwa hiyo niwaombe sana na Wizara nyingine muwape kipaumbele Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo yao ili wawewe kujadiliana nanyi na kuwapa kipaumbele ambacho kitasaidia kujua ni nini kipaumbele cha vitu ambavyo vitachochea uchumi katika maeneo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana kwa kupata fursa, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Margaret Sitta atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo mezani. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na wakati huo huo nawashukuru sana wananchi wa Urambo wakiwamo Ndugu zangu kwa ushirikiano wanaonipa mimi katika kutafuta maendeleo ya eneo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, akiwemo Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa jitihada zao kubwa ambazo zimetuletea hii bajeti ambayo tunajadili siku ya leo. Hongera sana Serikali kwa bajeti nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Urambo tumenufaika pia na bajeti hii tumehakikishiwa maji yatakuja, barabara zitatengenezwa, umeme utafika kwenye vijiji vyote.

Ombi letu kwa siku ya leo ni kwamba lini mafundi watafika Urambo kuhakikisha kwamba ule mradi wa maji unaotoka Lake Victoria unaanza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo ni muhimu sana katika Wilaya yetu kwa sababu tunategemea sana zao la tumbaku ili lituwezeshe kumudu maisha kwa upande wa biashara. Nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa sababu imetambua kwamba kuna umuhimu wa kufanya vikao na wanunuzi wa tumbaku. Kwa sababu kilio chetu kikubwa ni kuongeza makisio, wakulima wanapenda walime kadri wanavyoweza kwa hiyo tunapopata makisio makubwa yanatupa nguvu na sisi ya kulima zaidi. Kwa hiyo naipongeza Serikali kwa kitendo chake cha kukutana na wanunuzi mwaka jana mwezi Februari, 2020. Serikali kwa kuitia wizara ya fedha na wakati huo alikuwa Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Phillip Mpango ambaye alikutana na wanunuzi wa tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba utaratibu wa kukutana na wanunuzi uendelee kwa sababu kikao cha mwaka jana mwezi Februari, 2020 kilizaa matunda tukaongezewa makisio kutoka tani elfu 36 hadi kufikia tani 67 elfu. Kwa hiyo vikao tunaomba viendelee vyta kukutana na wanunuzi, kwanza vinawapa nguvu wale wanunuzi waliopo lakini pia kinatoa fursa ya kujadili tozo mbalimbali, changamoto wanazokutana nazo ili weendelee kununua tumbaku. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iendelee na utaratibu wa kukutana na wanunuzi, tunategemea kwamba wanunuzi watakapokuwa wengi kwanza watatoa makisio zaidi lakini pia kutakuwa na changamoto ya kuongeza bei, kutakuwa ushindani wa bei, kwa hiyo tutanufanika zaidi. Hivyo, utatatibu wa Serikali kukutana na wanunuzi tunaomba uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii tumeionna ina bilioni 294 zikiwepo bilioni 30 za umwagiliaji. Lakini Serikali inajua, kwamba kuna Azimio la Maputo ambalo walikuwa wamekubaliana kwamba kutenga asilimia 10 ya bajeti nzima iende kwenye kilimo. Tunajua kwa mwaka huu haiwezekani kwa sababu tayari wameshatenga bilioni 294. Ombi sasa kwa

Serikali kweli kwamba zile bilioni 294 basi zipatikane ziende kwa kilimo, fedha zote zilizotengwa ziende kwenye kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuipongeza Serikali kwa kuondoa VAT kwa upande wa *cold rooms* vyumba nya kuhifadhi baridi ili watu wanaosafirisha mazao nje, maua na mazao mengine yanayotokana na *horticulture* wapeleke. Tunaipongeza Serikali kwa suala hilo lakini tunaomba basi Serikali ituambie kwamba ina vituo vingapi nya kuhifadhi baridi yaani *cold rooms*. Na je, ina mpango wa kuongeza, kama ina mpango wa kuongeza inaongeza vyumba vingapi ili wenzenetu wanaosafirisha bidhaa nje kwa kutegemea hivyo vyumba basi na wenyewe wanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilombe Serikali imeweka asilimia mbili ya Kodi ya Zudio. Tunaomba hii kodi asilimia mbili iondolewe kwa upande wa mazao ya wakulima ili waweze kupelekea mazao yao vizuri zaidi. Naiomba Serikali kwa kuwa ina mpango wa kuongeza zao la alizeti, sisi kama Mkoa wa Tabora nasi pia tunalima alizeti, tunaomba tuongezwe kwenye mpango wa kuongeza zao la alizeti ili na sisi tuliwe kwa sababu tunajua kwa sasa hivi zao la alizeti ni muhimu katika upande wa kuongeza mafuta kama tunavyoona sasa hivi mafuta yamepanda bei sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Serikali kwa ujumla mimi mwalimu, ningependa sana nizungumzie suala la elimu naona sintatenda haki bila kuzungumza suala la elimu. Nampongeza Mheshimiwa Prof. Ndalichako nimemuona kwenye vikao vingi sasa hivi anatafuta maoni na jinsi gani ya kuboresha elimu nchini. Ni jambo zuri sana, nakupongeza kwa sababu sisi wote tumeomba Serikali ifanyie kazi suala la elimu ili liende na wakati llijbu hoja na mahitaji ya kipindi hiki. Lakini mimi nilikuwa namuomba Mheshimiwa Prof. Ndalichako na Wizara ya Elimu kwa ujumla iangalie uboreshaji wa elimu lakini iwaanglie na Walimu. Kwa sababu huwezi kuboresha suala la elimu bila ya kuangalia Watendaji, sasa hivi tumeona walimu wana changamoto nyingi sana,

wengi hawapandi madaraja kwa wakati na wengine wanapanda madaraja lakini mishahara yao hairekebishwi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi ningeomba Serikali iwachukue wale wote ambao wana mhudumia Mwalimu kwa sababu Mwalimu hahudumiwi na mtu mmoja anahudumiwa na vyombo vingi sana. Kwa hiyo mimi ningeomba kuwe na kikao cha kuangalia wote wanaomuhudmia mwalimu wanafanyaje yaani kuwe na *co-ordination* ili walimu waweze kupata haki zao kwa wakati na waweze kufanya kazi kwa bidi zaidi hata baada ya kuletewa maboresho hayo. Kwa mfano nilikuwa naangalia suala la *TSC* ilipoundwa ilikuwa na malengo gani? Mimi nilikuwa nategemea kwamba *TSC* itasaidia kuleta *co-ordination* yaani itaunganisha vyombo kwa pamoja ili mambo ya upandaji wa madaraja, kama ni kuchukuliwa hatua za nidhamu na vitu vya namna hiyo, lakini je, najiuliza *TSC* ilipoundwa na ikapewa majukumu yale kweli ndiyo tunachotegemeWa. Matokeo ya utendaji kazi wa *TSC* ndiyo yale tuliyoyatategemea baada ya kuomba iundwe? Kwa hiyo naomba *TSC* ifanyiwe tathmini kama kweli inafanya kazi iliyokusudiwa ya kurahisisha huduma kwa Walimu ambao ni walengwa. Wakati huo huo, pamoja tukija na maboresho ya elimu lakini pia tuangalie suala la ukaguzi. Je, ukaguzi inafanya kazi inavyopaswa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba nimalizie kwa kuzungumzia suala la posho kwa Watendaji wa Kata. Naipongeza Serikali kwa kwa Watendaji wa Kata wamefanya vizuri sana lakini niilombe pia na Watendaji wa Vijiji na Mitaa waangaliwe. Kwa sababu wao nao pia wanasaidia kuhamasisha suala la uchaguzi, sensa inakuja watatumika, masuala ya usalama, kwa hiyo naomba pia Watendaji wa Vijiji nao waangaliwe wapate posho kama walivyopata wenzao wa upande wa Kata. Itasaidia kuwapa motisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia *data*, nikaangalia kuna vijiji 12,319, mitaa 4,263 wakichanga na wale Watendaji wa Kata 3,956 naamini Serikali inaweza,

penye nia pana njia. Naipongeza sana kwa bajeti hii lakini naomba narudia tena kuomba watusaidie sana suala la kilimo kwa sababu kilimo ndiyo Utii wa Mgongo. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mheshimiwa John Marko Sallu ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza ninarejea hotuba ya Waziri ambapo katika ukurasa mmojawapo ulihamisha jukumu la uwekaji vinasaba kwenye mafuta ya petroli kutoka kwa Mkandarasi binafsi na jukumu hili ukalipa Shirika la Viwango la Tanzania. Sasa Mheshimiwa Waziri nataka wakati unajibu utueleze namna gani fikra kama hii ambayo kutokana na mikata milovu na hovyo kabisa ilisababisha Mkandarasi binafsi kwa mwaka kupata zaidi ya bilioni 68 kwa miaka nane aliyokuwepo zaidi ya bilioni 490. Umefanya jambo la busara kuondoa hilo jukumu kuipa taasisi ya Serikali ili haya mapato basi yaweze kuingia Serikalini na hata mkipunguza gharama yakiwa kwa kiwango kidogo vilevile yaweze kuingia Serikalini, hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka uniambie Mkandarasi huyu ambaye amepewa jukumu la kubandika stempu za *ki-electronic* ama *ETS*, kwenye bidhaa zinazozalishwa Nchini kwa ajili ya kutoza ushuru wa bidhaa mkataba wake utakoma lini ili hili jukumu ambalo amepewa Mkandarasi huyu kipewe ama chombo cha Serikali ama mfanye ushindani upya aweze kupatikana Mkandarasi kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza juu ya mafuta, sasa nitazungumza juu ya *ETS*. Kwa maelezo ya Serikali huu utaratibu ulianza mwaka 2018, maana tunaofikiria kipindi kile mambo yalikuwa *perfect* sana, lakini siyo kila kitu ni *perfect* kuna sehemu tunakosea na lazima tujirekebishe. Lengo lake lilikuwa ni jema kuweza kutambua bidhaa, kuzuia watu wasikwepe kodi, Serikali iweze kupata kodi yake stahiki,

jambo ni jema. Lakini għarama, tunaambiwa mpaka sasa hivi wazalishaji ambao wamefungiwa hima mashine wako 245, waagizaji 86. Sasa mafanikio ni nini! Kwa sababu kwa petroli ilikuwa akiweka kale kadude lita moja shilingi nane, huku kwenye bidhaa za vinywaji, vinywaji vikali na vyepesi na masigara na kadhalika kuna shilingi nane kwa mantiki ya dola nane na dola 20 kutegemeana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mafanikio ni nini kabla ya *ETS* na baada ya *ETS*. Kwa maelezo ya *TRA* kabla ya *ETS* tulikuwa tunakusanya shilingi bilioni 237 baada ya *ETS* tumekusanya shilingi billioni 246. Tafsiri yake ni nini, tofauti ninyi mnajua bilioni 46 toa bilioni 37 ni bilioni nane. Sasa għarama ambazo Makampuni yetu yanaingia kutokana na huu mchakato ni nini? Taarifa ya *TBL* ambao ni walipa kodi wakubwa nchini, wanassema katika kipindi cha miaka mitatu wanatarajja, kuanzia mwaka 2019 mpaka 2021 watamlipa Mkandarasi shilingi billioni 94 kampuni moja, hapo nimesema makampuni ambayo ama viwanda viliunganishwa ni zaidi ya 250, wakati *TRA* nyongeza yao ni kutoka bilioni 237 mpaka bilioni 246 *different* ya *eight billion*. *TRA* wakatupa *data* zao za mvinyo wa ndani, kabla mtambo wa *ETS* shilingi milioni 657 baada ya *ETS* on average imeongezeka mpaka bilioni 3.4. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha pili ni cha sigara, mmeshataja TBA hapo. Mkandarasi binafsi kalipwa na TBA bilioni zaidi ya 90. Serikali nyongeza mlifikiria kuna *cheating* kubwa mmepata shilingi bilioni nane. Hivi, tukisema hii ni busara, hii ni busara...

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa, taarifa!

**MHE. HALIMA J. MDEE:... TCC**

## **TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee kuna taarifa kutoa kwa Mheshimwa Kenneth Nollo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Alikuwa ni Nyongo hapa nimeomba taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Aah nani alisimama kwanza, kwa sababu mimi nilimuona ye ye kwanza ambao wote wawili mmesimama.

**MHE.KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa naibu Spika, nilianza mimi.

**NAIBU SPIKA:** haya.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mi nataka nimpe taarifa mzungumzaji. Nadhani anajaribu kutoa *opinion*, tangu kule alivyosema kwenye mafuta na hata huku. Na kitendo cha kuanza kutaja kampungi hii inalipa *this amount, this amount* ni kama anataka kusema kama kuna uonevu. Kwa hiyo hoja yake ya msingi hapa angejaribu kusema hapa labda *alternative* kwamba tutafute kampuni nyengine lakini anachokifanya hapa ni kwamba hawa wanalipa kiasi hiki, *as if* watu wanaonewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nimpe taarifa, anajua mchakato mzima tulivyompata mtu wa kuweka *stamp* za *TRA* na liliyokuwa jambo gumu. Kwa hiyo kinachotakiwa aelewe kwamba hiyo *opinion* anayoitoa ni kutafuta suluhu ya namna nyngine na asifanye kama kuna kuibiwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokizungumza hapa sina tofauti na alichokizungumza Mheshimiwa Tabasam *the other day* kuhusiana na utaratibu huu huu kwenye mafuta; hakuna tofauti na alichokizungumza mbunge wa Gairo, kuhusiana na utaratibu huu huu kwenye mafuta. Na tunazuzngumza hapa ili kuiambia Serikali kupitia wataalamu wetu; na nilisema hapa, dhamira ya ilikuwa ni nini njema, kuweza kujua bidhaa zinazozalishwa, lakini

dhamira njema mkijua kwamba mlchemka mnatakiwa mnakaa mnajitathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa mfano kwamba, tulimchukua mkandarasi ...

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee kuna taarifa kutoa kwa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimwai Naibu Spika, napenda tu kumtaafu Mheshimiwa Mbunge, kwanza kabisa yeye mwenyewe ni mjudje wa Kamati ya Bajeti, na haya yote yamepita kwenye kamati ya bajeti. Nkuhusu suala la ETS imekuwa *raised* kwenye Kamati ya Bajeti na Serikali imekuwa ikisimamia na kupambana na suala hili ili kuhakikisha kwamba inakuwa na faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine na cha mwisho, ameonesha kama kuna *difference* ya *eight billion, difference* ilikuwa ni kubwa, nia ilikuwa ni njema kama anavyosema, sema kiwango kimekuwa kidogo. Yeye akubali, na yeye ni mjudje wa Kamati ya Bajeti aendelee kuishauri Serikali vizuri kuliko kushutumu watu wengine wamechemka ilhali na yeye mwenyewe ni sehemu ya kuchemka. Ahsante sana. (*Makofî/ Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi sikuchemka kwa sababu mimi sikuwa sehemu ya mkataba uliotengenezwa wala hata siujui. Pili kuwa mjudje wa Kamati ya Bajeti hakunizui mimi kuchangia bungeni, na nimelichangia hili ili kutambua hatua ambayo Serikali imechukua kwa kuondoa jukumu la vinasaba kwa mtu

binafsi, imerudishwa Serikalini, kwa hiyo pesa inarudi Serikalini.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ninaitaka Serikali; na uzuri Mheshimiwa Mwigulu anasikiliza, nataka Mhesnishiwa Mwigulu hili la *ETS* ultioe huko kwa mkandarasi aliyepo sasa, kwa sababu tumeshapigwa vya kutosha, turudishe ama Serikalini, na kama Serikali haina teknolojia ya kutosha tufanye ushindani watu waje tupate mtu mwenye gharama nafuu.  
*(Makofi)*

Meshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha pili cha sigara, kwa mwaka mmoja kimelipa bilioni 14, kiwanda kimoja. Tukizungumza hivi viwanda vidogo vidogo ni bilioni tatu biloni nne, bilioni nane; ukijumlisha unaweza ukakuta wakati *TRA* mmeongeza si pungufu ya bilioni 20, mwenzenu huku kwa vile viteknolojia vya kudonoa donoa tu na kuweka nembo, amepata bilioni 400 labda, hivi hii ni busara. Mheshimiwa Mwigulu Nchomba, nitakuomba tu unijibu kwa sababu kiukweli tunapigwa pigwa sana, na si busara kukubali kuendelea kupigwa pigwa, na mimi najua wewe hupendi tupigwe pigwe. *(Makofi)*

Meshimiwa Naibu Spika, la pili. Mpango wa kwanza na wa pili tulifeli kwa sababu, kwanza hatukuwa na mtiririko wa fedha za kutosha, pili hatukuwa na takweimu za kutosha. So, mimi ninasikiliza ndugu zangu Wabunge hapa, kila mtu anasema Bungeni hapa, ooh sijui jimboni kwangu inakuja milioni 500, tunapiga makofi, yaani tunawahisha shughuli. Lakini Nheshimiwa Mwigulu unajua, kwamba kwenye bajeti yako wewe ambayo tunaimaliza sasa ni ya mtangulizi wako. Tulipanga kwa miaka hii yote kwa mikopo kwa mambo yetu yote ya ndani tuweze kukusanya trillioni 34. Juzi hapa unatusomea hotuba yako umeweza kukusanya trillioni 24, kuna *deficit* ya trillioni 10. Hivi kweli nisaidie; ni muujiza gani huu utakufanya Mheshimiwa Mwigulu na Serikali muweze kukusanya 10 trillion ndani ya miezi miwili? Pili, kama unajua ulishindwa mwaka jana hivi kweli ni busara kwenda kusema kwamba unaweza kukusanya trillioni 36, hivi ni busara?

Meshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu Wabunge wadogo zangu asilimia 70 hapa ni wageni, hizo 500 msipige kofi, tutakutana mwakani hapa tutaanza kutoana macho. Kwa sababu kwa mtindo wa ukusanyaji wa aina hii, naomba Waziri uje utuambie kuna miujiza mengine itakayokuja, lakini kwa utaratibu huu, siku zote nawaambieni tukiwa wakweli kama unauwezo wa shilingi mia, jipangie kwa shilingi mia yaki ili sasa tuendelee kuishi kwa matumaini, sio unaweka shilingi mia unakusanya buku unasema mimi naweza kukusanya elfu moja, wakati unajua ndugu yangu mia ndio saizi yako...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** haya ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee muda wako umeisha ahsante sana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** .... Kwa hiyo tuwe wakweli tuweze kulisiaidia taifa hili. Nitaomba majibu mahsus kwa ETS...

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa Halima Mdee, ahsante sana, shukran.

**MHE. HALIMA J. MDEE:**... nashkuru sana. (*makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee ahsante sana, shukran. Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga akifuatiwa na Mheshimiwa John Marko Sallu, Mheshimiwa Taufiq Salum Turkey ajiandae.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kutoa na mimi mchango wangu.

Meshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu na kumpongeza kwa kazi nzuri ambazo anaendelea nazo, na kwa kweli kimsingi kwenye hili nimpongeze sana kwa hatua ambaeo Mheshimiwa

Rais ameichukua ya kuteua wakuu wa Wilaya kutoka kwenye makundi mbali mbali, hongera sana. (*Makofi*)

Meshimiwa Naibu Spika, hizi siasa wakati mwengine huwa zinatufanya kama vile tunakuwa na hamaki hamaki halafu baadaye tunarudi kwenye mstari.

Nilikuwa naomba tu kumwambia ndugu yangu Mheshimiwa Halima Mdee, kwamba kati ya mambo licha ya kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ilikuwa anaelezea kwamba si mambo yote yalikuwa *perfect* kwamba mambo mengine yalikuwa na dosari, mimi nakubaliana nae. Lakini nataka nimwambie kubwa zaidi ambalo hatakiwi kulisahau, kwamba *perfect* kuliko yote ni wao kuendelea kuwepo hapa Bungeni. (*makofi*)

Meshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumpongeza Waziri huyu wa Fedha, kaka yangu Mwigulu, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa wizara hii, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. Bajeti hii ni bajeti ambayo kwa kweli wananchi wengi wanaipokea *positive*, ambacho wanakitaka na tatizo kubwa la wananchi; Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema kwamba Watanzania tufunge mikanda. Mimi nilikuwa naomba kumwambia Mheshimiwa Waziri, kwamba Watanzania hawana tatizo la kufunga mikanda, matatizo yao yapo kwenye maeneo mawilili tu. Ni kwamba wananchi wafunge mikanda lakini kinachopatikana kitumike kule ambako kunatakiwa kutumika. (*Makofi*)

Meshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwengine wa pili, ni kwamba wananchi wanasema wapo tayari kufunga mikanda lakini kusiendelee kuwepo na mianya ya upotevu wa pesa katika maeneo mbali mbali. Kwa hiyo hayo yakienda sawa sawa kwa kweli Watanzania hawana wasi wasi na wapo tayari kufunga mikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo mimi ningependa kushauri hapo, zipo njia ambazo Serikali imesema inataka kuongeza matumizi ikiwemo utaratibu mzima wa kupata fedha kwa njia ya kodi, kwenye simu, kwenye

majengo na kadhalika. Sasa mimi naomba kuuliza, hivi tangu siku ile bajeti imesomwa hapa ni nini kinaendelea huko chini kwa watendaji wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tusipoangalia, Mungu atajaalnia, najua kesho bajeti hii itapita. Tusipoangalia tunaweza kujikuta hapa tumekaa tumeponga vizuri lakini baadaye kutakuwa na kero kubwa sana kule chini kwa wananchi. Nilikuwa naomba Wizara zote za Serikali katika maeneo yote ambayo Wizara zote zitaguswa, na hasa pia kwa wananchi wale ambao watakuwa ni wamiliki wa nyumba (wenye nyumba), Serikali iweze kuwa na utaratibu wa haraka na utaratibu mzito sana na wenye kutilia mkazo ili kwamba mambo kule yaweze kwenda sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa sababu, ninajua watendaji wetu walivyo. Mpaka sasa hivi kule chini baadhi ya watendaji kwenye baadhi ya maeneo kumeanza ile kama kuamka amka wameanza kukimbizana kimbizana, hatuna *data base* ya vitu vingi. Sasa hivi hata ukiuliza tuna nyumba ngapi kwenye maeneo fulani watu bado hawana. Sasa vitu kama hivyo kama huna data ya vitu ufuatiliaji wake na utekelezaji wake utakuwa ni ule wa kukamatana, kushikana na kadhalika, Itasababisha *chaos* nydingi sana. Ndiyo mana nasema kwamba wenye nyumba, na ndiyo mana nasema Wizara nyengine zote tufanye kazi kwa pamoja kuhakkisha mambo haya mengine hayawezi kutokea.

Meshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka niliseme, kwenye kurasa wa 117 wa hotuba unasema, kwamba nchi yetu baada ya kuingia kwenye nchi ya uchumi wa kati wa chini, itaifanya nchi yetu kutakiwa kuijendesha kiuchumi bila ya kutegemea kwa kiwango kikubwa misaada na mikopo yenye masharti nafuu, ambayo hupewa nchi zenyе kipato cha chini.

Meshimiwa Naibu Spika, hili nilikuwa naomba niseme, kwamba humu ndani tangu watu wameanza kuchangia hakuna mbunge ambaye hajasimama au ambaye hawez

kusema kwamba kwake kuna matatizo ya maji. Hata kama hajasema maji, kwenye masuala ya pembejeo, na kama hatasema embejeo atazungumzia masuala ya barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inahitaji pesa, sasa tunapataje pesa hizo? Mimi nilikuwa naomba tuwe na njia mbili. Mheshimiwa Rais wetu ameanza vizuri sana, kwamba tusijifungie, ameanza kufungua; na kwe kweli niwapeni Habari njema, hata sasa hivi baadhi ya wafanyabiashara Kariakoo wanasema tunamshukuru Rais wetu, mambo yamebadilika. (*Makofii*)

Meshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kusema hivyo, kama nchi yetu inatakiwa pesa, ziko pesa ambazo zitapatikana, kwa maana ya Serikali kutafuta pesa kwa kutumia vyanzo mballimbali, lakini ziko pesa nyengine ambazo zitapatikana kwa hizi nafasi ambazo Serikali imeachia ili watu waweze kufanya shughuli zao kama kawaida, kwa kuwawezesha wananchi. Sasa mimi nilikuwa naomba kuishauri Serikali. Yapo mashirika ya wenzetu hapa duniani ambayo yanatoa mikopo kwa riba nafuu.

Nilikuwa naomba Serikali yetu, najua sasa kwamba sasa hivi imejifungua, kuna mashirika ya kiarabu bila ya kujali masuala ya itikadi za dini, twende tukajaribu kuangalia huko kwa wenzetu wana mashirika ambayo yanatoa misaada kwa riba nafuu sana sana. Kwa sababu tunachokitaka, hata kama watu watasema kwa sababu nyengine zozote, tunachokitaka hatuangalii mambo mengine sisi tunaangalia ni jinsi gani tutaweza kuwasaidia wananchi wetu.

Meshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuwawezesha wananchi kiuchumi. Mimi nilikuwa naomba Watanzania na watu wengine ndugu zangu tusiwachukie wanfanya biashara, tusiwachukie wafanyabiashara kwa sababu mfanya biashara au mtu mmoja akipata ile *chain ikishuka* mpaka chini watu wengi wananaufaika na mfanyabiashara huyo na kwa hiyo uchumi wa watu utakuwa mzuri kuanzia chini mpaka juu.

Meshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa sababu ninaomba sana Serikali tuweze kubadilisha utaratibu wetu wa jinsi ya kufanya kazi, tuwawezeshe Watanzania. Hivi kuna ubaya gani kwa Mtanzania mtu ametoka huko nje amekuja hapa kuwekeza, wakati wa *tender evaluation*, tukasema kwamba tunataka walau mtu akitoka nje awe walau na Mtanzania. Kwasababu kwa kufanya vile na tukiwapa masharti hayo yataweza kuwasaidia na Watanzania wenzetu. Kuna wakandarasi, kuna watu wanauwezo mkubwa sana wa kufanya hizo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi hebu niulize, Stiegler's Gorge Mtanzania anafanya kazi pale? Najuwa watu watasema wapo lakini anafanya kazi gani? Huku kwenye daraja la Kigongo Busisi jiulizeni Mtanzania anafanya kazi gani? Tukiangalia kwenye maeneo mengine, hata hilo daraja la Tanzanite, pale *Salender Bridge*, tuangalie Watanzania wanafanya shughuli gani? (*Makofii*)

Meshimiwa Naibu Spika, tukiwawezesha wananchi kiuchumi, itasaidia Watanzania hao wakiingia huko kupata si tu fedha pia na ujuzi. Siku nyengine Serikali hata ikisema inataka kufanya mradi mkubwa watu wa kufanya kazi hizo watakuwa wameshaingia, wamepata uzoefu na wao wanashiki kuendeleza shughuli mbali mbali za uchumi wa nchi yetu.

Meshimiwa Naibu Spika, tukiendeleza kusema wawekezaji wanakuja mtu anakuja na mitambo yake na ucjuzi wake anafanya, Mtanzania kazi yake iwe kupeleka *cement* na kupeleka kokoto, hatuwezi kuwawezesha Watanzania kiuchimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala linguine, kwa sababu ya muda, suala la *ranch* za taifa. Ninaomba kuishauri Serikali, ninafahamu kwamba kuna baadhi ya *ranch* za taifa, bado hatufanyi vizuri. Lakini na ninaomba niseme hivi, hata hizi dhahabu na madini mengine yote haya; kuna wakati Mwalimu Nyerere alisema tuache kwanza mpaka pale tutakapokuwa tayari. Si kila ardhi kwenye hii nchi ni lazima

itumike kwa ajili ya matumizi mengine yeyote. Mimi nilikuwa naomba hata, kama hizi *ranch* hazifanyi vizuri lakini tuwe makini sana sana, hatuwezi kujua zitatusaidia lini na kwenye jambo gani. (*Makof*)

Meshimiwa Naibu Spika, lingine nizungumzie suala zima la biashara. Kama ambavyo nimesema kwamba wananchi wawezeshwe kiuchumi; Wizara ya Viwanda na Biashara, unajua wakati mwengine kuna mambo yanakuwa yanafanyika watu wengine wanakaa wanapanga mambo makubwa halafu huku nje wapo ambaao wanakuwa kama hawapo, yaani kama tunachokiongea wao hakiwahusu. Ninasema hiyyo kwasababu, kama tumekaa tumesema kwamba tukae tuijandae kiuchumi tuwe na bajeti tutafute pesa, tupate pesa kwenye kodi na kadhalika.

Meshimiwa Naibu Spika, ninafahamu kaka yangu Waziri wa Viwanda na Bisahara unafanya kazi nzuri sana pamoja na Naibu wake. Wizara ya Kilimo kaka yangu Waziri wa kilimo pamoja na kaka yangu Bashe wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mashirika pale Wizara ya Viwanda, kama *CAMARTEC*, wapo pale, hivi mimi naomba kuuliza wanafanya nini? *CAMARTEC* kimsingi ukiangalia kwenye muundo wao, mimi nimeusoma, wanatakiwa waje na ubunifu kusaidia maendeleo katika sekta mbali mbali za kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule vijijini wananchi mpaka leo wanatumia majembe ya mkono, na wao wapo, majembe ya mkono yapo, hata kuwasikia huwasikii. kuna *TANTRADE* ambaao kimsingi wanatakiwa wawawezeshe wafanyakibashara wa ndani na nje, lakini leo hii *TANTRADE* Mama Samia au Waziri aende pale Kariakoo aende akaangali jinsi gani biashara zinafanyika, kwenda tu kuangalia hawaendi, wanafanya nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *TIRDO*, kuna *SIDO*. Walau *SIDO* wanajitahidi, wanafanya kazi mambo

yanaonekana, kuna *TEMDO*, lakini kuna hizi taasisi nyengine ambazo ukiwaliza mnafanya nini hawajui wanachokifanya na wapo wanapata mishahara kwa pesa za Serikali. Nilikuwa naomba Wizara hii ya Viwanda na Biashara, waweze kuamka, hivi vishirika shirika na viataasisi taasisi hivi, Serikali iweze kuviangalia waliundwa kwa sababu ya nini, ili tukjua waliundwa kwasababu ya nini tutajua kama wanafanya kazi na wanastahili kuwepo au wanakula kodi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyininge ambayo naomba sana, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara aweze kuangalia ni *BRELA*. Waziri wa Viwanda na Biashara, katika kitu ambacho kitamfanya aonekane kwamba amefanya kazi kwenye Wizara hii au hajafanya kazi ni *BRELA*, naomba sana afungue macho aende akaangalie *BRELA* nje na ndani. Najua kama yupo atakuwa ananisikia au hata kama hayupo najua akipata hii habari atajua kwamba imekaakaaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni kwenye Sekta nzima ya Maji. Pesa zote zinazokwenda kwenye Sekta ya Maji zaidi ya nusu hazifanyi kinachotakiwa.

Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kufumua ma-engineer wa maji kwenye Wizara ya Maji kwa sababu ambacho kilikuwa kinafanyika ni kitu ambacho kwa kweli kinasikitisha sana. Haliwezekani wewe ukawa huko Wizarani, halafu una mtandao wa wizi kuanzia kule juu Wizarani mpaka kule chini kabisa. Wananchi wanalamika kuhusu upungufu wa maji, mabomba yamepasuka na kadhalika halafu wewe umekaa umepumzika tu.

Naomba sana Mawaziri hawa, Waziri wa Maji, Waziri wa Viwanda, Waziri wa Fedha, Waziri wa Kilimo waendelee kufanya kazi ya kuangalia watu ambao wanawazunguka Wizarani, kwa sababu inawezekana tunaweza tukakaa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Mambo ni mengi, muda mchache. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa John Marko Sallu atafuatiwa na Mheshimiwa Toufiq Salim Turky na Mheshimiwa Minza Simon Mjika ajiandae.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nianze na shukrani. Naishukuru sana Serikali yetu sikivu. Namshukuru sana mama kwa kuja na bajeti hii bajeti sikivu. Hapa nipende kumpongeza ndugu yangu Waziri, Mheshimiwa Mwigulu, Naibu wake na watendaji wote walioko chini yake kwa kuandaa bajeti hii Sikivu, iliyosikiliza mawazo mengi ya Wabunge. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli namshukuru sana mama kwa jinsi ambavyo ametukumbuka kwenye barabara. Sisi wa vijijini kwa kutuongezea zile hela za *TARURA* zimetusaidia sana na zitasaidia sana kusisimua maendeleo ya kilimo kule. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najikita zaidi kwenye kilimo kwa sababu Jimbo langu linashughulika zaidi na kilimo, kwa hiyo, katika ile asilimia 65 ya watu wanaoshughulika na kilimo na jimbo langu tumo. Kwa kweli asilimia moja ya bajeti ni ndogo sana kwa kilimo, kwa sababu kilimo kwa sababu kilimo kimebeba asilimia 65 ya wananchi. Ili tuweze kupata maendeleo kwenye nchi yetu, tunahitaji asilimia 65 ya wananchi kusisimua ili iweze kulima kwa tija. Ili iweze kulima kwa tija tunahitaji Maafisa Ugani wa kutosha pamoja na mbinu za kuwaelimisha ili waweze kulima kwa tija kwani mazao yanayopatikana sasa hivi ndani ya heka moja yako chini sana hayana tija. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika kusisimua wakulima hawa soko ni muhimu sana la ndani na nje. Soko la ndani linaweza kusisimuliwa zaidi kwa kuwa na mbinu za kutengeneza viwanda vidogo vidogo ambavyo vitaleta tija ya ku-*add value*, kuongeza thamani mazao yetu. Kwa hiyo,

taasisi husika zinatakiwa hapa Serikali iziangalie kama alivyosema mwongeaji aliyejita, kuna hizi *CAMARTEC* watakiwa waje na mbinu ya kuhakikisha kwamba tunapata viwanda vidogo vidogo ambavyo vitasaidia kusimua uchumi kule vijijini. Uzuri ni kwamba ndugu zetu wa *REA* wamejitahidi umeme unaenda kila mahali, kwa hiyo sasa ni jukumu la viwanda hivi kusimuliwa ili viweze kuleta tija kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, soko la nje ndugu zetu wa *TANTRADE* wanajitahidi, naomba na sisi wafanyabiashara tujitahidi kutafuta soko la nje kwa kadri iwezekanavyo kwa sababu ukiangalia wenzenetu jirani wanaauza sana nje mazao yetu sisi. Mazao yetu mengi yanapitia Kenya. Kwa hiyo hapa kuna jambo la kujifunza. Kwa mfano, kilimo cha mbogamboga na matunda ambapo kwenye jimbo langu tuna eneo kubwa sana wanalima machungwa na maembe pamoja na mbogamboga, kata takribani 14. Hapa nashauri lijengwe soko la matunda pale Segera ili liweze kurahisisha matunda haya kukusanya na kuweka soko la Kimataifa pale ambapo litakuwa na majokofu ya baridi kwa ajili ya matunda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa napo pana kitu cha kujifunza kwa sababu baada ya kukusanya na kununua mazao haya ya matunda na mbogamboga tunatakiwa tuyapeleke nje, lakini bandari zetu bado hazijawa imara kusafirisha mazao haya. Maana ukiangalia kwa sasa hivi mazao mengi ya mbogamboga na matunda yanapitia Bandari ya Mombasa, hata yale maparachichi ya Njombe mengi yanapitia Mombasa badala ya kupitia Bandari ya Dar es Salaam au ya Tanga. Sasa hapa tuna kitu cha kujifunza. Serikali ikae na wafanyabiashara ili iweze kuona tuna upungufu gani ambaao bandari zetu ya Tanga na Dar es Salaam haiwezi kusafirisha mbogamboga na matunda kwa urahisi kiasi ambacho kinawafanya wakapitie kwenye bandari nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuongelea suala la umwagiliaji, kwa sababu umwagiliaji utaongeza sana

tija kwa wakulima wetu. Sisi wa Handeni Vijijini tunapitiwa na Mto mkubwa wa Pangani ambapo tungeweza kutumia vizuri Bonde ya Masatu na Bonde la Kwamgwe ambapo maji yameshafanya kazi ya kuzalisha umeme sasa yanaenda kutupwa tu baharini. Kwa kutumia mabonde haya tungeweza kusisimua sana kilimo kwa wananchi na kuleta tija na hatimaye kuongeza kipato cha wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mito ya msimu ambayo wakati wa mvua inaleta tafrani kubwa kwenye madaraja yetu. Sasa hii mito ya msimu tungeweza kuyakinga maji na tukayatumia kwa ajili ya umwagiliaji wa mbogamboga na matunda, tungeongeza tija kubwa kwa wananchi wetu. Mito hiyo ni kama vile Mto Msangazi na Mto Mnyuzi ambayo inakatiza katika eneo kubwa la Jimbo la Handeni Vijijini ambapo tukiitumia vizuri, basi tutatengeneza mazingira bora ya wakulima na hivyo kuongeza tija na kipato kwa ujumla na hatimaye kuongeza pato la halmashauri na nchi kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye suala la zile mashine za kukusanya kodi. Mashine zile zinahitaji mtandao wa simu (*network*) na eneo kubwa la Jimbo la Handeni Vijijini hatuna *network* ya kutosha. Hivyo tunatumia mashine ambazo zinaweza kukusanya kodi *offline* lakini inabidi lazima mkusanyaji huyo wa kodi atoke aende kutafuta mtandao ili aweze ku-*reconcile data* zake. Sasa hicho kipindi cha kwenda kutafuta mtandao na kupanda kwenye mti kupata mtandao ina maana kuna malori ya mizigo yanapita pale, kwa hiyo kuna mapato tunakosa. Hivyo, Wizara husika naomba itusaidie, mtandao upatikane katika maeneo yote ili tuweze kukusanya mapato ya halmashauri kadri inavyotakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kushukuru upatikanaji wa mbinu mbadala ya kupata hela ya kuchangia *TARURA* kwa sababu tukiimarisha *TARURA* tutaweza kutoa mazao yetu kwenda sokoni na bei itakuwa nzuri kwani sasa hivi kuna mazao yanaharibika na kuozea mashambani kwa kukosa barabara nzuri. Hivyo, nasihii ule ukusanyaji wa vyanzo

ambavyo tumevipanga hapa ufanyike vizuri na Fungu lilindwe vizuri ili kweli lipelekwe kutengeneza barabara zetu za *TARURA* zipitike mwaka mzima ili tuweze kutoa mazao na tupate maendeleo tarajiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Toufiq Salim Turky atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mheshimiwa Salim Mussa Omar ajiandae.

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutujaalia uzima tukafika katika Bunge hili. *Halikadhalika naomba tumwombee dua Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Ghati amepata ajali na yuko mahututi, lakini tumwombe Mungu amjaalie shufaa aweze kurudi katika Bunge hili tuwe nae pamoja.* [**Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge**]

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Turky, ngoja tuelewane vizuri. Taarifa kuhusu wagonjwa na vifo hutolewa na Kiti. Kabla Kiti hakijatoa maelezo usije ukasema hapa mgonjwa yuko mahututi kumbe sio mgonjwa. Kwa hiyo tafadhalii, hayo maneno yaondoke, madam Kiti hakijatoa bado Taarifa.

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafuta hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii tumuombee mzee wetu Hayati Kenneth Kaunda alikuwa katika waasisi wa Bara letu hili la Afrika. Alikuwa pamoja na mzee wetu Mwalimu Nyerere katika kuwakomboa Waafrika wenzetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuja na bajeti ya namna yake. Kwa kweli bajeti hii imewagusa karibu

Watanzania wote, tukisema wote pamoja na wa visiwani. Kwa kweli, mwenyewe nimeshaenda kwenye vikao tofauti katika Baraza la Biashara Zanzibar, Baraza la Biashara la Taifa la Bora na katika kilio kikubwa sana kilikuwa ni kilio cha VAT. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na Wizara ya Fedha kwa kuona kilio cha Watanzania. Watanzania sisi ni ndugu tuna ushemeji kila mkoa kutohana na kwamba, kuna Wasukuma wako Zanzibar, wako Wagogo Zanzibar, wanakuja kule kutembelea kwetu, wanaona *TV*, wanaona *blender*, wakichukua wanalipishwa VAT, wakija zao bara wanalipishwa VAT Bora, lakini hiki kilio cha Watanzania kimeonekana. Hongereni mno. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika tunafahamu Watanzania wengi waliokuwepo ni wajasirimali na wafanyabiashara wadogo wadogo. Kama hatujabuni miradi tofauti basi Watanzania tutabakia kuwa na vibaka au wakawa vaporaji. Leo kwa kupitia punguzo la bodaboda hizi faini peke yake, basi imeleta hamasa ndani ya nchi watu wameweza kufanya kazi zao ipasavyo. Ilikuwa ni juzi wakati inasomwa bajeti nilikuwa na Mheshimiwa Shabiby wakati linaongelewa suala la kupandisha mafuta bei, akasema sasa haya mafuta yameshapandishwa, nikamwambia kwani unadhani zile pesa za TARURA za 500 zingetoka wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara ya Fedha na Mipango kuja na ubunifu wa kutafuta vyanzo tofauti vya kuleta maendeleo ndani ya Tanzania yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda sana kuongelea suala zima la forodha ndani ya Afrika Mashariki. Hivi karibuni nilimwona rafiki yangu, Mheshimiwa Bashe akienda zake Namanga kwenda kupigania masuala ya mahindi. Tukajuliza, kwani hii kazi ya Waziri au ya Wizara? Kulikuwa kuna itifaki ya Forodha ya Afrika Mashariki. Katika itifaki hii ilipaswa kila

mwanachama atoe wajumbe watatu. Mjumbe mmoja ni Mwanasheria, anatakiwa Afisa wa Forodha halafu pia anatakiwa na Afisa wa Biashara. Toka 2005 itifaki hii kuititia Ibara ya 24 ya Biashara inatakiwa kuwe na Kamati ya Biashara ambayo inatatua changamoto hizi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya au nzuri wakaongezeka wanachama wawili wengine Burundi na Rwanda, ikabidi ifanyike *amendment*. Miaka 15 imechukua kubadilisha *amendment*. Kwa bahati nzuri *amendment* imekamilika, kinachohitajika sasahivi ni kuitisha katika Mabunge yetu kuhakikisha hii Itifaki ya Forodha inafanya kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo naomba sana kuititia Bunge hili la Kumi na Mbili kuweka historia kuwa Itifaki ile ya Forodha tumeweza kuitisha na tukawa katika mstari wa mbele kidiplomasia kushawishi wanachama wenzetu wa Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi kuititia Mabunge yao kuhakikisha ile itifaki inapitishwa. Baada ya hapo tutakuwa na Kamati sasa inayotatua haya masuala ya *NTBs*. Haiwezekani leo kuona tuna changamoto ya bidhaa fulani mtu anatoka katika Wizara yake anakwenda kutatua, anaenda mipakani na wakati tayari tumesha jipangia inawezekana kuwa na Kamati ya Biashara kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaelekeea katika *AfCFTA* ukanda wa Afrika nzima kuwa na biashara huru wakati *East Africa* pekee mpaka sasa hivi tunatafuta Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu waende kutatua matatizo haya. Kusema ukweli ile ndoto ya kuwa na Ukanda wa Afrika ya Biashara Huru, basi itakuwa ni ndoto tu. Kwa hivyo, nawaomba sana tuipitishe itifaki hii kuhakikisha Kamati ya Biashara inafanya kazi yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia nataka niongee kidogo kwenye suala la ufugaji. Tanzania sisi ni wa pili katika kuwa na wanyama (*cattle*) wengi. Hata hivyo, ukitazama *value* katika wanyama hao, yetu iko chini mno.

Nimetazama kuna Mabara ya Japan wana *steak* inaitwa *Wagyu*, kuna wenzetu kuitia Scotland wanaitwa *Angus*. Ile nyama kilo moja inaweza kufika mpaka dola 200 sawasawa na ng'ombe mzima tunayeua sisi. Sasa hebu tuwasaidie wakulima wetu kuhakikisha tunakuwa na *prime steak* pia. Leo katika hoteli zote za nyota tano nyama zinatoka Afrika Kusini, Argentina, New Zealand na sisi bado nyama zetu haziko katika *quality* za kuwepo katika *five Star properties*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani hata siku moja tuwe wa pili katika Bara la Afrika na nyama zitoke nchi nyingine kwa sababu kiwango chake bado hakijafikiwa. Naiomba sana na naishauri Wizara husika kuhakikisha tunaelimisha wafugaji wetu kuweza kuwalea ng'ombe, mbuzi na wanyama wetu kuhakikisha wanakuwa wa kiwango, sio tu kwa kutumika kwenye hoteli zetu lakini kuitia ukanda mzima wa Afrika na dunia kiujuimla. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Mussa Omar na Mheshimiwa Mwita Kembaki Michael ajiandae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mungu sana kwa kutupa uhai ili leo tuweze kuzungumza machache kuhusu Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwape pole sana vijana wa timu ya Mwadui kwa namna walivyoonewa jana na lile goli la *offside*, kwa kweli lile goli halikuwa goli, Yanga walibebwa sana, lakini *Insha Allah* tutawalipia tarehe 3 Mungu akipenda. Vijana wasilie, wanyamaze tutawalipia tarehe 3. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa uteuzi wa Mheshimiwa

Mwigulu Lameck Nchemba pamoja na *Engineer Masauni* Masauni kukaa kwenye Hazina Kuu ya Nchi kwenye Wizara ya Fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kitendo cha kuaminiwa tu na Mheshimiwa Rais, nasi hatuna mashaka na uelewa na uchapakazi wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na Mheshimiwa Eng. Masauni, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha pamoja na watendaji wengine wote. Mimi ni mionganini mwa Wabunge wanaotoka kwenye familia masikini. Kitendo alichokifanya Mheshimiwa Rais cha kutupa Shule ya Sekondari kila jimbo, cha kutupa shilingi milioni 500 kila Jimbo, kimetugusa masikini wengi wa nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amegusa nyoyo za watu masikini wa nchi hii kwa sababu maeneo anayoyagusa ni yale yatakayoinua sana uwezo wa watu masikini wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Shule moja ya Sekondari itazalisha watoto wengi sana kwenda kwenye ufaulu wa kati na kwenda kwenye kujitegemea na kupata ajira. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais amepanda mbegu njema kwenye miyo yetu, tunamshukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine watasema tuna Shule za Sekondari kila Kata; kweli, chukulia mfano katika Kata yangu ya *Mvumi Mission*, watoto waliopo Darasa la Saba mwaka huu ambao ndio wanategemewa kwenda Kidato cha Kwanza mwakani wapo 450. Utawapeleka shule gani hata kama una shule? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kitendo cha Rais kutupa tu shule moja hii, popote tutakapoiweka itasaidia sana wakazi wa Jimbo la Mvumi kuweza kupata elimu bora na kuendelea, lakini watu hawajaelewa sawa sawa, hii shilingi milioni 500 ilizungumzwa vizuri sana na Mheshimiwa Mama Kilango pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine. Mwaka 2020 tulipata mvua nyingi sana. Mmvua zile ziliharibu sana barabara za vijijini. Sasa Mheshimiwa Rais kuliona hili na kutupatia hii fedha, sisi hatusemi kidogo. Asiyeshukuru kwa

kidogo hata kwa kikubwa hawesi kushukuru. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa tendo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tu wenzetu wa TARURA, zikatengenezwe barabara za kiwango cha Mheshimiwa Mama Samia. Tumemwona, mama hacheiki katika mambo mabaya. Likitokea jambo ambalo halimfurahishi, hapo hapo anakula kichwa cha mtu. Kwa hiyo, tusije tukaanza kushuhudia maumivu. Tusifikiri ametoa tu kama zawadi, atataka baadaye aone kazi iliyofanywa kutokana na fedha hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tuishauri Serikali kuendelea kutanua wigo wa walipa kodi. Hili jambo ni jema sana. Unajua tunawezaje kuwapata walipa kodi wapya? Kama tutaboresha kilimo chetu kwa nchi nzima, tutatengeneza wakulima wa chini kupanda kuwa wakulima wa kati na hivyo kilimo chao kuwa kilimo cha biashara. Hapo tutapata walipa kodi wapya tusiendelee na wale wale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine jipya, tumekuwa tukishauri sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. Dodoma tukitengeneza bandari kavu hapa tutapunguza mafoleni yote kuelekea Dar es Salaam, mizigo mingi inayokwenda kanda ya ziwa inayokwenda nchi za Kongo, Burundi na Rwanda itatokea Dodoma badala ya kutokea Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunashauri tu kwamba mkitengeneza bandari kavu hapa Dodoma, mtarahisisha sana uchumi wa hapa Dodoma pamoja na Kanda nzima ya Ziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kupunguza kodi ya pikipiki, lakini kuja jambo wamelisahau pale. Siyo pikipiki pekee inayobeba abiria mmoja, hata *taxi/inabebe* abiria mmoja, lakini bado faini yake ni shilingi 30,000. Vile vile *taxi* zimebanwa sana, ujio wa bodaboda pamoja na bajaji umeua kabisa madereva *taxi* wengi, hali zao ni mbaya. Sasa tukiwaacha na faini kuwa ile ile shilingi 30,000, kwani *taxi/inabebe* watu wangapi jamani? *Taxi* siyo daladala, inabeba mtu mmoja anayekodi, akipigwa

faini ni ile ile shilingi 30,000. Kwa hiyo, Waziri alitazame hilo nalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina maeneo mengi ambayo yanategemewa kuzalisha. Tumesikia hapa watu wanazungumza habari ya biashara katika Soko Kuu la Kariakoo, kwamba imepooza. Ni kazi ya Serikali kwenda *harmonize* biashara pale, kwa sababu pale tulikuwa tunapokea wageni wengi. Nchi nyingi wamekuwa wakija Kariakoo pale wanalala kwenye hoteli zetu, wananaunua bidhaa hapa kwetu. Sasa tuiangalie ile kodi ya wafanyabiashara, ikiweza kupunguzwa kufikia kiwango ambacho wafanyabiashara wengi watalipa, itasababisha Serikali ikusanye mapato ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mashaka na Mchumi daraja la kwanza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na *Engineer*, hebu nendeni mkae mwangalie namna ya kulifanya lile soko lirudie ubora wake kama ambavyo liikuwa Dubai ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nimeona na nimpongeze sana kwa habari ya kuweka kodi kwenye michezo ya kubahatisha, hizi *betting*. Ushauri wangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, kwanza niwapongeze sana *Sports Pesa* wamekuwa wakidhamini timu ya Simba, Yanga na Namungo. Taasisi nyingine nazo zichukue, tuweke walau hata sheria ya lazima, hawa wanaoendesha michezo hii nao wadhamini *club* nyingine ili hizi *clubs* ziweze kupata wadhamini, ziweze kucheza michezo ya kibiashara na baadaye kukuza mpira wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaona soko kubwa, tuna wachezaji wa nje hapa wanalipwa fedha nyingi sana na wachezaji wetu wa ndani viwango vyao vimeongezeka. Unaweza kuona katika ukanda huu wa *East Africa* sasa hivi hakuna *forward* kama John Raphael Boko. Sasa tukizalisha akina Boko wa kutosha, maana yake ni nini? Maana yake Tanzania nayo itauza wachezaji nje, tutanufaika na uchumi wa michezo.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Halafu mimi nikichangia huwa kengele inawahi. (*Kicheko*)

Mhehsimiwa Naibu Spika, kazi tuliyonayo nimesema kwanza ni kuhakikisha kwamba tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika kazi njema anayoifanya katika nchi hii, lakini tuelewe kwamba Rais anaandika historia yake na kuna vitu vya tofauti huko mbele ya safari vitatokea ambavyo havikuwahi kutokea katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna wengine hawalitazami, sisi tumekuwa tuna uchaguzi tofauti kati ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwenye chama chetu, uchaguzi unatangulia wa Zanzibar, halafu baadaye tunakuja Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mungu akimpa uhai, akaendelea mpaka miaka 10 ijayo Mheshimiwa Samia, atakutanisha Uchaguzi wa Zanzibar na Uchaguzi wa Jamhuri, vyote vitakutana pamoja chini ya uongozi wa Samia. Sasa tumuache huyu mama aandike historia hiyo, yaani atakuwa Mwenyekiti wa Chama 2030 anayetafuta Rais wa Zanzibar na wakati huo huo anatafuta Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo jipya kabisa halijawahi kutokea, lakini litatokea 2030. Kwa hiyo, hapa katikati mimi sioni kama kuna mtu ye yeyote katika nchi hii ambaye atasema anaweza kushindana na mama. Katika jambo gani? Maana mama anapiga hii mitano, anapiga mitano ya mwisho, halafu anaunganisha pande zote mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Omari Salim, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Kembaki Michael ma Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka ajiandae.

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia machache katika Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu wa *Azza wa Jalla*, kwa kutukutanisha leo hapa tukiwa wazima na tukiwa na akili timamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nakishukuru chama changu cha Mapinduzi kwa kuniamini na kunteua na leo ni Mbunge wa Jimbo la Gando ndani ya Bunge hili Tukufu. Kipekee nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitawashukuru wananchi wa Jimbo la Gando walionichagua kwa kishindo kunileta katika mjengo huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua tu fursa hii kuwaambia kwamba sitawaangusha na kama ilivyo sasa hivi mambo yanarindima, *Suluhi Cup* inaendelea Jimbo la Gando, karibuni sana. Mimi nina mambo matatu ambayo nataka nichangie katika hotuba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kama walivyotangulia Wabunge wengi ndani ya Bunge hili kumshauri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Wizara yake kuhusiana na *Bureau De Change*; mimi ni Mbunge kutokea Pemba. Wafanyabiashara wengi waliopo Dar es Salaam ni wapiga kura wetu au ni ahali, au ni ndugu wa wapiga kura wetu. Sasa nisipolizungumza suala hili, kidogo nitakuwa sijawatendea haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kutokea Pemba tumejikita sana kwenye biashara. Unapofunga moja kati ya *component* za biashara, unatuua kiuchumi. Unapoweka kizingiti katika biashara kama ya *Bureau De Change* unaua kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hainiingii akilini mwangu hata kidogo kuwekwa kwa shilingi milioni 300 mtaji wa kufungua *Bureau De Change*. Binafsi kama Salim, naiomba Serikali kupitia Wizara ya Fedha iliangalie tena jambo hili... (*Makof*)

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Omar Salim kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

## TAARIFA

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kumpa taarifa mzungumzaji. *Capital requirement* ya kuanzisha *bureau* kwa mujibu wa *regulation* ya 2019 ni shilingi bilioni moja na siyo milioni 300 kama alivyosema. Hiyo ilifutwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Omar Salim, unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, hicho ni kichakaa. Kule kwetu tunaita kichakaa, yaani balaa. Hilo ni balaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi, mpaka namaliza Chuo Kikuu pale *UCC* kuchukua Diploma yangu ya Teknolojia, Habari na Mawasiliano sikuwahi kufikiria kuajiriwa na Serikali; na huu Ubunge haikuwa ndogo yangu kabla, umekuja tu kwa sababu nilihisi ninao uwezo wa kuwasemea wananchi wa Gando Bungeni baada ya kumaliza chuo. Nilikuwa nategemea sana kujajiri, lakini sasa kama kutakuwa kuna vingiziti kama hivyo, sidhani kama wale ambao hawajabahatika kuwa Wabunge kama Salim watakuwa na uwezo wa kujajiri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lipo *serious* ndani ya Dar es Salaam. Mimi binafsi nilikuwa na rafiki zangu ambao

waliokuwa na *Bureau De Change* wanafika hata 125 kwa ambao ninawafahamu, leo hii wamekaa *dormant*. Sio hao tu, hata wale ambao walikuwa ni wafanyakazi wao, wamerudi Pemba wengine na ndio hao wanaoshika mabango kuitukana Serikali pale wanapoambiwa waandamane na wale watu ambao hawaitakii mema Serikali hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoke huko nielekee katika dirisha la kupeleka *claims* kwenye masuala ya *business dispute*. Narudia tena kama nilivyoungumza siku ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Wako vijana ambao wamepewa nafasi kubwa, nami leo ni-*declare interest*, nilikuwa ni mfanyabiashara na ni mmiliki wa Kampuni kubwa ndani ya Taifa hili katika wamiliki wa kampuni hiyo (*shareholder*). Unafanya kazi na Serikali lakini mwisho wa siku anatokea mtu, kwa sababu tu ya cheo chake na nafasi yake, anatengeneza mazingira ya kuwakwamisha bila kujali kama akikuangusha wewe...; na inawezekana tu ana *personal conflicts* na mmoja wa *director* katika Kampuni, anatengeneza namna ya kuizua kampuni hiyo kutokuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni hii inawezekana ina wafanyakazi zaidi ya 300; ni familia 300 hizo ambazo ni nyingi katika Taifa letu hili; lakini anatengeneza mazingira, anaikwamisha, inashindwa kufanya *progress* zake za utendaji na mwisho wa siku kampuni ile ina-*collapse* na inaanguka. Sijui sasa anamlaani nani? Mwisho wa siku ukiwa unamiliki kampuni kama hii na mtu anakutengenezea mazingira kama hayo kwa sababu ya nafasi yake kubwa, unashindwa kuamua: Je, umshitaki au uende wapi? Maana yake unaenda kumshaki sehemu ambayo wewe ndipo unapatia riziki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mimi nafanya kazi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Kampuni yangu. Akinitengenezea mtu mazingira, nashindwa kulishtaki Bunge kwa sababu nafikiria kesho itakuweje? Inawezekana lile tatizo likatatuliwa lakini kwa sababu

nililipeleka Mahakamani Bunge lako, litashindwa kuweza kuniamini kwamba labda nitakuwa sina imani nalo. Kwa hiyo, unakuta makampuni yanafanya kazi na baadhi ya taasisi za Serikali, lakini mkandarasi yule anashindwa kwenda Mahakamani kuishtaki taasisi ya Serikali na mwisho wa siku anajikuta anarudi mtaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atutengenezee dawati la *Claim* la chini kwa chini...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salim, unaweza kusimama kawaida, bado utasikika. Maana mpaka ukimaliza kuchangia unaweza ukawa unaumwa mgongo. Kwa hiyo, utaweza kuchangia ukiwa umesimama na bado utasikika. (*Kicheko*)

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, usijali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri Mheshimiwa Waziri atutengenezee dirisha la kutusikiliza chini kwa chini kwanza. Kuna baadhi ya Kampuni zinaonewa na hili liko wazi. Ukweli tuuseme. Hata mimi ndani ya Chama changu cha Mapinduzi niliapa kwamba nitasema ukweli daima, fitina kwangu mwiko. Sasa kama niliapa hivyo na nimeapa ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni lazima ukweli tuuseme. *A spade, call it a spade, not a big spoon.* Pauro libaki kuitwa pauro, tusilliite kijiko kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kutakuwa na *window* ya kupeleka *claims* zetu ndani ya Wizara ya Fedha, basi itatusaidia wafanyabiashara wengi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoke hapo, niseme tu, maana yake imefikia mahali mfanyabiashara anatega teuzi zinazokuja za Rais atachaguliwa Waziri gani? Je, namjua? Sasa ole wako achaguliwe mtu ambaye alikupigia simu hujapokea. Unaanza kufikiria, eeh, nirudishe tena ile *missed call* yake ya jana. Yaani tunaenda katika mazingira ya kumtegemea mtu kwa sababu ya nafasi yake sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui nafahamika! Yaani akiteuliwa mtu, unafikiria huyu nitamfikiae? Hakuna ule mfumo uliowekwa kwamba hapa mimi nitafanya biashara zangu na nitakuwa salama na sitoathiriwa na awamu itakayokuja. Hili lipo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na *crew* yako tafadhalini sana tuokoeni kwenye hili, mambo ni mengi na wafanyabiashara tunaumia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema pia nichangie katika suala la *special number/plate number*. Ni kweli, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na *crew* yako kwa kupunguza kiwango kile cha shilingi milioni 10 mpaka kikaja kuwa milioni tano. Bado tunaomba hebu tupunguzieni kidogo hadi ifikie shilingi milioni tatu. Vijana wengi wataweka majina yao ndani ya *plate number*, itatusaidia kuweza kufanya *accumulation* ya hizo fedha nydingi sana watakazolipa na pia itasaidia katika vyombo vya usalama kuweza kugundua kwa haraka zaidi pale ambapo tunamtafuta mtu ambaye ana gari ambalo limeandikwa jina. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nielekee katika kuchangia kidogo kwenye masuala ya utalii. *Next year, inshallah* tutakapofika hapa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na *crew* yako pamoja na Waziri wa Utalii hebu tutengenezeeni kifungu cha kutafuta fedha kwa namna ya kuwekeza katika *digital tourism*. Tuwe na fedha ambazo zitatuwezesha kumpata mkandarasi duniani atuwekee *digital tourism* ambayo itaweza ku-*display* hata katika *slogans* za kule kwenye *airport*. Mfano Dubai pale, tuweze kuona swala wetu wa Tanzania, Mlima Kilimanjaro, popo wetu wa Pemba ambao hawawezi kupatikana sehemu yeoyote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo vivutio vya Utalii ambavyo haviwezi kuonekana sehemu nydingine yoyote isipokuwa Zanzibar au Tanzania Bara. Tunao Kima Punju, tuweze kuwa na *display* kule katika *airport*; watu wanaposubiri ku-*connect* ndege kutoka sehemu moja kwenda nydingine waweze kuona Zanzibar kuna nini? Tanzania

Bara kuna nini? Tuweze kuongeza wigo mpana wa kupata watalii na kupata fedha za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache niliyochangia, naomba niunge mkono hoja, niwaombee kila la heri Mheshimiwa Rais pamoja na watendaji wote, *Ishallah* tutafika. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mwita Kembaki Michael atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, ajiandae.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika bajeti yetu hii ya mwaka 2021/2022. Nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea bajeti ambayo kwa kweli imekoza kila mtu. Imegusa wafanyabiashara, wamachinga, wakulima, wafanyakazi, wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya yote, Mheshimiwa Rais wetu Mama yetu ameweza kufanya jambo lingine la kipekee kwa kutoa shilingi milioni 500 kwa kila Jimbo. Tayari fedha ile imeingia, nimefanya mazungumzo na Meneja wa TARURA kuongeza Kilometra moja ya lami katika Mji wetu wa Tarime Mjini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitakuwa sina fadhila kama sitampongeza na kumshukuru kwa shillingi milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa Sekondari katika Jimbo letu la Tarime Mjini ambapo tulikuwa hatuna Sekondari katika Kata ya Saba Saba, sasa inakwenda kujenga. Nampongeza na ninatoa shukrani sana kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na watalaaam wote katika Wizara ya Fedha

kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, kuhakikisha kwamba wanatuletea bajeti ambayo imeshiba. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Nchemba pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer Masauni. (Makofî)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa mchango wangu kwa upande wa tozo au ushuru kwa bidhaa zinazotoka nje. Ukienda katika nchi jirani ya Kenya unapokuwa unatoa bidhaa hapa unapeleka Kenya, kwa mfano kama sasa hivi *juice* hizi za Azam zinavuka sana kwenda Kenya, wewe unavusha tu hamna usumbufu wowote unaopatikana katika upande ule. Wafanyabisahara wanaovusha bidhaa zile wanapita *custom* kawaida, wanapita wanalipa ushuru na bidhaa zao wanafanya biashara kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitolea mfano mwingine ng'ombe wanatoka Tanzania kwa wingi sana wanapita tena pale mpakani bila shida yoyote wanavuka na wanaenda wanaauza bila shida yoyote. Sababu kubwa inayosababisha biashara hii iweze kufanyika vizuri ni kwa sababu ushuru wa Kenya uko chini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchukue mfano katika Mji wetu wa Tarime nyumba zinajengwa kila siku, wakati wanajenga wanatumia simenti, mabati, misumari, na kadhalika lakini sasa tuchukulie mfano wa simenti inayozalishwa Tanzania inauzwa shilingi 22,000 mpaka shilingi 24,000 ilhali simenti ambayo inatoka Kenya inauzwa shilingi 16,000 mkapa shilingi 17,000, sasa kwa mkulima au mtu wa kawaida pale Tarime kununua simenti shilingi 22,000 na huku anajua kwamba, kuna simenti hapa inauzwa shilingi 17,000 inakuwa ni ngumu kidogo. Nini kinafanyika sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika sasa vijana wanaamka wanaanza kufanya wanapita njia *panya road* kuitisha ile simenti na matokeo yake Serikali inapoteza mapato makubwa sana. Mimi ningeshauri Serikali waangalie, wajifunze kutoka katika nchi ya Kenya walifanyaje ili

wafanyabisahara waweze kulipa kodi kwa hiyari badala ya kufukuzana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kuna vifo vinatokea mara kwa mara pale na hivi vinatokana na vijana ambao wanasonba hizi bidhaa au magendo kutoka nchi ya Kenya kuanguka au kugongwa pale ambapo wanafukuzana, hii inatokana na kwamba, anapopita aliye ushuru kawaida ushuru ule unakuwa ni mkubwa zaidi kiasi kwamba, hawesi kupata faida, lakini iwapo kama ushuru huu ungekuwa wa kawaida kama nchi jirani...

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kembaki kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Abdullah Mwinyi.

## TAARIFA

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ningependa tu kumpa taarifa mchangia mada taarifa ya kwamba, simenti ya Kenya kwa mujibu wa Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ikija Tanzania haitozwi kodi na simenti ya Tanzania ikienda Kenya haitozwi kodi, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Kembaki unapokea taarifa hiyo?

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mimi naona inatozwa na ndiyo maana wanafukuzana. Kwa hiyo, nikipokea na ilhali kuna kufukuzana na inakamatwa na hivi juzi punde tu *TRA* imegawa zaidi ya simenti 150 kwa shule za sekondari na msingi ambazo zimekamatwa kutokana na hii biashara ambayo wafanyabiashara ambao wanafanya magendo katika barabara hii ya Sirari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, sipokei hiyo taarifa.  
(*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Sasa ili taarifa zetu rasmi za Bunge zikae vizuri, hao wamepokonywa kwa sababu ya kodi au wamepokonywa kwa sababu ya magendo?

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wanunua simenti Kenya wanaileta Tarime. Kwa hivyo, wakati wanaileta wanakamatwa.

**NAIBU SPIKA:** Wanaileta kwa njia ya magendo ama wanaileta kwa njia halali?

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanaileta kwa njia ya magendo, kwa jina maarufu njia za panya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, kwa njia hii kumbe kuna haja ya Serikali kutoa elimu kwa wafanyabiashara elimu ambayo itasaidia wafanyabiashara kujua hizi namna ya kupitisha au namna ya kuagiza bidhaa kutoka nchi nyingine ili kuepuka ukwepaji kodi au hii bidhaa kupita kwa njia ya magendo. Ukweli ni kwamba, Serikali ikifanya hivi kwa kutoa elimu ya kutosha pia kuhakikisha kwamba, hizi tozo au ushuru unakuwa wa chini kwanza itahamasisha watu kulipa kodi wenyewe kwa hiyari, lakini pia itasababisha Serikali kupata mapato yake bila usumbufu wowote ikilinganishwa kwamba, mipaka ya nchi yetu na wafanyakazi walioko *TRA* hawatoshi kudhibiti haya mazingira ya ukwepaji au utoroshaji wa bidhaa ambazo zinaingia nchini. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia, Serikali ifanye utafiti wa kina ni kwa nini viwanda vyetu au bidhaa zinazosalishwa nchini zinauzwa kwa bei ya juu ikilinganishwa na bidhaa zinazotoka nje. Bila kufanya hivi bado ukwepaji kodi utaendelea, vilevile hatutapata suluhu ya nchi yetu kuwa tegemezi. Ningependa sana utafiti huu ufaniyiwe kazi na baada ya utafiti huu kupatikana tutafute majibu namna gani

tunaweza kutatua changamoto hizi ambazo zinasababisha bidhaa zinazozalishwa nchini kuuzwa kwa bei ya juu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsanteni sana, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa. Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo ajiandae.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama na kuchangia bajeti ya Serikali leo hii. Pili nimpungeze Mheshimiwa Rais Mpendwa, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambazo anaendelea kuzifanya. Pia, niipongeze Wizara ya Fedha ikiongozwa na Waziri wake Mheshimiwa Mwigulu Nchemba pamoja na timu yake kwa bajeti nzuri ya Serikali na bila kusahau Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Daniel Sillo kwa bajeti yao nzuri ambayo imeendelea kutekelezeka na hatimaye kufikia muafaka hapo itakapopitishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ni bajeti ambayo itaondoa changamoto nyingi za wananchi wetu wakiwemo wananchi wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara wakubwa na wadogo, wachimba madini na makundi mengineyo. Pamoja na haya ninaomba nieleze kwamba, wakati wa kutekeleza miradi ya maendeleo Serikali hii haiwezi kutekeleza miradi yake bila wananchi hawa kulipa kodi ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia katika maeneo matatu. Eneo la kwanza ni eneo la miradi ya maendeleo viporo, eneo la pili miradi ya kimkakati na eneo la tatu ni eneo la ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye eneo hili la miradi ya kimkakati. Miradi hii lengo la Serikali kuleta miradi ni zuri sana ambalo litaiwezesha kila Halmashauri kutekeleza miradi yake yenye we wakati huo wakiwa wanajielekeza

katika kukuza uchumi wa kila Halmashauri yake. Pamoja na lengo hili, dhamira ya Serikali ni nzuri, lakini utekelezaji wa miradi hii kule kwenye Halmashauri imekuwa ni kinyume na matarajio ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali wakati wa kufanya upembuzi yakinifu wa miradi hii ni vema tukawashirikisha wanancbhi wetu wa maeneo yale pamoja na wadau wa maendeleo wa kila eneo husika. Eneo hili la miradi ya kimkakati lina changamoto zake nyngi sana, changamoto hizo tumeona wakati miradi hiyo imeshakamilika na kuanza kutumika. Tukija mfano wa Mkoa wa Ruvuma, Wilaya ya Songea Mjini, Mheshimiwa pale kuna changamoto kubwa sana. Mradi mkubwa wa kituo cha mabasi umejengwa lakini mradi huu unashindwa kufanya kazi vizuri kulingana na ushirikishwaji wa wananchi wa maeneo yale pamoja na wadau wake wa maendeleo wa Mkoa wa Ruvuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini ya kwamba, kama tungewashirikisha wananchi katika utekelezaji wa mradi ule, eneo lile la mradi uliojengwa kilometra 21 kutoka Songea Mjini usingejengwa mradi ule kule, badala yake mradi huu ungejengwa kwenye eneo rafiki na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma. Kwa kweli, wakati wa utekelezaji wa miradi yetu ya maendeleo ni vema dhana ya ushirikishwaji wa jamii iwe ni nyenzo muhimu katika dhana nzima ya utawala bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye eneo la miradi viporo. Kwanza niipongeze Serikali kwa dhamira yake nzuri ya kuweza kubadilisha eneo la Kanuni ya 21, Fungu Namba 439, ambalo changamoto hizo zitaondolewa kwa kutorejeshwa fedha katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na badala yake fedha hizi zitatumika kuendeleza miradi ya maendeleo kama ilivyopangwa. Changamoto hii tumekuwa tukiipata kila mwaka kwenye kila Halmashauri, inapofika tarehe 30 ya Juni ya kila mwaka fedha hizi hurejeshwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na badala yake miradi ile

husimama au kutoendelezwa kabisa kwa changamoto ya kuwa hii imekuwa ni miradi viporo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuondoa changamoto hiyo na sasa miradi yote ya maendeleo itakuwa inatekelezwa kama ilivyopangwa. Niiombe Serikali sasa kuhakikisha ya kwamba, miradi yote ambayo imeanza kutekelezwa ikamilishwe kama ilivyopangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye eneo la ajira. Ajira ni changamoto hapa nchini. Kwa kipindi hiki chote ambacho tuko hapa Bungeni ninaamini ya kwamba zaidi ya asilimia 80 ya Wabunge wamepigiwa simu na wananchi wao wakiomba kupata msaada wa kupata ajira. Wakati huo changamoto hii tunaweza kuitatua tu kama Serikali yetu itaweka uwiano wa ajira kwa kila Mkoa kwa kuzingatia sifa au vigezo vya muombaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu nchi yetu hii ni kubwa sana, lakini wananchi wake wengi wapo maeneo ya vijijiini na pembezoni mwa nchi. Hivyo, basi niiombe Serikali hii iweze kuhakikisha kwamba, wananchi walioko vijijiini na maeneo ya pembezoni wanapatiwa ajira badala ya wananchi wale kuona usumbufu kubakia kule vijijiini na kuona ni vyema waje mjini kwa ajili ya kutafuta ajira hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba niunge mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Philipo Augustino Mulugo. Mheshimiwa Amsabi Jeremiah Mrimi ajiandae.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii adhimu. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa wetu Rais kwa kazi nzuri anazoendelea kuzifanya. Nasema anazoendelea kuzifanya maana ni kazi ambazo alikaa kama

vile Mungu alivyokaa na utatu wake mtakatifu wakaumba wanadamu na mambo yote duniani na yeye alikaa na utatu wake na Mheshimiwa wetu Hayati wakapanga mipango yote hii iliyokuwepo na miradi yote hii inayoendelea, kwa hiyo ni vitu ambavyo anaendelea navyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale ambao wanadhani na wanauliza ngoja tusubiri Mama atafanya nini? Wanapaswa kujua kwamba, hata haya yanayoendelea yeye ndiye aliyekaa pia na kuyapanga na Hayati na anaendelea kuyatekeleza. Sasa tunapaswa kum-support na kumpa nguvu ili kusudi aendelee kufanya mengi mazuri baada ya kuyamaliza haya walijyoanza nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa wetu Waziri mtani wangu Mwigulu Nchemba kwa kukalia kiti hiki cha fedha. Kwa kweli, naamini kabisa fedha yetu iko mikono salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye suala la umeme. Kipindi kilichopita tulikuwa tuna vijiji 12,312 ambavyo vilikuwa havina umeme, lakini Mama kwa mapenzi mazuri na Tanzania yetu ameona kwa mwaka huu vijiji 10,317 vyote vipate umeme. Basi kwa maana hiyo ninaamini kabisa kwa kasi hiyo, kipindi kijacho, bajeti ijayo basi hata hivi vijiji vilivyobaki 2,005 naamini kabisa vyote vitapatiwa umeme kiasi kwamba, hata Mkoa wangu wa Mara utapata umeme Mkoza mzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa wasambaza umeme. Umeme upo, umeme umetolewa, lakini sasa kasi ya usambazaji ni ndogo. Ukiingia ndani kule vijijini unawakuta watu hawajasambaziwa umeme, kwa hiyo umeme unabaki tu kuwa jina kwamba tuna umeme. Kwa hiyo, mimi niwaombe sana Ndugu zangu wasambazaji wa umeme wafuatilie sana susla la kusambaza ili kusudi wasaidie vijiji vyote na maeneo yote yapate umeme ili kuleta pato zuri kwa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la miradi ya maji. Ninamshukuru sana Mheshimiwa wangu Rais

kwa kuweka miradi na kuendelea kujenga au kutekeleza miradi mizuri ya maji ya kimkakati. Kwa kweli, Mungu ambariki sana kwa sababu miradi ya maji yote ikitekelezeka, akimtua ndoo mama kichwani atakuwa ameponya ndoa za wanawake asilimia 98 ambazo zilikuwa zinavunjika kwa ajili ya kufuata maji mbali au umbali mrefu. Wanawake wengine walikuwa wanachoka sana wanashindwa kutekeleza majukumu yao ya ndoa, lakini pia wanawake wengine walikuwa wanaenda kwenye maji mbali sana, wanapokuwa wameenda mbali wanachelewa kurudi nyumbani kwa hiyo, inawaletea *conflict* ndani ya familia zao, suala ambalo Mama yetu naamini kabisa yeye kama Mama sasa ameona kwamba, alimalize kabisa ili kusudi liende vizuri kwa hiyo, mimi niseme Mungu ambariki sana.. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Watanzania, niwaombe Watanzania wenzagu tumuunge Mama mkono, tum-*support* Mama, tuwe na umoja na ushirikiano, asitokee mtu mwingine wa nchi nyingine akaibenza Tanzania na wewe ukakubali. Mtu yeyote anayembeza Mama amelibenza Taifa la Tanzania. Mtu anayebeza Taifa la Tanzania amekubeza wewe Mtanzania.

Kwa hiyo, mimi niseme umoja wetu ndio ushindi wetu ili malengo yetu yatimie tufikie malengo yetu, tufikie uchumi wa kati na ikiwezekana tufikie uchumi wa juu zaidi, kama tunavyoona kasi ya Mama ni kubwa sana sio kama watu wengine wa huko nje walivyokuwa wanategemea na wachache waliokuwa wana nia mbaya na Tanzania walivyokuwa wanategemea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mama anaenda kwa kasi ya ajabu, Mama anapiga kazi, Mama yuko vizuri kwa sababu, wao wenyewe ni mashahidi na mashuhuda. Walidhani kwamba, miradi iliyokuwa imeanzishwa kipindi cha Hayati, kipindi kilichopita kwamba, italala, mama amesema miradi yote itatekelezwa. Na ikishatekelezwa atafanya mengine makubwa zaidi ambayo tumeshaona sasa hivi mama anaendelea kufanya mambo makubwa zaidi hata yale ambayo watu hawakutegemea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe sana Watanzania tuwe wamoja, tulilinde Taifa letu kwa nguvu zote. Niwaombe sana watu wetu wa dini zote bila kujali ni dini ya aina gani, watu wa imani zote, kila siku kukicha, asubuhi, mchana na jioni tuliombee Taifa letu la Tanzania ili tufikie malengo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii imeongelea vizuri sana kwenye suala la wachimbaji wa madini lakini la wawekezaji kwa ujumla wa Tanzania. Ombi langu, niombe sana kuna watu ambao walathirika katika mgodi wa *North Mara* kule kwetu Tarime kipindi kilichopita, kwanza kabisa maeneo yao walipoyatoa walitarajia *at least* watabadilisha kidogo maisha, lakini waliheshimu sana Serikali yao kwamba wanapotoa yale maeneo na wao watahifadhiwa vizuri, naishukuru sana Serikali yetu kwamba waliskiliza vizuri na baadhi yao walipewa fidia lakini hawajapewa fidia wote, mpaka leo kuna wengine wameingia umaskini kwa kile kinachoitwa uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii imeongelea vizuri sana kwenye suala la wachimbaji wa madini, na wawekezaji kwa ujumla Watanzania. Ombi langu niombe sana, kuna watu ambao walathirika katika mgodi wa *North Mara* kule kwetu Tarime kipindi kilichopita kwanza kabisa; maeneo yao walipoyatoa walitarajia *at least* watabadilisha kidogo Maisha. Lakini waliheshimu sana Serikali yao kwamba wanapotoa yale maeneo na wao watahifadhiwa vizuri. Naishukuru sana Serikali yetu kwamba waliskiliza vizuri na baadhi yao walipewa fidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hawajapewa fidia wote mpaka leo kuna wengine wameingia umaskini kwa kile kinachoitwa uwekezaji, unapokuwa uwekezaji Tanzania basi mawaziri wetu, waangalie hili suala la wawekezaji, waangalie watanzania wanashida gani, na uhitaji gani ili hawa Watanzania walipwe fidia zao kutokana na mali zao walizozitoa. Siyo watoe wao eneo halafu wabaki kuwa maskini kila siku wanalia siyo jambo zuri hata kwa Mwenyezi Mungu Tanzania tunahitaji baraka. Kwa hiyo, niombe sana

kwa wale waliobaki watu wa Tarime Mheshimiwa Waziri ufuatilie hili suala ili wakalipwe maeneo yao na wao waifaidi mali yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikuombe sana Mheshimiwa Waziri au Waheshimiwa Mawaziri katika wawekezaji wanaokuja Tanzania ninaimani kabisa mnajitahidi sana. Kuna jambo moja naona kama tunafeli hivi inapokuwa kuna uwekezaji mkubwa mahali basi maeneo hayo yang'ae yatakate kutokana na uwekezaji ule siyo tu watu wanawekeza kuna madini sisi tunaonekana kwenye madini. Lakini Mheshimiwa Agnes nikitoka kule Tarime vumbi limeshanipiga mpaka basi. Eti! Mpaka tusubirie bajeti ya Serikali! Kwani wale wawekezaji jamani! Si wangetutengenezea hata lami kidogo hata kuonyesha wamechukua fedha kutoka kwetu, kuchukua pesa kwetu maana yake ni kwamba wanapopata mali kutoka kwetu wanakwenda kuuza wanapata fedha nyngi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, basi wanapopata pesa nyngi na sisi wanaotuacha pale angalau basi tunukie nukie na sisi ile dhahabu siyo tu tuna barabara mbaya maji, hatuna sisi tunaitwa tu tuna wawekezaji jamani hili suala niombe sana mawaziri wetu mkae karibu na hawa wawekezaji muwaambie ukweli kwamba faida wanazofaidika nazo kutokana na nchi yetu ya Tanzania na wao pia watufaidishe.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Philipo Augustino Mulugo, atafatiwa na Mheshimiwa Msabi Jeremiah Mrimi, Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga ajiandae.

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa wasaa huu niweze kuchangia bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza kabisa pamoja na ushauri wa mambo

mengi nitakao shauri hapa niunge kabisa mkono bajeti hii ni nzuri na Mheshimiwa Waziri wa Fedha hongera sana. Lakini tumpe hongera sana mama yetu Samia Suluhu kwa sababu ndiyo Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hongereni sana kwa kuja na bajeti hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini masikitiko yangu kidogo tu kabla sijaanza kuchangia Waheshimiwa Wabunge tunaposema tunachangia bajeti ya Serikali bajeti kuu nilitegemea Mawaziri wote wawepo humu ndani. Hapa nawaona Mawaziri watano na kwa sababu nawaona Mawaziri watano, nitachangia kwenye hoja zangu kutokana na Mawaziri ninaowaona kwa sababu lazima wanisikie na wasikie ushauri wangu huwezi kuwa unachangia sehemu ambayo Waziri hayupo halafu inakuwaje. Bajeti Kuu ya Serikali siyo kwa ajili ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu peke yake Bajeti Kuu ya Serikali ni bajeti kuu yote pamoja na Mawaziri wote. Kwa hiyo nilikuwa nataka kwanza kutoa hiyo *scenario* tunaomba Mawaziri wawepo Bungeni...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo subiri kidogo nitoe ufafanuzi Waheshimiwa Wabunge nimeshasema mara kadhaa humu ndani leo nitazungumza kwa kifupi Serikali iko Bungeni.

Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi Mheshimiwa Mlugo kama huwaoni hapa ni kama vile ambavyo viti vingine vya Wabunge viro huko nje vikizungumza na hawa Waheshimiwa Mawaziri kwa hiyo lazima wawasikilize Wabunge lazima kazi zote zifanyike kwa pamoja. Na wakati huo huo hii bajeti tunayojaribu kujadili hapa Wabunge mmeshatoa mawazo mengi ambayo mengine yanatakiwa kuanza utekelezaji mara moja hayo yote lazima Serikali ikayafanyie kazi.

Mheshimiwa NaibU Spika, kwa hiyo, usiwe na wasiwasi Mheshimiwa Mulugo changia hata zile Wizara ambazo unaona Waziri hayupo hapa kwa sababu Serikali ipo ndiyo maana wewe unazungumza na mimi ujumbe kwangu wataupata usiwe na wasiwasi wowote Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILIP A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, unilindie dakika zangu, nianze na Wizara ya Madini Mheshimiwa nchi hii ingekuwa na fedha nyingi sana nchi hii kwa jinsi unavyoiona hata Mheshimiwa marehemu Mhe. Dkt. Magufuli alikuwa akisema Mungu amlaze mahali pema peponi. Lakini ni kutokana na watumishi wetu wa Serikali wanakuwa ni legelege katika kufanya mambo mengine ambayo unaona kabisa fedha zile pale unaziona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mmoja kwenye jimbo langu kule kwangu kuna sehemu kunaitwa Ngwala toka mwaka 2010 kuna kampuni inaitwa *Heritage Tanzania* imefanya utafiti wa madini, madini adimu duniani yanaitwa *rare earth* madini hayo kama yangeazwa kuchimbwa Serikali ingeweza kukusanya kodi nyingi sana zaidi ya biliioni 25 Serikali ingepewa kodi mwaka mmoja. Zaidi ya billioni 83 zinakwenda kwenye gharama za uendeshajl, zaidi ya bilioni 7 mrahaba wa Serikali na mambo mengine ajira peke yake karibuni watu 1300 kule kwangu wangepata ajira na nchi nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini toka mwaka 2010 wanazungushwa kupata leseni *special mining* nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Biteko nakuomba kwa unyenyekevu mkubwa wapatieni leseni hawa Ngwala *Peak Resource* wawefe kuchimba madini hayo ni madini ambayo hayapo Tanzania hii, hayapo Afrika hii yapo kule Songwe na Mheshimiwa Waziri unajua nilikuwa nakuomba ikiwezekana mwezi wa saba usiishe uwape leseni wale watu wanataka kukata tamaa wanataka kuondoka nchini kama walivyoondoka watu wengine ambao walikuwa pale Mbangala wameondoka mafuta yamepatikana pale ukingoni mwa Ziwa Rukwa wamefanya utafiti Serikali imekuja imesema hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mlikuwa mnafanya utafiti wa gesi mmepata mafuta mmepata na gesi lakini kabla hamjapata mafuta wamekutana na madini ya *helium*. Baada ya hapo *TPDC* wamekuja wamesema hapana tufanye pamoja wameshindwa wamekasirika wameondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, inauma sana. upande mwagine ambao ningeweza kuishauri Serikali naomba nirudi kwenye Wizara...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dotto Biteko Waziri wa Madini.

## TAARIFA

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa tu taarifa ndogo kwa Mheshimiwa Mulugo najua anachangia kwa hisia kubwa na angetamani uwekezaji ule utokee naomba kutoa taarifa kwenye Bunge lako Tukufu kwamba Kampuni ya *PLG* itapatiwa leseni ya uchimbaji mkubwa kwa mujibu wa sheria na tuko kwenye taratibu za mwisho za kuwapatia leseni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusiana na utafiti wa mafuta pamoja na gesi ya *helium* naomba kumpa taarifa vilevile kwamba kampuni ya *helium one* tayari imeshapewa leseni ya kufanya utafiti kwenye eneo hilo na taratibu zinaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mlugo unapokea taarifa hiyo?

**MHE. PHILIP A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata furaha ya ajabu sana hawa ndiyo Mawaziri wanaotakiwa katika nchi hii nimefarijika sana na huo ndiyo unapelekea kwamba kweli mimi naongea ubunge. Ubunge lazima uongee halafu Waziri *a take reaction* ndiyo maana nilikuwa nimekwambia mara ya kwanza kwamba kuna Mawaziri ukiongea wanakuwa hawapo nilishawahi kuongea mwaka juzi kuhusu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo ngoja ngoja tuelewane vizuri Waheshimiwa Wabunge nimesema hivi Serikali iko Bungeni na Waziri hapa angeweza kunyamaza wala siyo kazi yake yeze kutoa taarifa angeweza kuja kuchangia na yeze kama Mbunge mwagine na ndiyo

maana Wabunge wengine ambao pengine Waziri hajasimama kujibu kwenye hoja yako haimaanishi wewe hujachangia sawasawa ama hajakusikia.

Nadhani tuelewane vizuri hilo Mheshimiwa Mulugo wewe ulikuwa Serikalini unajua zaidi mambo haya kuliko watu wengine ambao hawajawahi kuwa Serikalini. Mheshimiwa Mulugo malizia mchango wako.

**MHE. PHILIP A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba dakika zangu zilindwe nimalizie mchango wangu kwa amani. Nije upande wa elimu, ni mwalimu na *declare interest* kwamba nilikuwa Serikalini kweli kwa kutumikia Wizara ya Elimu kama Naibu Waziri, lakini vilevile nina shule binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo lazima tulichangie lakini na dada yangu Mheshimiwa Prof. Ndalichako pale unanifahamu wewe ni rafiki yangu tunaongea mengi na ninakushauri mengi naomba ushauri huu upokee vizuri. Wakati Mheshimiwa Rwekiza akichangia jambo moja hapa ulisimama ukatoa na mwongozo lakini binafsi sijakuelewa Mheshimiwa Waziri naomba nikushauri kama mwalimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema darasa la mitihani darasa la nne, darasa la saba, *form two, form four, form six* kwa mwaka husika hakuna popote duniani ambapo madarasa hayo yanaweza yakawa hayana mkakati wa kufaulu mitihani hakuna na wote hapa Wabunge tumetoka kusoma wote tumetoka *form four* huko tumetoka *form six* tulikuwa darasa la saba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa darasa la saba mwaka sijui tisini na ngapi huko lakini Mheshimiwa Waziri nilikuwa nasomea koroboi mpaka nikafaulu mitihani ni mkakati wa kusoma usiku zinaitwa *prepohata mchana sasa watu wameanzisha June program* shule zimeanzisha *June program* na mfano mzuri ni kwa Mheshimiwa Mtaka Mkuu wa Mkoa wa Simiyu na mpaka Mheshimiwa Rais alikuwa

anamsifia namna alivyoanzisha *academic June program* wakati wa likizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Mheshimiwa Waziri unasema kwamba hapana watoto warudi nyumbani, darasa la saba mtoto yule akirudi nyumbani saa hizi na mtihani wa Taifa ni mwezi wa tisa watafeli mitihani ndiyo maana Watoto wanafeli lakini sababu ni viongozi nyie mnakataza zile *program*. Angalia shule binafsi wanavyofanya Watoto wanasoma usiku, wanasoma *March program*, wanasoma *June program*, wanasoma *September program*. Madarasa ya mitihani lazima yawekewe *program check it* walimu kwenye shule za Serikali tunakosa walimu wa *mathematics*, tunakosa walimu wa *physics* tunakosa walimu wa *chemistry* wakati shule zimefunga, tunasema darasa la sita walimu kwa sababu watoto wameenda nyumbani wale walimu wanaofundisha darasa la sita masomo ya sayansi waweze kuwasaidia kaka zao pale walimu wanajitolea wazazi wameamua kwa pamoja wamelipa fedha ya chakula wamelipa fedha ya malazi, wamelipa fedha za *stationary* wameamua wenyewe watoto wao wabaki shulenii waweze kujisomea kwa ajili ya mitihani...

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Cosato David Chumi

## TAARIFA

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mulugo kwamba mimi pale Mafinga shule ya Changarawe haijawahi kuwa na mwalimu wa *physics*. Kwa hiyo, Juni hii tunachukua walimu kutoka Mafinga *Seminary* ili waje pale watusaidia kuwa-*brush* wale Watoto naomba kumpa taarifa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo unapokea taarifa hiyo?

**MHE. PHILIP A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa miguu miwili na mikono miwili, naongea jambo ambalo mimi naishi huko niko kwenye *field* mimi ni mwalimu nafundisha *economics Form Vna VI* wakati wa mitihani lazima tuwawekee wanafunzi *program*, na wewe ulikuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pale ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri leo naomba nikatae kabisa *program* zako eti watoto darasa la saba leo warudishwe nyumbani wakienda kule watakuwa wanatumwa sokoni, watakuwa wanacheza cheza acheni wakae shulenii wasome ni jambo zuri naomba *sometime* Serikali muwe mnasikia mawazo ya wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho kipo kitu lazima tukifanye kwenye elimu kinaitwa PPP, naomba nitoe takwimu ambayo ukiyapata hayo unaweza ukaona nini naongea mwaka kesho Serikali itashindwa kuwapeleka watoto *form one* kwenye shule za Serikali kwa sababu gani. Mpango wa elimu bure ulianza miaka sita iliyopita watoto waliopo leo darasa la sita wako takribani 1,800,000 wanakwenda wapi? Serikali ina uwezo wa kuchukua kwenye darasa yao na madawati Watoto 750,000 tu kwa hiyo ni asilimia kama 100 kwa mwaka kesho lazima Serikali ijenge shule zaidi ya hizi zilizopo shule za Serikali sijui kama tutawenza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais ametoa shule moja moja kila Jimbo lakini bado tuko moja ya mia moja. Serikali naomba ije na mpango wa PPP shule za *private* zina madarasa, zina madawati zina walimu lakini zinakosa wanafunzi. Nchi ni yetu wote watoto ni wetu wote twendeni tukakae pamoja watu wa shule za binafsi tukae na Serikali tuone namna gani watoto hawa wengine waanze kwenda kwenye shule za *private* wakajaze madarasa huko halifu Serikali ianzu kuwalipa mishahara kule mbona ni kitu kile kile kama ambavyo mlifanya kwenye afya ni jambo jema mno naiomba sana Serikali isikilizage ushauri huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nasema naunga mkono hoja lakini naomba mawazo yangu yachukuliwe na Waziri wa Elimu ahsante sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Amsabi Jeremiah Mrimi atafatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga muda wetu ukiruhusu atafatiwa na Ally Anyigulile Jumbe Mlagila.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/2022. Awali ya yote nimpongeze sana mama yetu Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuijenga nchi yetu na kuwaleta maendeleo watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika moja ya hotuba zake Mwalimu Julius Nyerere mwaka 1962 alisema *to build this country we have to make many changes. And to change it we must be willing to try what is new.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Wizara ya Fedha wamekuja na mambo mengi mapya bajeti yetu kwa mwaka wa jana kutoka trillioni 34 sasa trillioni 36 hongereni sana. Lakini kuna mabadiliko mengi tumeyaona wamekuja na mapendekezo mengi mazuri na mimi naamiini kama Waingereza wanavyosema *where there is a will there is a way.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kazi yetu sisi Wabunge ni kuwachangia kuwaonyesha njia ni kuwashauri nimeona baadhi yetu wakiwa na wasiwasi naamini tunaenda kufanikisha bajeti hii na ninadhani yawezekana tukavuka hata lengo hili endapo Wizara itaenda kuwekeza vizuri katika mambo yafuatayo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja Wizara ya Fedha tunaishauri sana nimeona katika bajeti hii bajeti kwa maana ya kiasi gani cha fedha kimetengwa katika *research and*

*development* bado ni kidogo. Nimejaribu sana kuzisoma nchi za China, nchi za Taiwan, South Korea, nchi za Israel nchi hizi zinaenda kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siri pekee ambayo wameifanya leo ukiangalia China kila mahali tunanunua vitu vyao kila kitu tunanunua China vitu vingi tunanunua China na uchumi wao unapaa sana lakini China kwa miaka 10 iliyopita kila mwaka katika bajeti yao wanatumia zaidi ya dola bilioni 380 katika *research and development*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kufanya maajabu katika kuzalisha ajira nyingi kama uwekezaji wetu katika *research and development* bado ni kidogo. Taiwan, South Korea kila mwaka wanatumia Zaidi ya asilimia tatu ya *GDP* yao katika utafiti. Nchi ya Israel kila mwaka inatumia Zaidi ya asilimia nne katika *research and development* leo nchi ya Israel ni nchi ambayo inazalisha ajira nyingi pamoja na makampuni mengi ni ya pili baada ya Marekani na hii ni kwa sababu ya uwekezaji mkubwa katika *research and development*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuna vijana wengi wanamaliza vyuo kuna watanzia wengi katika *private sector* wanahitaji kufanya vizuri lakini ni kwa sababu hatujawekeza sana katika *research and development*. *Tax base* yetu bado ndogo naamini tukiwekeza sana katika *research and development* tukawekeza kwa kiasi kikubwa *investment spending* yetu ikiwa kubwa katika *research and development* lazima *tax base* yetu itaongezeka. Kwa miaka hii na ijayo lazima pato letu litaongezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili lazima hizi sekta tatu kilimo, viwanda na biashara ya huduma lazima tufanye uwekezaji mkubwa sana *investment spending* katika sekta hizi tatu itakuwa ni tiketi pekee ya kuiondoa Tanzania katika umaskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kilimo chetu uwekezaji ni mdogo sana uwekezaji katika kutafuta masoko, uwekezaji

katika kuwa-*train* wakulima, uwekezaji katika mitaji bado ni mdogo tunaionomba sana Wizara iangalie kila namna kupata fedha kwa ajili ya kuwekeza zaidi katika eneo hili la kilimo, viwanda pamoja na biashara ya huduma hasa ile ya utalii, na uwekezaji katika sekta hizi tatu utatutoa katika umaskini kwa sababu kubwa tatu sababu ya kwanza sekta hizi tatu zinaweza kuzalisha ajira nyingi sana na kwa sababu hiyo tutakuwa tumeongeza *tax base* kubwa sana katika nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, sekta hizi tatu ndizo sekta zinazoweza kutusaidia kuongeza sana mauzo ya nje. Vilevile tukiwekeza vizuri kwenye sekta hizi tatu itatusaidia kuondoa sana *inflation* katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaombwa sana Wizara iwekeze sana katika viwanda, tutoe fedha za kutosha sana na tuweke mazingira mazuri na ya kutosha *ku-support* ukuaji wa viwanda ili tuongeze ajira kwa vijana wengi ambao sasa wamehitimu na wako *willing* kuweza kuchangia katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie sekta ya miundombinu. Miundombinu inayo-*support* utalii bado. Inasikitisha sana kuna maeneo tuna *potential*/kubwa ya utalii lakini bado miundombinu ya barabara pamoja na ya viwanja vya ndege ni shida. Leo ukienda upande wa Magharibi wa Serengeti watu wengi wanahitaji kuwekeza lakini bado ujenzi wa barabara unasuasua, tunaendelea kupoteza Pato kubwa la Taifa. Kwa hiyo niiombe sana Wizara twende na *priorities* watu hawashindwi kwa sababu hawana uwezo bali wakati mwingine tunashindwa kwa sababu ya vipaumbele visivyo sahihi. Tukiongeza uwekezaji katika sekta hizi ni lazima tutaongeza *tax base* yetu. Hivyo ni lazima mapato yetu yata-shoot tunaweza tukafikia huko mbele hata ku-*double* hii bajeti ya tirioni 36.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais katika hotuba yake Wizara mbalimbali zimeahidi mambo mengi makubwa; na sisi sote tumeona Waheshimiwa Wabunge waki-report

changamoto nyingi zilizoko majimboni. Tunaweza kufikia hili kama tutaongeza *tax base* tukakusanya mapato makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tukiangalia sekta ya utalii utangazaji bado ni mdogo, *investment* yetu katika *marketing* ya *tourism* bado ni ndogo. Sasa niwaombe sana Wizara itafute namna ya kuongeza uwekezaji katika matangazo katika vivutio vyetu tulivyonavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuweza kufanikiwa sana katika *tourism* siyo *function* ya kuwa na rasilimali nyingi, kwa maana ya vivutio vingi ila ni *function* ya *good marketing*, na hii itatokana na uwekezaji mkubwa wa fedha katika eneo hili. Niiombe sana Wizara ya Fedha katika bajeti hii itafute kila namna inavyowezekana, kila mahali tunapoweza kupata fedha tuwekeze sana katika kuendeleza *VETA* pamoja na elimu ya ufundl nchini, hawa ndio wanawenza wakatusaldla katika kuzalisha ajira nyingi tukaongeza *tax base* na tukaweza kukusanya fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nashukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Benaya Liuka Kapanga, tutamalizia na Mheshimiwa Ally Anyigulike Jumbe Mlaghila.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Kwanza kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali ya Awamu ya Sita, kwa muda mfupi ilillyoanza kufanya kazi imefanya mambo mazuri sana, imewatia moja sana Watanzania. Tulifika mahala watu walikuwa na hofu totauti tofauti lakini sasa kwa awamu hii ya sita matumaini yamerudi kwa kasi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri Dkt. Mwigulu Nchemba, nimpongeze *engineer* Masauni pamoja

na wataalamu wa Wizara hii, mmeefanya vizuri sana, niwapongeze sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kwa fedha waliyotowa. Kwa muda huu mfupi fedha nydingi imekwenda kwenye majimbo yetu. Tumepata fedha kwa ajili ya madarasa pamoja barabara na vilevile tutapata fedha za shule mpya. Kwa jimbo langu mimi niseme tu kata sita hazikuwa shule kabisa, lakini sasa tunamatumaini ya kwenda kupata shule hizi mpya. Ahsanteni sana Serikali hii ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nishukuru sana kwa wazo lile la kuwalipa Madiwani moja kwa moja kutoka Serikali Kuu ilikuwa ni kilio kikubwa sana cha Madiwani, hasa Madiwani wa halmashauri yangu ambao waliniletea kero nydingi sana. Na kabla sijapeleka kwa Waziri, Waziri ameliona hilo na tayari ametoa ufumbuzi. Ombi la Waheshimiwa Madiwani, wanasema tunashukuru sana lakini wafikiriwe kuongezewa kidogo, waongeze kidogo pale. Tunafahamu Madiwani wana kazi kubwa, wakiamka asubuhi wale ndio wanaokuwa na wapiga kura wetu, muda wote wanao shida zote wanazo, lakini wanafanya hivyo kwa namna mungu anavyowasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nishukuru sana sana Serikali kwa maamuzi haya ambayo Mheshimiwa Waziri kuititia bajeti hii alituambia hapa. Ninamatumaini makubwa sana kwamba zahanati zangu, maana tutulikuwa na maboma ya zahanati zaidi ya 34; kwa maneno aliyosema Waziri hapa sasa yanaenda kukamilika. Nilivunjija madaraja zaidi ya 24 wakati mvua hizi zilizopita. Sasa kuititia mpango ule wa *TARURA* ninauhakika yanaenda kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunashida ya kero ya hospitali sisi tulikuwa hatuna hospitali sasa hivi tumepokea milioni 500 ujenzi umeanza nina uhakikia kwa mipango hii hospitali ile inaenda kukamilika mapema iwezekanavyo; pamoja na mambo mengi mazuri, kama vile mikopo kwa wanafunzi, tulikuwa tunashida na wanafunzi, na mimi kama

Mbunge nasomesha baadhi ya wanafunzi, lakini sasa najua kupitia mikopo hii aliyotuambia Mheshimiwa Waziri hapa sasa na mimi Mbunge hapa nitapumua, nitafanya mambo mengine. Niishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivi naomba nishauri kidogo. Tumefanya vizuri kwa upande wa Madiwani lakini kiko kilio kikubwa kwa upande wa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Wenyeviti wa vijiji. Niliona mahala fulani kwenye halmashauri zenyne uwezo, ziliwahi kufanya kitu wakati fulani. Ninafahamu Serikali yetu, Serikali Sikivu, inaweza kufanya kitu kwa wenyeviti hawa wa vijiji. Kama halmashauri za manispaa ziliweza kulipa 50,000 kwa mwezi kwa wenyeviti wa mitaa ninauhakika tukipanga tukiamua tunaweza kuwalipa kitu fulani wenyeviti hawa wa vijiji, Kwa hiyo nikombe Mheshimiwa Waziri utakapohitimisha basi wape matumaini wenyeviti wetu wa vijiji nawao wapate kitu fulani, inawezekana kwa mwezi hata kwa miezi mitatu mitatu kwa kuanzia ikibidi tufanye kitu fulani kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa upande ule wa fedha za majumuisho; tumepeleka fedha milioni 500 kwa kila halmashauri kwa kila jimbo. Hata hivyo, yapo majimbo yenye ukubwa wa kipekee. Inatakiwa majimbo haya pamoja na kuwapa hizi milioni 500 tuyafikirie Zaidi, kwa sababu hatuwezi kufanana, hata vidole hivi havifanani. Yako maeneo yamefika mahala pazuri, lakini yako yana majimbo makubwa sana. Tukisema tumetoa tu milioni 500 na tukapiga makofi kwa kweli zile fedha zinaweza zisionane kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa mfano ile milioni 500 naenda kuendeleza ujenzi wa barabara ya kutoka Mbiga – Litoo hadi Ngumbo kwa Mheshimiwa Stella Manyanya, ni barabara ya TARURA, tulipata msaada pale tumejengewa kilometra 34 34 kwa kiwango cha lami, lakini sasa zimebaki kilometra 14, kwa hiyo tunaenda kuendeleza kilometra moja; unaweza ukano. Na hii ni barabara yenye kilometra nyingi sana ndani ya jimbo. Kwa hiyo ombi langu kwa Serikali, pamoja na kutoa fedha hizi tuyaangalie majimbo makubwa, tuyaongezee fedha ili zikafanye vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo kwa upande wa...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara anayozungumzia Mheshimiwa Benaya ambayo imebakiza kilometra 14 kujengwa kwa lami inayopita kwenye Ukanda wa Ziwa Nyasa ambako kuna vivutio vingi vya utalii na vivutio vingi vya asili; mimi nilikuwa tu nataka nimuongezee mchangiaji kwamba, ni vizuri sasa Serikali ikatenga pesa kwa ajili ya kumalizia kilometra 14 badala ya kutoa kilometra moja. Kwa sababu kilometra moja inakuwa haina tija labda wangetoa pesa za kilometra 14 ingeleta tija zaidi. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Benaya, malizia mchango wako.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipokea taarifa yake kwa mikono miwili, nakushukuru sana dada yangu Msongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na barabara hii mwezi wa kwanza tulipokwenda hata Mheshimiwa Waziri Mkuu alitolea maelekezo, kwamba ikamilike kwa sababu ina muhimu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nitoe ushauri upande wa kilimo. Wananchi wa nchi wamefanya vizuri sana kufikia hapa tulipofikia, kiasi kwamba kwa kiasi kikubwa

Tanzania haina njaa. Wakulima wetu wamefanya kazi wenyewe kwa nguvu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifuata taarifa za bajeti hapa upande wa huu wa kilimo hatukufanya vizuri sana, tuwe wa kweli, hatukufanya vizuri sana. Fedha zinatengwa lakini zinazokwenda ni kidogo sana, na hii ipo tofauti na nchi Jirani. Hata kwa bajeti hii tunayoijadili nchi za wenzetu kwa upande wa kilimo zimefanya vizuri zaidi kuliko sisi. Unaweza kuona Kenya wao wametenga trillioni 1.2 kwenye kilimo, Uganda wametenga *almost* hela ya kwao trillioni 45...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie dakika moja tu.

**NAIBU SPIKA:** Sekunde thelathini.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Rwanda pia wametenga fedha nydingi, sisi Tanzania tupo chini kuliko nchi za wenzetu. Kwa hiyo nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwamba bajeti inayokuja tufanye mambo makubwa, fanya, weka alama kwenye kilimo ili taifa hili likukumbuke. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 30 machi, nilimuandikia *message* ndugu yangu Mwigulu Nchemba nikimuombea kwamba ikitokea baada ya kuchukuliwa Mheshimwa Mpango kuwa Makamu Rais basi nikasema

naomba Mheshimiwa Rais ikimpendeza uwe Waziri wa Fedha; na bahati nzuri yale maombi yalitokea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanya hivyo kumuombea kwa sababu nilijua uwezo wake na nilijua uzalendo wake alionao kwa nchi hii ya Tanzania. Sasa tumeshakupata Mwigulu Nchemba na baada ya kukupata tumeshaanza kuona matunda yako pamoja na ya Naibu Waziri wako. Matunda haya hayajajificha, tumeanza kuyapata kwa kuyashika mkononi. Katika hili naomba nimshukuru sana Mama yetu, Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Ingekuwa tupo mtaani ningesema ameupiga mwangi kukupata wewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaona matunda ya kupata shilingi milioni 500. Kwa jimbo langu mimi Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa pesa hiyo tunakwenda kujenga kilometa 2.5 za lami mjini. Hii itakuwa ni alama kubwa sana ya kazi kubwa ulioanza nayo kuifanya. Maana yake ni nini? Kama naweza kujenga kwa milioni 500 kilometa 2.5 kwa kujiongeza ninaomba niilongezee shilingi zingine milioni 500 niende vijijini nikapige kazi ya mara mbili ya hiyo pesa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninaomba niseme, sifa zangu zitakuwa nyingi sana baada ya kuona matunda mengine yajayo, hasa kwenye eneo la jinsi utakavyogawanya hizi pesa zilizopo kwenye bajeti. Huko nyuma tumekuwa tukiona wakati mwingine sehemu nyingine hazifikiwi ilhali ni sehemu muhimu.

Ninaomba kama ni *ma-flyover* basi hata Tunduru kule, hata Iringa wayaone, siyo Dar es Salaam tu. Kama ni *flyover* pale Mbeya napo nani amewaambia *hai-fit?* Inakaa vizuri, tena inapendeza; ninaomba twende huko. Lakini hebu tupeleke akili sehemu zote za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapozungumza watu ambao wanastahili kupata hata ile reli ya *SGR TAZARA* inastahili ifike hapo, tuisirudi tu huku kwenye mpya, tukitengeza

TAZARA, nataka nikuhakikishie, uchumi wetu utapanda zaidi ya ulivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunapotoa hizi rasilimali Mheshimiwa Mwigulu, wakati mwingine inasikitisha. Kyela ni sehemu ambayo inapata magonjwa mengi kwa sababu ya jiografia yake. Hata hivyo tangu mwaka jana hospitali imeungua wodi zimeungua pesa leo ndiyo zinapelekwa milioni 500 tu ilhali tuliomba na kwenye bajeti ilitengwa *1.3 billion*, lakini sehemu zingine utakuta pesa zimeenda na wala hawakuunguliwa. Mimi ningombwa Mheshimiwa Waziri, hebu iangalieni Kyela kwa jicho tofauti na sehemu zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ile ndiyo inayopokea masalia yote ya maji yanayotoka milimani, lleje, Rungwe na Busekelo. Sasa miundombinu yake yote imeharibika kiasi kwamba hata kupeleka wagonjwa hospitalini ni ngumu, watu wanakufa vijijini kwa sababu hawawezi kufika haraka sehemu za kutolea huduma za afya. Kwa hiyo ningombwa hili tuliangalie si kwa Kyela tu lakini kwa Tanzania nzima. Twende tuangalie maeneo ambayo yapo *prone* namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni suala la takwimu. Katika kitu muhimu kuliko vyote kwenye uchumi ni takwimu sahihi. Leo kwenye bajeti tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya sensa ya wananchi wa Tanzania, lakini hivi tunahitaji kutenga hizo fedha? Mimi kwa mawazo yangu, nilitaka nishauri kwamba inawezekana hatukuwa na haja hiyo iwapo tungetumia vizuri sana rasilimali watu tulionayo; na nina uhakika wala tusingekuwa tunakisia idadi ya Watanzania, tungekuwa tunasema kwa uhuru tena kwa uhakika; kwamba leo hii tumeamka asubuhi tupo na watu kiasi fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tuisiwaitumie hata mabalози kwamba watoe taarifa za kila siku watu wapo wangapi hapo kwake Inawezekana ikaenda kwa mwenyekiti wa kitongoji tukatengeneza *system* nzuri ya mtandao.

Tunaweza tukawa na *computer* zikaa pale kila siku au hata kwa wiki zikawa zinatolewa taarifa za idadi ya watu waliopo hapo. Mimi nafikiri kiasi hiki kisingefikiwa tungefanyia kazi nyininge. Ninaomba sana hebu twende tuangalie takwimu zetu za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za Ulaya zimefanikiwa sana. Hakuna mtu anayelala nchini au kwenye nyumba ya mtu asijulikane yupo hapo na ameingia lini na anaondoka lini; na hata kwa usalama wa nchi itatusaidia sana. Zamani ilifanikiwa sana, hata kwa mabalozi, balozi alikuwa anajua ni nani ameingia kwenye eneo hilo na anatoa taarifa kwa nini haya tumeyaacha. Hivi, vyama vingi ndivyo vinatakiwa kuondoa hayo? Mimi ningeomba turudi huko tufanye mambo makubwa nchi yetu ipo kwenye eneo zuri na inaenda kuzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kwenye mapato ya simu. Tumesema sana na Serikali inategemea kupata kama 1.2 *trillion* kutoka kweney simu. Mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri, hebu kaa na watoa huduma wa simu wakuhakikishie uwezekano wa kupata kiasi hiki. Kwa sababu kuna sehemu kuna kuwa kama inaonekana haiwezekani ikapatikana hii. Sasa ili kuweka vizuri mimi nikuombe hebu fanya utafiti zaidi ili pesa hiyo ipatikane. Maana katika utafiti wangu nimegundua kwenye *GSM*na kwenye *M-Pesa* au *Tigo Pesa* pato lote la wao ni takriban bilioni 700. Sasa je, sisi tunaendaje hapo juu? Mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri lifuatilie hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la polisi. Tunahitaji kuwatanza sana polisi. Kuna sehemu tunasahau kuwasemea, na bahati nzuri Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Masauni wote mmepita huko. Ninawaomba nendeni mkawaboreshee mafao hawa, hawa jamaa ndugu zetu wanalala nje kila siku na tunawategemea sana.

Naomba sana polisi tuwaangalie kwa jicho linguine. Lakini pia ningeomba nikutafutie chanzo kingine ambacho kinaweza kikawa ni *privilege*, lakini pia inaweza ikaonyesha uzalendo hata kwa Wabunge hapa hapa. Hebu tengeneza

*plate number za Wabunge halafu wawe wanalipia kidogo kidogo. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *plate numberza* Wabunge tu zinaweza zikalipa. Hebu angalia hata huko kwenye Serikali sehemu ambazo tunaweza tukatafuta, zikawa na Karangi kazuri kabendera yetu, tukawa tunalipia kwa mwezi au kwa mwaka itakwa vizuri zaidi na tutaongeza mapato. Unapokuwa Dodoma huwezi kupeperusha bendera, lakini ili ujulikane huyu ni Mbunge usijifische ile *plate number* inaweza ikakusaidia, lakini iende kwa uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kusema nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ninawaombe tu viongozi wetu wote wa Tanzania waendelee kumuenzi Mungu na waendelee kumkumbuka Mungu, kwamba tupo hapa kwa sababu Mungu amelchagua Tanzania kuwa Paradiso yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza kwa siku ya leo. Kwanza ninayo matangazo machache hapa, Waheshimiwa Wabunge ambaao wataanza kuchangia mchana. Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mheshimiwa Taska Mbogo na wengine tutaendelea kuwataja kadri muda utakavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge wapo wageni ambaao walitangazwa asubuhi, lakini hawakupata fursa ya kuingia humu ndani. Kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Kenneth Nollo, ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine wakiongozwa na ndugu Peace Faraja, karibuni sana. (*Makof*)

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, ambaao ni Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA)

wakiongozwa na ndugu Peter Mwabuja, karibuni sana.  
*(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge nawaona wageni wengi kwa hiyo huenda sijajua ni wageni gani ambao walitangazwa asubuhi, lakini wamepata fursa ya kuingia sasa, ila ninayo matangazo mengine ya wageni.

Kwanza ni wageni wangu ambao ni umoja wa wanafunzi wanaotoka Mbeya wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma yaani MBESO wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Alipipi Jimmy, karibuni sana wanafunzi kutoka Mbeya tunawatakia kila heri katika masomo yenu mmalize salama na mje na nyie mtusaidie kulijenga Taifa letu. *(Makof)*

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Sylvia Sigula ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Mkoani Kigoma, sijui wamekaa upande gani, wakiongozwa na ndugu Kenneth Mpondela, karibuni sana, vijana kutoka Kigoma. *(Makof)*

Tunao pia wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, na hawa ni wa wanafunzi 40 na walimu watano kutoka shule ya Jumapili ya Watoto wa Kanisa la Moravian la Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Daudi Mwakasala, karibuni sana Bungeni Watoto wetu. *(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge nimekumbushwa hapa juu usimamizi wa kanuni. Wapo Waheshimiwa Wabunge akisimama akiwa anataka kutoka haangalii mchangiaji yupo upande gani, nawakumbusha kila wakati. Haitakuwa jambo jema ukisimama halafu uambiwe rudi ulikotoka na ndiyo utaratibu unavyokuwa ukisimama ukakatisha unaambiwa rudi ulikotoka sasa hili tusifanye hayo ndiyo maana tunawakumbusha kila wakati. Ukitaka kusimama tazama anayechangia yupo upande gani ili usipitie katikati yake yeze na mimi ninayesimamia huku mbele, kanuni zetu zinakataza.

Lakini lingine la mwisho, kukiwa na SIWA hapa mbele wanaoruhusiwa kupita ni hawa watumishi wetu humu ndani.

Waheshimiwa Wabunge kwenye mduara huu muiache SIWA inakaa peke yake. Mnaruhusiwa kupita huko pembedi na siyo hapa katikati, nadhani hilo nalo limeelekwa.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11:00 jioni leo.

*(Saa 07:10 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilitrudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na majadiliano tutaanza na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe Mheshimiwa Forent Laurent Kyombo ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Niipongeze Serikali kwa mpango mzuri ambao imetuletea. Pamoja na kuipongeza kwa sababu imekuwa ni bajeti ambayo imekwenda kugusa maeneo muhimu sana ya wananchi wetu na kutatua changamoto za wananchi wetu, lakini bado nina mchango katika sehemu tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwenye suala linalohusu elimu, kwa kuwa ili tuendelee tunahitaji tupate watu ambao watakuwa na elimu bora. Niombe sana katika mabadiliko ya mtaala wenzetu watu wa elimu waangalie na kuzingatia mazingira yetu ya Tanzania na kuona namna

gani vijana wetu watafundishwa ili waweze kupambana na mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia na elimu yetu imekuwa nadharia sana, sio ya vitendo. Watoto wanakaa darasani muda mwingi sana, hawana *practical*, kwa hiyo wanapotoka inakuwa ni shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo kipengele cha ujasiriamali, ni cha muhimu sana, mtoto lazima ajifunze kuwa ana maono au ana *vision* tangu kwenye elimu ya msingi. Kwa hiyo lazima tuangalie namna gani tutaingiza kipengele hicho kwenye elimu yetu ili tuwe na watoto wenye mipango kuanzia wadogo watengeze *road map* ya maisha yao kuanzia shule ya msingi mpaka watakapolaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno niende kwenye suala lingine linalohusiana na masuala ya miundombini, leo tunajadili bajeti ya Serikali, lakini zamani wakati Taifa letu linaanza kwenye nchi hii tuliwahi kuwa na *program* ya vijiji vya ujamaa. Nia ilikuwa ni kusogea huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii katika mipango yetu ya ardhi hata tunapokuwa kwenye shughuli zetu za kisiasa kutafuta kura, unaweza ukaona kwamba tumeacha sasa ile *program* atuangalii ni namna gani tunawapanga watu wetu kwa makazi na namna gani tunaigawa ardhi yetu kwa ajili ya masuala ya kilimo na kazi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaondoka, anakwenda anahamia kwenye mlima alikuwa mwindaji, anahamia huko analeta na mke wake na watoto wanazaliana wako mbali juu ya mlima na hakuna mamlaka ye yote iliyowaambiwa jamani hapa sio sehemu ya makazi, mrudi mkakae na wenzenu. Hii inazidi kutuongezea gharama na ndio maana sasa kumfuata yule mtu ili umpelekee huduma ya barabara, maji, afya ni mbali, yuko mbali na wenzie lakini tayari anataka kupata huduma kutoka kwenye Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweka bajeti ya kujenga barabara kumfuata mtu au kuwafuata watu 600 ambao wako mbali, unatumia zaidi ya bilioni sita au nane na wale watu wamekaa kule wanalima mbogamboga, ukiangalia *return* kiuchumi pale ni hasara. Kulikuwa kuna sababu gani hawa watu wajitenge na wenzao waende mbali wakaishi peke yao, wakati wangeweza kuishi na wenzao, tukaweza kuwashudumia vizuri pale, wakiwa wamekaa pamoja. Kwa hiyo tunaomba wenzetu hawa wa ardhi waliangalie hilo na mipango yetu iwe hivyo makazi lazima yaimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani hawafanyi mambo mapya ila wanafanya mambo yaleyale katika ubora zaidi. Leo hapa tumeava nguo lakini ni sawa tu na Adam na Eva walivyokuwa wanavaa nyasi, wao walivaa nyasi *direct*, magome ya miti na walivaa ngozi moja kwa moja, lakini sisi tunavaa ngozi *zillizokuwa processed*, vinakuwa viatu. Leo tunavaa magauni kutoka kwenye mimea ya pamba. Hicho ndicho tunachosema hatukutakiwa kuacha zile *program* za Vijiiji vya Ujamaa, lakini kuitengeneza ile *program* iwe ya kisasa na kutusaidia zaidi kwa sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *point* yangu nyingine naomba leo kidogo tukumbushana na maneno ya Mungu humu ndani. Kwa sisi wa kristu wenye biblia ya Isaya 32 mstari wa 17 unasema: "*Haki kazi yake duniani imetumwa kuleta amani, haki kazi duniani imetumwa kuleta utulivu na matumaini.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndio kazi kubwa ya haki tunaomba sana wenzetu hawa walioko Serikalini, tunapoongea watusikie na wafanyie kazi. Yapo mambo waliyofanyiwa Watanzania wenzetu kwenye nchi yetu hayana tija na yamewajeruhi na hayana tija kwa maendeleo na mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tumeongelea sana hapa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni. Wenzetu wale wengine ukiangalia ni wajane, wenzetu wale wengine ukiwaangalia walianzisha zile biashara baada ya kupata

viinua mgongo vyao, wengine walianzisha zile biashara mitaji waliipata kwa shida. Ni kweli kama Kamati ya Kudumu ya Bunge inavyosema katika Sura ya 56 ya bajeti yake na mapendekozo yake, kile kipengele cha 8.4, kwamba kulikuwa na lengo la Serikali la kuhakikisha kwamba haya maduka ya kubadilisha fedha za kigeni yanafuata sheria za Serikali na kanuni za Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, *operation iliyofanyika* kwenye yale maduka, watu hawa bado hawakutendewa haki, tunaomba haki itendeke kwa sababu mwenye kuhukumu kwenye suala la haki ni Mwenyezi Mungu. Nchi yetu tumejipambanua sana kwamba tunamtegemea Mungu na hatuna ubishi kwenye hili. Ni kweli Mwenyezi Mungu ametusaidia na tumeona aliyotupigania hata wakati wa janga la *corona*, sasa basi sisi kama viongozi tufanye hiyo *practice* kwa matendo, kama tunamheshimu Mungu tuheshimu na watu aliowaumba sisi tuwaongoze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwatendee haki wale watu wanaolia kwa ajili ya vitu vyao walivyochukuliwa, fedha zao kilizochukuliwa, mali walizochukuliwa warudishiwe. Wenzetu *TRA* tunawaomba sana, wakati fulani unakuta Mheshimiwa Rais namshukuru sana, kwa sababu alitoa kauli mwenyewe, kwamba kweli tunahitaji kodi, lakini hatuhitaji kodi ambayo ni ya dhuluma. Tunahitaji kukusanya mapato, lakini hatuhitaji ya dhuluma ndani yake. Tukusanye mapato ambayo hata tunapokwenda kumwomba Mwenyezi Mungu atusaidie, atatusikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaomba wenzetu wa *TRA* kwanza wawe wanaelewa, leo hii Mheshimiwa Rais anatoa kauli kwamba sasa kodi zote za miaka ya nyuma, miaka sita au saba iliyopita jamani basi, ukienda *TRA* ndio kwanza wanatoa *demands note* za kuwadai watu kodi miaka nane au tisa iliyopita. Unawauliza hili likoje, wanakuambia sisi tupo tunafuata maelekezo na sheria, ni kweli kauli ilitolewa kisiasa, lakini sisi tunafuata mwongozo, tunataka maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Rais anapokuwa anatoa, ameshafanya uchunguzi wa kina, kwa sababu yeye ana milango mitano ya fahamu ana vyombo vimeshamsaidia mpaka anafikia hatua ya kutoa tamko. Kwa hiyo wenzetu wafuate mambo ambayo tunawaambia tutende haki kwenye Taifa letu, tuwatendee haki, hii iendane na kesi zingine za biashara. Wapo wafanyabiashara wengi waliofanyiwa vitu vingi ambavyo havikuwa sahihi. Tunaomba sana kero zao zitatuliwe kesi zao na mashtaka yao yaangaliwe kwa kina ili kama kuna uonezi wowote uliofanyika, watu hawa waweze kusaidiwa na warudishwe kwenye hali ya kawaida ili tuendelee kujenga imani kwa wawekezaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la elimu, tumejipambanua kwamba elimu yetu haina ubaguzi na mimi hapa naomba niseme tunesema tunataka Watanzania washiriki kwenye uchumi, lakini wapo wawekezaji waliowekeza kwenye nchi hii kwenye sekta ya elimu, wamejenga shule, wamejenga vyuo, lakini namna ambavyo wakati mwagine tunawachukulia, hatuwachukulii kama ni watu ambao wanatusaidia kama Serikali kutoa huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwachukulie kama ni watu ambao wamechukuwa nafasi ya Serikali kuwashudumia wananchi na wao wana-*feel gap* ya kutoa elimu kwa wananchi. Kwa hiyo suala la kutoa elimu bure, tuwasaidie basi hata hawa *private* pamoja na kwamba wao au shule binafsi wanachaji ada, leo Serikali inashindwa nini hata kuwachangia gharama za mitihani tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale ni Watanzania wanaolipa kodi na walikuwa na haki ya kusoma kwenye *public schools* au kwenye shule zetu za Serikali, lakini wameamua kusomesha watoto wao kwa gharama na ndio walipa kodi wazuri wa nchi hii. Kwa nini leo shule ina wanafunzi 10 kwa sababu hajifikisha wanafunzi 35 inatakiwa ilipie wale wanafunzi 25 ada za mitihani hata kama hawapo. Kwa hiyo, katika nchi hii bado tuna malipo hewa kwenye

elimu, imefanyika michakato ya wafanyakazi hewa, lakini sisi kwenye sekta ya elimu na Wizara ya Elimu bado watu wanalipa ada za mitihani hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema hivi namaanisha kwamba, ikiwa huna watoto 35, una watoto 10 unachajiwaa fedha ya watoto 35. Hawa watu wanawekeza *return on investment* kwenye elimu inachukua miaka 10, ndio mtu aanze kupata faida kwa hiyo tunawaomba wenzetu wa Wizara wajue hawa ni *partners* wetu, hawa ni Watanzania, wamewekeza kwenye elimu, tunaomba wasaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyaraka za elimu pia ziangaliwe. Tuna tatizo kubwa sana tunaweza kuona la kawaida, leo tunatangaza shule zote zitafunga tarehe 30 mwezi wa Sita, tunaomba tuulizane maswali, je, miundombinu ya kuwasafirisha wale watoto wetu kutoka kwenye mashule kwenda kwa wazazi wao tuna uhakika ipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto kubwa unakutana na watoto wamelala stendi, Mbunge unapigiwa simu sijui watoto wa shule gani wamekosa basi wamelala *stand* au mabasi ndio yametolewa mabovu wakati ule, wamepakiwa watoto wetu wanalala njiani unapigiwa, usalama wao unakuwaje? Kwa sababu mabasi yanayotumika ni yale yale ambayo siku zote ndio yanasaferisha abiria. Yakinika mengine ni mabovu kwa sababu hakuna mtu atakayenunua basi asubiri tu msimu wa shule kufunga asafirishe tu wanafunzi. Kwa hiyo watu wa wizara tunaomba watusaidie katika waraka mbalimbali wanazozitoa na maelekezo wanayoyatoa, basi wawe wanaangalia na mazingira na hali halisi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno haya, nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, atachangia kwa dakika tano; Mheshimiwa Frorent Laurent Kyombo, naye dakika tano na atafuatiwa na Mheshimiwa Abood.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Kwanza nianze kusema tunaipongeza sana Serikali kwa vile ambavyo wameandaa bajeti yao kwa kuzingatia maoni mengi ya Wabunge na wamewatendea haki kwa sababu kazi za Mbunge ni pamoja na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana mama kwa namna ambavyo anaendelea kusikiliza na kupokea michango ya vijana wa Tanzania. Tarehe 22 mwezi wa Tano nilisimama kwenye Bunge hili Tukufu na kuchangia kuhusiana na mambo ya *blockchain technology*, *cryptocurrency* na *digital currency* na tarehe 13 mwezi huu mama aliweza kutoa kauli na kuwaomba *BOT* waweze kuendelea kufuatilia teknolojia hii kujifunza ili nasi tusiweze kuitwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito huu wa mama umepelekea kufanya aingie kwenye orodha ya marais wachache ambaao wameonyesha kuongea kitu kikubwa sana duniani na kuunga teknolojia mpya ambayo inaweza ikaleta uchumi mkubwa lakini kuongeza ajira kwa vijana lakini na kuchochaea uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya kufupisha muda naomba niendelee kuiomba Serikali na kuishauri kwamba, *BOT whether taasisi zozote za kifedha kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango*, watakapokuwa wanaunda Kamati zao tunaomba ushirikishi kwa vijana wa Kitanzania ambaao wanauelewa ili waweze kuwasaidia, lakini elimu iendelee kutolewa kwa sababu elimu ni bure itawafanya Watanzania hawa waweze kuelewa na wasiendelee kudanganywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hilo naomba, wakati tunaendela kusubiri *BOT* waendelee kuamua na kujifunza kwamba uko mfumo ambaao unatumika kwenye hizi *online business*, unaitwa *PayPal*. Ikiwa kama *BOT* imekubali kwamba Watanzania hawa waweze kulipa kwa kutumia *PayPal*, lakini wao hawawezi kupokea malipo kwa kutumia

*PayPal*, tunaomba basi *BOT* tena waone namna gani watawasaidia hawa vijana wa Kitanzania ambao wanalahazimika kutoa hela nje ya nchi, lakini wao hawawezi kupokea na wanalahazimika kutumia nchi za jirani kulipwa na hivyo kupoteza mapato yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri wangu mwingine kwa Serikali kuhusiana na teknolojia ya miundombinu. Hapa nataka kuongelea *nanofiber technology*, kwa ajili ya muda nitafupisha tu, kwamba, teknolojia hii ina faida nyingi sana na ina faida nyingi sana especially kwa barabara ambazo zinatusumbua vijiji sisi Wabunge ambao tunatokea vijiji. Hata hivyo, teknolojia hii inaweza ikatumika hata mjini *nanofiber technology* wataalam wanasema kwanza ina *PSI* 11,000, kwa hiyo ina maana kwamba ina uwezo wa kuhimili kiwango ambacho lami haiwezi kuhimili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lami juu linapowaka magari makubwa yanapopita inatengeneza vitu kama mbonyeo. Kwa hiyo inapelekeea Serikali kupoteza hela nyingi inapokuwa ina-*maintain* zile barabara, lakini *nanofiber technology*, Serikali itakapoamua kuitumia inaendana na mazingira yote hata kwenye zile mbuga zetu za wanyama ambako hatuwezi kuweka lami kwa sababu tunaogopa teknolojia ambayo tunatumia sasa ina *emission*, lakini teknolojia hii iko vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *nanofiber technology* ina uwezo wa ku-save gharama ambazo zinatumika kujengea lami za sasa kuanzia asilimia 25 mpaka asilimia 50. Kwa hiyo unaweza ukaona ni kwa kiasi gani Serikali itakapoamua kutumia teknolojia inaweza ika-save mapato yake, sitaweza kuendelea nitaandika andiko kwa ajili ya muda ili niseme vitu vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba kuchangia kwenye suala la miradi hii ya kimkakati na nifupishe. Kwenye hii miradi ya kimkakati naomba niongelee mradi wa kimkakati ambao uko ndani ya Jimbo la Mwomba mradi wa chumvi. Kwenye soko letu la Tanzania inaonyesha

kwamba kiwango cha chumvi ambacho Tanzania inahitaji ni tani milioni moja na laki tatu na kuendelea, lakini viwanda vyetu vya ndani kwa mfano Uvinza; viwanda vilivyoko Pwani au viwanda viliko huko Lindi vina uwezo wa kutengeneza tani za chumvi 270,000 tu. Kwa hiyo Serikali inapelekea Serikali kuangiza chumvi nydingi kutoka Nchi za Kenya na zingine ili tuweze kutosheleza soko la ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali ikiwa miradi hii ya kimkakati tulilileta kwa lengo tu kwamba iweze kuzisaidia halmashauri kuongeza mapato yake, lakini iweze kutoa ajira kwa Watanzania na tuweze kuimarisha viwanda vyetu vya ndani, tunaomba Serikali irudi na kupitia tena kuangalia miradi hii ya kimkakati ikiwa ni pamoja na hiki Kiwanda cha Chumvi ambacho kipo Ivuna kwenye Jimbo la Mombasa. Wakati kiwanda hiki kinaendeshwa na *TRC* kilikuwa na uwezo wa kuzalisha tani mpaka 25,000, lakini toka kiwanda hiki kimerudi kwenye mradi wa kimkakati kinazalisha chini ya tani 100. Kwa hiyo tunaomba Serikali ipitie tena ili tuweze kunufaika na miradi hii ya kimkakati, iweze kwenda kutimiza lengo ambalo lilikusudiwa kwa Watanzania hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Azizi Abood na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi ili niweze kuchangia katika mapendekezo ya bajeti ambayo yamewasilishwa kwetu kwa nafasi ya pekee nikushukuru kwa nafasi lakini pia nimshukuru Rais wetu, Mama yetu mpendwa, Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuja na bajeti yake ya kwanza ya Awamu ya Sita ambayo kwa kweli inalenga kabisa katika dhima ambayo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, salamu hizi za pongozi zimfikie Rais, lakini ziwafikikie wasaidizi wake askari wake wa miavuli ambaye ni Waziri wetu wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Mwigulu Nchemba Madelu, lakini pia na msaidizi wake Mheshimiwa Masauni Masauni na watendaji wengine wa Serikali bila kusahau michango ya Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Bajeti ambayo inaweza kuboresha mpaka bajeti yao inakuja imesheheni maono mazuri kwa ajili ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia katika maeneo mbalimbali, nikaona kwamba bajeti yetu hii inaakisi na imeweza kugusa katika makundi mbalimbali ya wananchi ndani ya nchi yetu na hakuna kundi lilobaki. Tumeona katika maeneo ya watumishi ni maeneo mengi ambayo yameguswa kwa ajili ya kuhakikisha sasa watumishi wanakuwa na ari ya kazi kwa kuweza kutenga fedha kwa ajili ya kuwapandisha vyeo, zaidi ya bilioni 449 zinatengwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sisi wote tuunge mkono Serikali kwa kuzipitisha kwa kishindo. Pia tunaona, PAYE, kodi ya mshahara wa mtumishi inapunguzwa kutoka 9% kwenda 8%. Ni mambo mengi mazuri kwa watumishi ambaye tumeona katika Jeshi letu la Polisi, muda wa kuajiriwa katika mkataba wa kudumu unapunguzwa kutoka miaka 12 kuja miaka sita. Tunaona Watendaji wa Vijiji wakipewa posho na Maafisa Tarafa Sh.100,000 kila mwezi. haya ni mambo ya kumshukuru Rais wetu mpendwa, lakini na maono mazuri ya wasaidizi wake, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuja na mambo mazuri ambayo yanagusa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika eneo hilo tumeona kundi la wanasiasa nalo limeguswa kwa kuona kwamba wawakilishi wa wananchi ambao ni Waheshimiwa Madiwani, na wenyewe posho zao zitokE Mfuko Mkuu wa Serikali Hazina. Mtu ambaye hawezi kuelewa umuhimu wa suala hilo, mimi katika wakati wangu wa maisha niliwahi kutumika kama Mkurugenzi. Nilipoenda kwenye Halmashauri hiyo, nilikuta Waheshimiwa Madiwani hawajawahi kulipwa

posho zao kwa miezi 12. Kwa hiyo, ilikuwa ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naona Serikali imekuja na njia Madhubuti ya kuweza kutatua tatizo hili ambalo lilikuwa la muda mrefu, kuhakikisha Madiwani wetu wanalipwa kwa wakati. Kwa hiyo, niendelee kumpongeza Rais wetu, Waziri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wengine ambao wamewezesha hili suala kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa ajili ya vijana wetu. Vijana hawa tunawawezesha kupitia asilimia nne za Halmashauri; tunawapa mikopo wanununa bodaboda na wengine wanaajiriwa na wenye bodaboda. Kwa siku moja, kijana wetu anayeendesha bodaboda kipato chake ni shilingi 7,000 mpaka shilingi 10,000. Akikutana na faini ya shilingi 30,000 aidha bodaboda hii analitekeza au analiacha hapo kwa siku nne anakimbia kazi. Kwa hiyo, kwa shilingi 10,000 hata akikopa, maana yake anajua ndani ya siku mbili anaweza kurudisha hizo fedha. Tuendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais na Wizara kwa michango mizuri ya namna hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwa kundi la wananchi ambalo Serikali imeliona hasa kwa kuangalia yale maeneo mahususi kwenye maeneo ya maji, barabara, afya na Bima ya Afya kwa Wote pamoja na uboreshaji wa elimu. Katika eneo hili tunaona tunakwenda kuchanga shilingi mia moja, mia moja katika kila lita ya dizeli na petroli. Ni suala ambalo ni zuri. Naiomba Serikali iendelee kulismamia ili sasa wenzetu wanaomiliki vyombo vya usafiri wasije wakaona ni sababu ya kupandisha gharama za usafirishaji. Kwa hiyo, Serikali iweze kutoa bei elekezi za nauli na gharama za usafirishaji ili isije ikawa ni mzigo tena kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili, tunaona tozo ya shilingi 10 mpaka shilingi 10,000 kwa muamala wa fedha wa kutuma na kutoa, lakini tozo ya shilingi 10 hadi shilingi 200 kwa laini ya simu ambayo tutaweka fedha; eneo hili niseme, Waheshimiwa Wabunge huku sisi wote ni mashahidi. Wote katika eneo hili tunakubali kuchangia kwa

kuwa kila Mbunge hapa leo anaweka na kutoa fedha. Kwa *nature* ya wateja wetu tulionao, kwa siku wanapiga simu nydingi kulingana na wateja wetu tulionao katika majimbo yetu, lakini kila Mbunge hapa yuko tayari kutoa hizo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tuwasihi na wananchi wetu wapendwa, suala hili ni zuri. Tunachoomba sasa Serikali iendelee kusimamia vizuri katika eneo hili, barabara zijengwe, maji yafike kwa wananchi, umeme ufile, lakini pia na bima kwa afya kwa wote iweze kufika kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aziz Abood atachangia dakika kumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo na Mheshimiwa Eric Shigongo ajiandae.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti ya mwaka 2021/2022. Natumia nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya. Nawapongeza Mawaziri wote, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu, kwa kazi nzuri mnayoendelea kuifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri wa Fedha na Naibu wake kwa bajeti nzuri sana. Naunga mkono bajeti kwa asilimia 101. Ila hii moja naitoa kwa sababu katika kusoma bajeti yake, hakuitaja Simba, kaitaja Yanga peke yake. Kwa hiyo naibakisha asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijikite kwenye Sera ya Viwanda. Tanzania tupo kwenye Sera ya Viwanda. Ili tuwe na viwanda vingi ambavyo vinamilikiwa na wazawa wenyewe, lazima tuwe na *investment banks*. Tanzania hatuna

*investment banks*, tunayo moja tu ambayo ina mtaji mdogo. Lazima tuwe na *investment banks* zenyе mitaji mikubwa ambazo zinaweza zikakopesha na wananchi wakawenza kufungua viwanda vikubwa vitakavyotoa ajira nyingi kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukichukulia kwa mfano *TIB*, tuna benki moja tu Tanzania na mtaji wake ni mdogo. Ukichukua majirani zetu Wakenya, wana *investment banks* karibu kumi na riba yao iko chini, 4%. Sisi hapa Tanzania riba yetu ni kuanzia asilimia 12 mpaka 18. Kwa hiyo ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba tujitahidi; na hasa hizi *pension funds* zote tungezifanya pia *investment banks* ili ziweze kutoa mikopo ya muda mrefu kwa wawekezaji wazawa wa Tanzania na mikopo mikubwa ili kuwekeza katika viwanda na kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye viwanda vya kilimo bado tuko nyuma sana, tunahitaji lazima tuwekeze kwenye viwanda hivi. Viwanda hivi vinategemea sana wakulima. Sasa jinsi ya kuwakopesha wakulima nayo vilevile Serikali iangalie. Kwa sababu ukitazama wakulima wa nchi mbalimbali duniani, huwa wanakopeshwa kwa riba ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukichukua Malaysia ambao ni wakulima wakubwa wa mawese; *minimum* mkulima anakopeshwa shilingi bilioni tano kwa ajili ya kilimo cha mawese kwa miaka kumi. Hapa Tanzania *agro-processing* inahitaji tuwe na sera ya muda mrefu, siyo ya mwaka kwa mwaka, ili wakulima wajitayarische; na wenye viwanda wanaokopa wawe na sera ya muda mrefu ya kuweza kuzalisha mazao haya, kama ni mafuta ya kula, kama ni nini, ili kama anakopa anaweza akarudisha mkopo wake kwa muda wa miaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala lilishawahi kutokea mwaka 2004. Wakulima walilima sana alizeti, baada ya kodi ya mafuta kupanda. Baada ya mwaka mmoja kodi ikaondolewa, wakulima wakazima. Kwa hiyo, mimi naomba sera iwe ya muda mrefu, siyo ya mwaka kwa mwaka ili

viwanda hivi vya *agro-processing* viweze kujipanga kwenye kilimo kwa muda mrefu na wakikopa wajue kabisa kwa miaka kumi, sera haitabadilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, linguine ni kuhusu pesa za wahisani zinazokwenda kwenye miradi mikubwa. Pesa hizi naishauri Wizara ya Fedha kwa kumtumia Msajili wa Hazina, wafuatilie. Kwa mfano, Morogoro, tumejata Euro milioni 70 kwa ajili ya mradi wa maji, ambayo ni sawasawa na shilingi bilioni 180, lakini Wizara ya Maji mpaka leo hatujui kama hizo pesa zimefika na Morogoro mradi hakuna. Sasa tunataka tujue, hizo pesa ziko wapi ili mradi wa maji uanze? Sasa Hazina nayo itusaidie kutupa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amekuja kule, ametumbua tumbua, hatujui pesa ziko wapi? Kwa hiyo, naishauri Serikali kwa kumtumia Msajili wa Hazina, miradi mikubwa kama hii ingekuwa inafuatiiliwa ili tuwe tunapata majibu ya haraka kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tu,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda wangu umekwisha. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Umemaliza kuchangia au bado? Kwa sababu naambiwa hapa hiyo ilikuwa ni kengele ya kwanza. Ama umemaliza?

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimemaliza. (*Makof/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Taska Restitura Mbogo, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric Shigongo na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kutupa uhai. Vile vile napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, jemedari wetu, mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi tukiwa kama wanawake nchini Tanzania tunatembea kifua mbele kwa ajili yake na tunamuunga mkono na tutaendelea kumpambania hata kule katika majimbo yetu kwa kuyaeleza yale mazuri yote anayowafanya wananchi wa Tanzania. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa yafuatayo: Kwanza kabisa, ameweza kuongea na wazee pale Jijini Dar es Salaam, aliweza kuongea na viongozi wa dini, aliongea na sisi akina mama hapa Dodoma na pia aliongea na vijana pale Mwanza na kukubaliana na maombi ya vijana kwamba wataunda Baraza lao la Vijana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuja na bajeti nzuri ambayo imekwenda kuwapunguzia kodi wafugaji, wakulima pamoja na wale wenye *NGOs* zao. Pia ni kodi ambayo imeangalia mpaka yule mtu wa hali ya chini, bodaboda kwamba kipato chake ni cha chini na kuweza kumpunguzia kodi ya adhabu kutoka shilingi 30,000 kwenda shilingi 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi za Mheshimiwa Rais, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu wake, Mheshimiwa Engineer Masauni kwa bajeti yao nzuri sana ya mwaka 2021/2022. Nawapongeza sana watendaji wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na Katibu Mkuu pamoja na Gavana wa Fedha, Mheshimiwa Luoga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Naibu wake kwa kuja na wazo la kukusanya *Property Tax* kutoka kwenye Luku. Pia nawapongeza sana kwa sababu *area* hii ya ukusanyaji wa kodi ilikuwa imeleta shida, Halmashauri zilishindwa kukusanya, lakini *TRA* pia walivyopewa walishindwa kukusanya. Kwa hiyo, kwa kuja na wazo hilo, nawapongeza sana. Naomba mawazo hayo wayapeleke pia kwenye *land rent*, waweze kutafuta utaratibu ambao viwanja ambavyo vimepimwa nchini kwetu Tanzania vitawenza kukusanya kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, nawapongeza pia kwa suala la kuja na kodi ya miamala ya kwenye simu na tozo zile kwenye vocha tutakazokuwa tunaweka kwenye simu. Hii inamfanya hata Mtanzania wa hali ya chini aweze kuchangia kodi ya nchi yake. Kuchangia kodi ya nchi, ndiyo utaratibu wa nchi zote duniani. Hii itamwezesha mwananchi kuiuliza Serikali ni kwa nini haijajenga barabara? Ni kwa nini haijaleta maji kwenye eneo? Kwa nini haijajenga kituo cha afya; zahanati pamoja na kuhudumia wananchi kwa ujumla? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kuzungumzia Mkoa wangu wa Katavi. Sisi katika bajeti iliyopita tuliahidiwa kujengewa reli kutoka pale Mpanda Mjini kwenda sehemu moja inaitwa Karema ambako kuna bandari ambayo itakuwa inapokea mizigo kutoka Kongo. Naomba tu hili zoezi la ujenzi wa hiyo reli lisiishie kwenye karatasi, litekelezwe ili wananchi wale wa Mkoa wa Katavi waweze kufanya biashara kwenda Kongo na pia Taifa letu la Tanzania liweze kupata kipato kutokana na ushuru utakaotokana na wale wafanyabiashara ambao watapitisha mizigo yao. Maana yake hiyo reli ikiisha, mizigo utakuwa unatoka Dar es Salaam unapita Tabora - Mpanda mpaka kwenye Bandari ya Karema. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuliahidiwa barabara ya lami kutoka pale Mpanda Mjini kwenda kwenye hiyo Bandari ya Karema. Naomba pia Waziri wa Fedha asije akatusahau. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kupongeza miradi iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, kama Mradi wa Umeme wa *Stiegler's Gorge*. Ni umeme ambaao utauzwa mpaka nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eric Shigongo, atachangia kwa dakika kumi, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu atafuatia na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kwa Taifa langu katika bajeti hii ya mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijazungumza mengi, naomba nitoe shukrani nyingi sana kwa Serikali ya Awamu ya Sita; kwa Mheshimiwa Rais kwa mambo ambayo mimi peke yangu, sijui kwa wenzangu; amenitendea kwenye jimbo langu. Katika historia, tangu mwezi Januari mpaka Aprili, nimeshapokea karibu shilingi bilioni tatu za maendeleo.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo, mimi na Wabunge wenzangu tulipata nafasi ya kukutana na Mheshimiwa Rais kabla hajaja Mwanza kwenye kikao kidogo, nikawa nimeomba kupewa kituo cha afya kwenye Kisiwa cha Maisome. Ni jana Waziri wa TAMISEMI, dada yangu Mheshimiwa Ummy, alinipigia simu ya kwamba kituo hicho kitajengwa. Kwa hiyo, natumia nafasi hii kuishukuru sana Serikali hii kwa usikivu na namna ambavyo inafanya kazi kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango nitakaoutoa leo nilikuwa nimetarajia kutoa wakati wa Wizara ya Afya, lakini bahati mbaya nafasi haikupatikana. Hata hivyo, kwa sababu tuna Wizara ya Fedha na Waziri wa Fedha yuko hapa na ndio

mpangaji wa *ceiling* za kisekta na Wizara zote, ni vizuri nikazungumza suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uhusiano mkubwa sana (*correlation*) kati ya afya za watu na maendeleo ya Taifa. Kuna uhusiano mkubwa sana. Wanasema *there is a correlation between the wellbeing of the people and socio-economic development*. Nchi yoyote ambayo watu wake hawana afya, haiwezi kuwa nchi yenye maendeleo. Nchi yoyote ambayo vijana wake ni wagonjwa, haiwezi kuwa nchi yenye maendeleo. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuwa na Taifa lenye afya. Watu wenye afya wataleta maendeleo ya nchi yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama huo ni ukweli, nataka nikurejeshe wewe na Wabunge wenzangu kwenye Azimio la Abuja. Mwaka 2001 mwezi Aprili, nchi zote za Afrika ikiwemo Tanzania chini ya *OAU*, walikutana Abuja na zikakubaliana na wakaazimia ya kwamba *fifteen percent* *ya annual budget* itaelekezwa kwenye huduma za afya. Hayo yalikuwa ni makubaliano. Hayati Mzee Mkapa alikuwa pale na wote walikubaliana na nchi zote zikakubaliana kwamba kila tunapopanga bajeti yetu, asilimia 15 lazima iende kwenye afya kwa sababu tunataka kujenga Taifa la watu wenye afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, miaka 20 baadaye; nina habari ya kusikitisha kuhusu azimio hilo ya kwamba hatujaweza bado kutimiza suala hilo, nafahamu ya kwamba tuna matatizo ya bajeti, uchumi kwenda taratibu, lakini ipo sababu ya Wizara ya Fedha kutazama na kupanga jinsi ya kuiwezesha Wizara ya Afya iweze kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka 20 baadaye, nitakupa mfano wa mwaka 2017 na 2018 tulikuwa asilimia 7 tu, ya bajeti yetu kwa Wizara ya Afya na hiyo ilikuwa chini ya azimio la Abuja ambalo lilitaka asilimia 15. Mwaka 2018/2019 tulishuka na kwenda asilimia 6.7 inaendelea kushuka bajeti ambayo inatakiwa kuhudumia afya ya watu wetu. Mwaka 2021/2022 bajeti tunayojadili hapa leo tumeshuka mpaka asilimia 2.7 maana yake nini, maana yake ni kwamba tuna

bajeti ya trillioni 1 kwa afya, lakini tuna trillioni 36 *annual budget* hiyo peke yake inaashilia ya kwamba tumeshuka mpaka 2.72 percent hiyo ndiyo *allocation* yetu kwa afya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi kama tunaweza kuwa na Taifa lenye afya kwa bajeti ambayo tumeipanga kwa mwaka huu. Nafahamu kabisa ya kwamba tuna matatizo kama nchi, nafahamu ya kwamba mnahitaji kufunga mkanda kama Taifa. Lakini afya za watu wetu ni kitu cha muhimu sana na kikubwa kabisa ambacho nataka nikizingumzie hata hiyo kidogo ambayo tunaipata, tunai-*allocate* yote huwa haiendi kwenye wizara. Tunawezaje kuwa na Taifa lenye afya linaloweza kujenga ustawi wa watu wake wakachangia utumishi wake, hatuwezi mpaka tuweze kuhakikisha ya kwamba hata kama hatuendi 15 percent, lakini lazima tuweze kupandisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kodi hapa, kodi mpya tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri, tumekuja na kodi mpya, kodi ya simu, kodi ya majengo, kwenye mafuta tumeweka shilingi 100 na fedha hizi zimeelekezwa kwenye ujenzi wa miundombinu, kwenye elimu, kwenye maji na vilevile kwenye afya, ndiyo maana nazungumza hapa leo ya kwamba ipo sababu kubwa sana ya Mheshimiwa Waziri atakavyopata fedha hizi azielekeze kwenye afya za watu wetu ili bajeti iweze kuongezeka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupe mfano, mfano huu ni wabajeti ya Wizara ya Afya mwaka 2019, nitakueleza jinsi ilivyogawanywa, asilimia 41.9 kwa mujibu wa *health forum* chini ya UNICEF ilielekea Wizara ya Afya na nyingine asilimia 40.7 ilielekea kwenye TAMISEMI ambayo ndiyo watekelezaji wa Sera huo ndiyo ulikuwa mgawanyo, nyingine ikaenda NHIF asilimia 10, nyingine 0.4 ikaenda TACAIDS sasa tuachane na hizo zilioenda TAMISEMI tuachane na hizo zilioenda NHIF na TACAIDS.

Mheshimiwa Naibu Spika, twende moja kwa moja kwenye iliyokwenda Wizara ya Afya, nionyeshe namna ambavyo fedha hiyo iliweza kutumika na nionyeshe ni kiasi

gani kama Taifa hatupo *serious* kwenye suala la kuzuia magonjwa yasitokee.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokifanya ni kama tunatamka hivi ugueni mkishaugua mje tutawatibusi, kama Taifa nimeona hatuna *capacity* ya kuwatibusi watu wote wanaougua ipo sababu ya kuyazuia magonjwa kabla hayajatokea. Leo hii wote tunafahamu ya kwamba kansa inatafunaa Taifa letu, lakini wangapi wanafahamu ya kwamba kansa inayotusumbua inasababishwa na *Aflatoxin* sumu kuvu ambayo ipo kwenye mazao. Niishukuru sana Wizara ya Kilimo wanajenga ghala kwenye jimbo langu kwa ajili ya kuhifadhi mazao ili watu wasiweze kuhifadhi mazao vibaya hatimaye kukawa na sumu kuvu ikawasababishia kansa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo ni suala la elimu tu, ni elimu peke yake ikitolewa hapa nchini watu wataweza kuepuka kansa inayosumbua Taifa. Wizara ya Afya asilimia 41.6 inayokwenda kule 33.5 inalipa mishahara, asilimia 31.8 inakwenda kwenye *capacity building* mambo ya kuelimisha watu, kuelemisha watumishi wetu wa wizara ya afya ili waweze kufanya kazi vizuri, sina tatizo lolote na *capacity building* hata kidogo ni sawa, lakini asilimia 31.8 *capacity building*, asilimia 7.1 inakwenda kwenye tiba, sasa sikiliza hapa, asilimia ngapi inakwenda kwenye *preventive medicine*, asilimia inayokwenda kwenye *preventive medicine* ni asilimia 3.7, tunawezaje kuzuia watu wetu wasiugue kwa asilimia 3.7? Hiyo ndiyo hoja yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nazungumza hapa leo natoa mchango wangu kumkukumbusha Mheshimiwa Waziri na nimeikubali bajeti yake na haya kama hayatafanyiwa kazi hivi sasa, yafanyiwe kazi huko mbele tuongeze bajeti yetu kwenye *preventive medicine* asilimia 3.7 haitoshi kuzuia watu wetu wasiugue.

Mheshimiwa Naibu Spika, napozungumza hapa leo, tarehe hii ya leo *infant mortality rate* kwenye Taifa letu, watoto wanaokufa chini ya miaka mitano wanakufa watoto 60 katika kila watoto 1000, katika kila watoto 1000 watoto 60 wanakufa.

Navyozungumza leo kwa mambo ambayo yangeweza kuzuiliwa kwa elimu peke yake, leo ninapozungumza hapa, leo siku ya leo, jioni ya leo *mortality rate* ya kinamama wanaojifungua ni wakina mama 558 katika kila vizazi 100,000, tunawapoteza wakina mama wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki mbili zilizopita mama kapoteza maisha akiwa ndani ya Mtumbwi anaenda hospitali mtoto katanguliza mkono, tutawazuiaje wakina mama wasiendelee kufa mpaka tutenge elimu, pesa ya kutosha, wakina mama wetu wasiendelee kuugua, inawezekana. Navyozungumza leo hapa *hepatitis B*, Homa ya Ini ni asilimia 6 watu wengi wana Homa ya Ini tunaweza kuwazuia kwa kuwachanja watu wetu kuna shida gani kama *NHIF* wakikubali Chanjo ya Homa ya Ini iingie kwenye Bima ya Afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuendelea kupoteza maisha ya watu wetu ni lazima sasa Mheshimiwa Waziri akumbuke suala la muhimu sana kwenye Taifa hili *preventive medicine* tuzue watu wetu wasiugue kwa kuongeza bajeti angalau kutii azimio ambalo tulilisaini wenyewe, Azimo la Abuja, Abuja *declaration*. Nchi yetu inapita kwenye wakati mgumu na ninafahamu nani wajibu wetu kama watanzania kujua tunawezaje kufunga mkanda ninachokiomba, Mheshimiwa Waziri nakusihii rafiki yangu wakumbuke Wizara ya Afya uokoe maisha ya watu ambaao hawatakiwi kuugua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo dakika tano, Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwa hizo dakika tano. Sitoacha kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri

mwenye dhamana ya wizara hii ya fedha na Mheshimiwa Naibu Waziri wake na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri waliyofanya kutuletea taarifa hii ya hotuba ya bajeti na hali ya uchumi wa nchi yetu ambayo imeeleweka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nitajielekeza katika maeneo machache na hasa katika mazingira ya Sera ya Mapato pamoja na Sera ya Matumizi. Katika Sera ya Mapato pamoja na kuendelea kutekeleza mpango mzuri wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji wa viwango Mheshimiwa Waziri ametuelekeza eneo la mapato ataliangalia sana kwenye maeneo ya kodi, tozo na ada mbalimbali na hapa ndiyo nataka kusema, moja ikiwa ni kodi ya majengo sura 289.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka sana nakubaliana sana, zilikuwepo *option* nydingi sana, lakini hii moja aliyoichukua Mheshimiwa Waziri yakutumia mifumo ya *LUKU* ni moja ya utaratibu mzuri sana kati ya taratibu nydingi ambazo zingeweza kuwepo. Na hii kwa sababu ameona uchumi wa sasa unakwenda na teknolojia ya *TEHAMA* kwa hiyo, akaona ni vizuri tuelekee na njia hiyo nami nampongeza sana. Lakini pia limesaidia wale ndugu zetu wa Chama chetu cha Mapinduzi walikuwa wanatumika vibaya sana katika eneo hili bila tija yoyote kwa hiyo sasa kwa njia hii wanaenda kupumzika na fedha nydingi tutazipata katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia eneo la Ukaguzi wa Umma sura 418, Mheshimiwa Waziri ametuambia hapa nia ya Serikali kupeleka *CAG* akakague makampuni yetu yale ambayo Serikali ina *HISA* chache *minority interest* ni jambo zuri, lakini linachangamoto kwa haraka. Moja ya changamoto; linaweza likatuletea shida kwenye uwekezaji, hizi *minority interest* tulizonazo kwenye makampuni yale, yale makampuni yana utaratibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili ambalo ni changamoto; ni katika eneo la Bodi ya *Directors*, yale yanasmamiwa na bodi zao, bodi zao zina taratibu zake, kwa hiyo nia yetu nzuri kupeleka *CAG* akafanye kazi mle, lakini

hebu tuone kama hizi bodi zao zina uwezo wa kupeleka KPMG na wengine wengi *priest house* Water, Beroke and Tuch na wengine hebu tuone katika maangalizo hayo ili tuweze kwenda sambamba. Lakini tunajua mpaka sasa CAG mwenyewe hajawenza kukamilisha asilimia 100 ya ukaguzi wa yale ambayo yanatakiwa kwa Mujibu wa Sheria. (*Makoffi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema pia maeneo mawili ya mwisho katika eneo la mapato, moja ni eneo hili la ushuru wa barabara na mafuta, jambo nzuri sana tumeelekeza shilingi mia kwa *petrol/na diesel/sisi* tunalifurahia kwa sababu tunaenda kuongeza fedha takribani bilioni za kutosha ambazo zitaenda kutusaidia kwenye barabara zetu za *TARURA*. Na hii lazima niwaambie wananchi wa Kibamba wafurahie hili walifurahiye jambo hili. Kwa sababu barabara za jimbo lile ndiyo barabara changamoto kwa Mkoa wa Dar es Salaam bilioni hizi zaldi ya 399 ziklongezwa mule maana yake *TARURA* watapata fedha na fedha zaidi ya bajeti waliokuwa wamewekewa awali, sasa wananchi wategemee barabara zao zitapitika kwa wakati wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo tozo ya posta na mawasiliano hii ni shilingi 10 hadi shilingi 200 hii nataka niwaambie wananchi wangu waieleewe vizuri sana hii inatija na itatusaidia sana, itatusaidia kwa sababu fedha hizi zinaenda kuongeza bajeti ya maji na ndiyo Mkoa wa Dar es Salaam una asilimia 92 za mafanikio katika wizara, lakini asilimia 8 hakuna maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikisema hapa hizi ni shida ambazo ziko ndani ya Kibamba, sasa wakikubali kulipa hizi shilingi 10 hadi 200 maana yake tunaenda kuongezewa zaidi ya bajeti iliyokuwa imepangwa katika wizara hii na maji yanaenda kupatikana vizuri ndani ya Kibamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini upande wa sera ya matumizi kwa haraka, nitasema kidogo hapa juu ya fedha zinazotumika mwisho wa mwaka kuzibakiza ndani ya Sekretari zetu za Mikoa kama tulivyokuwa tumeomba sisi wenyewe

Waheshimiwa Wabunge jambo nzuri na mimi nalikubali, linamaangalizo. Sheria iko vizuri sheria ya fedha lbara ya 29(1) hadi (5) inazungumzia *unspent* amount katika mwisho wa mwaka wa fedha ni vizuri zirudishwe katika mfuko mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunasema hazitorudi so zimekwenda kwa kuchelewa vizuri lakini *regulation* ikatueleze vizuri na ije hapa kwenye Bunge lako Tukufu ili tuweze kuweka vizuri muda sasa ambao itaendelea kubaki kule ili baada ya muda fulani ikishindwa maana ilikuwa tarehe 15 kabla ya mwaka kufungwa watoe taarifa kwa *Pay Master General*, sasa itaongezwa zaidi hata ya mwezi na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia inaleta sura ya kutumia vibaya hizi hela ndani ya *deposit*, vizuri *regulation* ikija hapa tuiunge mkono katika mazingira ambayo yatasaidia utimilifu wa nidhamu na maadili ya matumizi ya fedha za Serikali. Najua muda ni mdogo sana lakini niseme vizuri juu ya jambo la *DMDP II Dar es Salaam nimeliona* Mheshimiwa Waziri kalisemea vizuri ametenga dola za Kimarekani milioni 120. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naomba niunge mkono hotuba ya Waziri na bajeti ya Serikali ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Malizia sentensi ametenga milioni 120...

**MHE. ISSA J MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Dollar za Kimarekani kwa ajili ya Mto Msimbazi na kutengeneza *guidon* katika hili, lakini wajielekeze sasa kuna Mto Mbezi kuna shida sana Mheshimiwa Waziri katika bakaa utakayokuwa nayo najua *re-allocation* zinawezekana utusaidie na Mto Mbezi ndani ya Jimbo la Kimbamba nakushukuru sana kwa kuniongezea dakika moja hii ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa

Hassan Selemani Mtenga dakika tano, Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, ajiandae.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwanza kabisa nami nitoe shukrani nydingi sana kwa Serikali kwa kuweza kutoa fedha kwa kila jimbo kwa maana ya kupeleka fedha *TARURA* shilingi milioni 500 kwa kila jimbo hongereni sana na ninawashukuruni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mdogo nitataja mambo kwa juu juu tu, ninachokiomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye upande wa Kilimo kuna mpango wa kilimo *Agricultural Sector Development Programme*, mpango huu ni mzuri sana umeelezea namna ya kuongeza uzalishaji, imeongelea namna ya kuweza kufanya *processing* kwa mazao yetu ya kilimo, ni namna gani ya kuweza kufanya *packaging*, namna gani ya kuuza na kufanya masuala yote ya *environmental protection* haya mambo ni muhimu sana katika kuuza uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha habari tulizonazo sisi Wabunge na taarifa tulizonazo mpango huu hamuupi fedha, kama hamuupi fedha tutaendelea kupiga kelele siku zote hapa tunaongeza kilimo tuongeze kilimo, tuongeze uzalishaji kama *ASDP Phase II* hamuupi fedha tutakuwa tunaendelea kupiga *mark time*, naomba muwapelekee Wizara ya Kilimo fedha mpango huu uweze kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa utalii ongezeni matangazo, utalii wetu hautangazwi na kibaya zaidi, Waziri humu wa Utalii ulishawahidi kusema vivutio tulivyonavyo sisi ni vingi hatuna haja ya kutangaza, tangazeni tunataka biashara ya utalii iongezeke katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, China ina 1.7 bilioni *population* ya watu wa China, mkitangazia watu wa China mkaapeleka matangazo kwenye *CCTV* ya China 1.7 bilioni *population* wakisikia watu nusu ni milioni zaidi ya 800

watakuwa wamesikia habari hiyo, wakasikia na kuelewa nusu yao ni milioni 400 nusu yao wakaamua kuja kutembelea Tanzania ni milioni 200, nusu yao wakafanikiwa kufika Tanzania ni milioni 100, mkitangaza China tu tumeongeza idadi ya watalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mnasema hakuna haja ya kuongeza kufanya matangazo ya utalii, nawashukuru Simba mmekwenda mbele, mmekwenda kwenye mashindano makubwa mmeandika *visit* Tanzania hiyo ni hatua nzuri endeleeni kutoa matangazo ya utalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya elimu Mulugo ameongelea kuhusu mambo ya *PPP* nendeni kwenye *PPP*. Watoto wanaokwenda kumaliza darasa la saba ni wengi hatutaweza kuwa *accommodate* watoto kwenye madarasa tullyonayo ya Sekondari muwa-*Involve private sector* watusaidie na kazi ni nyepesi tu, kama mtoto anagharama tunamgharamia fedha inatoka *BOT* inakwenda kwenye shule za msingi na sekondari kuna gharama ya kila mtoto, gharama hiyo pelekeni kwenye shule ya Serikali na gharama hiyo hiyo wapeni watu binafsi wata-*accommodate* hawa watoto wawafundishe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa afya ndugu yangu hapa Mheshimiwa Shigongo kaongea vizuri kwenye *preventive measures, preventive medicine*, mama yangu hapa Mheshimiwa Dkt. Gwajima anakuja kuomba siku zote anaomba bajeti ya tiba, mishahara na kununua vifaa tiba *pprevention* haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Ofisi ya Waziri Mkuu isimamie suala la *prevention* kuna tatizo kubwa na *non-communicable diseases* limeongezeka sana bila utaratibu na uratibu wa Waziri Mkuu hatuwezi kufanikiwa wananchi wetu wanakwenda kupotea kwa sababu ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza, vyanzo vya vifo ni zaidi ya asilimia 36 tunapata vifo kutokana na *non-communicable diseases*. Ukiangalia ni magonjwa ya kisukari, magonjwa ya moyo na magonjwa ya kansa pamoja na ajali, tunaomba sana uratibu

wa Waziri Mkuu katika kuhakikisha tunawanusuru Watanzania kutokana na majanga ya magonjwa yasiyokuwa kuambukiza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho bandari yetu ninasoma mipango ya uchumi siku zote. Upande wa bandari yetu ni kubwa ina uwezo wa kupakia tani nyingi sana kushusha na kupakia, lakini hatuna ujenzi wa meli kubwa ya kupeleka bidhaa *abroad*, kupeleka nje ya Tanzania. Tumekalia kuzungumzia bandari ujenzi wa meli, meli ndogo ndogo Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa sijui Tanganyika, tuamue sasa kujenga na meli kubwa ya kupeleka bidhaa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada kusema hayo naunga mkono hoja ahsante sana kwa kunipa nafasi (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, Mheshimiwa Sylvia Sigula, ajiandae.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti. Kwanza nianze kwa kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini niwashukuru wasaidizi wake kwa ujumla nimshukuru Waziri wa Fedha na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie dakika tano hizi kwa mambo kidogo ya msingi, tunapotaka kuzungumza uchumi wa nchi yetu lazima tujikite kwenye viwanda, lakini tunapotaka kuzungumza uchumi wa nchi yetu lazima tujikite kwenye kilimo, lazima tuwe na watu amba wana nguvu za kutosha na watu wenye uelewa. Nini maana yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu walizungumza kuhusiana hapa na vijana amba wapo mtaani wamachinga. Genge hili la wafanyabiashara wadogo wadogo limekuwa ni kubwa mno, lakini bado sijaona kama Serikali ikiwa inajikita kuelekeza wapi iwapeleke hawa watu.

Lakini nataka nitoe mfano mmoja, vijana hawa wanapanga biashara barabarani, lakini vijana hawa tayari wanafamilia zao majumbani kwao. Imetokea siku kijana huyu ambaye yupo barabarani ameumwa, kwa hali ya kawaida hawezি kumchukua mkewe aende pale barabarani akapange zile nyanya au akapange zile nguo zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa jambo lingine kwenye wamachinga hao hao kwa hali na mazingira ambayo yapo, hatuwatengenezi hawa vijana kwenda kujitegemea. Kwa sababu, kwanza hawana *insurance* hawakopesheki kwenye mabenki vijana hawa. Sasa, rai yangu tunayo maeneo sisi ya kutosha, maeneo haya Serikali sasa ifike mahali itambue kwamba, inaweza ikwajengea maeneo ya kisasa. Kwanza, faida yake baada ya kuwajengea maeneo ya kisasa tutawenza kupata kodi, vilevile kwenye fursa sasa ya kuwajenga vijana wetu kutoka kwenye umachinga kwenye wafanyabiashara wakubwa. Nina imani kubwa sana hata Mheshimiwa Shigongo ametokea kwenye umachinga, lakini leo amekuwa mfanyabiashara mkubwa kwa sababu yeye aliwezeshwa. Ninaiomba Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie masuala ya bandari na uchumi. Masuala ya bandari na uchumi tunazo bandari katika nchi yetu, lakini napenda sana niizungumzie bandari ya Dar es Salaam, niizungumzie bandari ya Mtwara. Ukiangalia bandari ya Dar es Salaam kwa shughuli zinazofanyika kila siku, bandari ile inaonekana kwamba iko *tight*. Lakini kwa nini tusifike pahali tukapanua wigo tunayo bandari ya Mtwara tunayo bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tukienda pale Dar es Salaam tunakuta zaidi ya meli 20 au 30 ziko *hangarzinabiri* kupakua pale mzigo, lakini bado tunawapelekea kupata hasara kubwa jinsi meli inavyokaa kule *hangarzinabiri* iingie pale. Kuna *service charge* ambazo zinaingia kutohana na ghamama za watu ambao wamekodi meli zile. Rai yangu, tutumie bandari sasa ambazo tayari zina uwezo wa kubeba hizo meli kubwa ili tupate fursa zingine za kimaendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka nizungumze Mheshimiwa Naibu Waziri leo hii tunaishukuru sana Serikali yetu, kwa kweli mimi kwangu pale Mtwara haya mafuriko yaliyotokea hali ilikuwa ni mbaya sana. Nilivyoambibiwa ninapewa milioni 500, kwanza nilisali na nikasema eeeh Mama nakushukuru sana na Serikali yako. Haijawahi kutokea katika nchi yetu kwamba, Serikali imeamua kutoa *package* moja kwenye mzunguko mmoja kwa Majimbo yote. Kwamba leo mnipata milioni 500 kila Jimbo, kwa ajili ya matengenezo ya barabara zetu. Hongera sana Mama Samia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunazungumzia zao letu la korosho la Mtwara, tulikuwa tuna Mfuko wa *Export Levy*. Mfuko ule ambao Serikali iliuchukua lakini mpaka leo hii kila tunapozungumza Wabunge wa Mtwara kuzungumzia juu ya fedha zetu za *export levy* bado hatujapata muafaka na hatujaambibiwa nini kinaendelea. Rai yangu kwako Mfuko huu ndio ulikuwa unazalisha korosho kwa asilimia kubwa. Kwa sababu, ulikuwa una uwezo wa kuwenda kununua pembejeo, kwenda kuwasaidia wakulima na wakulima walikuwa hawana shida ya pembejeo kwa sababu tayari walikuwa wana mtaji wao, niiombe Serikali, nina imani Serikali yetu ni sikivu sana na inaweza kutusaidia, mfuko huu tunaomba urejeshwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niishukuru Serikali, niishukuru Serikali kwa mpango ambao umeletwa wa *NLG* tunakwenda kujenga viwanda Lindi. Viwanda hivi ambavyo vinakwenda kujengwa Lindi, mimi niiombe tena Serikali gesi inatoka Mtwara na kama gesi inatoka Mtwara, basi kwenye Wizara ya Uwekezaji muda sasa umefika wa kuiangalia Mtwara kama Mtwara, iwe nayo ni *zone* ya kimaendeleo. Kwa sababu haiwezekani kwamba gesi iko Mtwara, lakini Mtwara hatuwajibiki kwenye masuala mazima ya gesi. Nilikuwa naomba, nimuombe Waziri wa Uwekezaji kwamba, hili ni jukumu lake na ana mamlaka makubwa sana ya kuweza kutusaidia wawekezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasamu dakika Tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvia Sigula dakika tano, Mheshimiwa Nicodemus Maganga, ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii lakini nakuomba kidogo Mwenyezi Mungu akikujaalia basi uniongezee muda kidogo kwa sababu nina suala la kuisaidia Serikali yetu katika suala la mapato nakuomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kwa kuunga mkono hoja. Nazungumzia suala la uagizaji wa mafuta kwa pamoja. Hili suala la uagizaji wa mafuta kwa pamoja lilianza mwaka 2014 kwa ajili ya kupata zabuni ya kuagiza mafuta, kupata mzabuni atakayetuletea mafuta kwa pamoja. Shughuli hii imekwenda imefanyika kwa vizuri zaidi mpaka leo hii takribani mwaka wa saba, lakini yapo maeneo ambayo katika uagizaji huu wa mafuta tunakosa fursa ya kupata mapato katika eneo hili. Kwa nini nasema hivi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni kwamba, katika eneo hili kuna suala la kupata nafuu ya bei katika uagizaji wa mafuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo nchi marafiki. Tuna nchi kama Saudi Arabia, Iran, Kuwait, Abu Dhabi, Bahrain, Dubai pamoja na Oman. Nchi hizi zote zina Mabalozi katika nchi hii. Kwa nini tusitumie uagizaji sasa wa *tender* yetu iwe ya nchi kwa nchi badala ya mtu wa kati? Huyu mtu wa kati anaweka faida yake hapa ndani, hili liangaliwe sana katika mfumo huu wa uagizaji. Tunaiomba sana Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Nishati, wakae Makatibu Wakuu waanze kuangalia upya tathmini ya uagizaji wa pamoja je, nchi inapoteza kiasi gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivi ni kwamba, fedha hizi za uagizaji ni kwamba, bei zao za watu wa *OPEC* wanatoa *discount* ya asilimia 30 katika uagizaji. Kwa nini tunapoteza kiasi hiki cha asilimia 30 wakati sisi ni

maskini lakini wakati huo huo tuna shida na fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara zetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha katusikia Wabunge na Kamati ya Bajeti wametusikia Wabunge kwa kuweka shilingi mia moja. Hii shilingi mia moja iliyowekwa katika bei za mafuta, bei hizi za mafuta zinapanda na kushuka. Leo hii wananchi wanalamikia jambo hili kwa sababu bei iko juu, lakini mwaka jana mwezi wa Nane bei ilikuwa chini shilingi 1,500 mpaka shilingi 1,600 kwa lita. Hii *gap* isingeonekana sasa hivi inaonekana hapa kwa sababu hiyo, lakini fedha hii shilingi 100 ina faida kubwa sana katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haijawahi kutokea nchi hii toka imepata uhuru tumekuja kuweka jambo kubwa sana hili la kutengeneza barabara zetu katika Halmashauri zetu na vijiji. Kwa nini nasema, ni kwamba fedha za *toll road* ambazo zilikuwa zinakusanya zinakwenda kwenye Mfuko wa barabara, ilikuwa ni shilingi 263. Katika shilingi 263 *TARURA* ilikuwa inapewa asilimia 30 na asilimia 30 ilikuwa ni shilingi 78.90. Sasa leo hii shilingi 78.90 ukiongezea shilingi 100 tunapata shilingi 178.90. Ni sawa sawa na makusanyo kwa siku bilioni 2,148,000 pigeni makofi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa aliyoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Samia Suluhu kwa jambo hili tunakuambia Mheshimiwa Rais, tunakwenda kutengeneza barabara zetu kwa kiwango kikubwa haijawahi kutokea tokea uhuru. Hongereni sana, hengereni sana kwa bajeti nzuri na wananchi wanakwenda kuiona faida yake. Nini ambacho kinapungua *TARURA*, kinachokwenda kupungua *TARURA* ni kwamba tunawapelekea fedha nydingi zaidi ya bilioni 770 tunakuja kupata kwa ajili ya kazi ya barabara za *TARURA*. Sasa, ninachoomba ni kutengeneza *ring fence* ya hizi fedha. Mheshimiwa Waziri wa Fedha hizi fedha tunatakiwa tuzitengenezee *ring fence* zisitoke. Waheshimiwa Wabunge sijui mnanielewa ndani ya hili Bunge! Ni kwamba hizi fedha jamani lazima tutengeneze sheria kabla ya kuondoka hapa *kuzi-fence* hizi fedha zikawe na manufaa

kwetu, zitakwenda kutumika katika maeneo mengine.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kukuambia hii fedha tunazokwenda kuzitengeneza kule shilingi bilioni 78 ni fedha nyangi sana. Tunakwenda kupata bilioni 770 za TARURA lakini pamoja na hali hii ni kwamba hapa kuna fedha zingine ambazo zinapotea. Hizi fedha za EPShawa wanaweka *stamp* katika vinywaji, wanaweka *stamp* katika sigara, hawa wanachukua shilingi bilioni 94 wakati tunalo Shirika la Posta. Hili Shirika la Posta ndilo kazi hii ikafanye kama walivyoenda kufanya TBS. Posta ndiyo wenye kazi ya *stamp* katika nchi hii iweje aachiwe mtu binafsi akaweke *stamp* hizi, wakati Shirika la Posta linakwenda kafilisika na kufa? Tuliokoeni Shirika letu la Posta na hizi fedha bilioni 94 zikienda kule Posta, Posta itatoa gawio kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani ninachotaka kuwaambia hapa kuna fedha nyangine zinatumika Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Fedha zinazokwenda MaxMalipo tuna kitengo chetu sisi cha fedha za Serikali GPE. Kama GPE ni watu wa mfumo wa malipo kwa nini tunatumia MaxMalipo wanaondoka na mabilioni ya shilingi kila mwezi? Haiwezekani fedha Mheshimiwa Mwigulu. *(Makof)*

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja nimalize jambo la muhimu sana hapa. *(Makof)*

**NAIBU SPIKA:** Hapo nilishakupa mbili tayari umeongeza sekunde 30 malizia sentensi yako.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni hawa watu wa mfumo wa malipo ya Serikali. Tunao watoto tumesomesha wamesoma katika hivi vyuo, tunavyo vyuo vyetu sasa hivi tulivyonavyo katika nchi hii, kwa nini tuisiwaterumie tunakwenda kutumia MaxMalipo anaondoka na

fedha nyingi? Haya, kule Posta kuna wafanyakazi ambao hawana kazi sasa hivi na *stamp* hizo zinatengenezwa na hawa watu wa Posta ndio wanatoa kibali kumpa *EPS*, tunaruhusu jambo hili liende *EPS* wakati kuna Posta inakwenda kufilisika isifanye kazi hii?

Naiomba sana Serikali, jamani tuweni wazalendo kwenye nchi yetu tumsaidie Mama tuvuke. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tabasamu umeongea jambo la msingi sana hapo, hebu tusaidie hao *MaxMalipo* ni vijana pia wa Kitanzania au wao siyo Watanzania?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hawa *MaxMalipo* ni kampuni imekuja kutoka nje ikaja hapa, Watanzania wachache sana hapo. Mnabisha nini hayo maneno gani?

**NAIBU SPIKA:** Aah! ngoja Waheshimiwa Wabunge.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi ndiye ninaye mooliza Mheshimiwa Tabasam, vijana tumewasomesha wengi, nauliza hawa wa *MaxMalipo* ni Watanzania pia au siyo Watanzania?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hajui.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hata kama watakuwa ni Watanzania ndiyo ninachotaka kuwaambieni.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi!

**NAIBU SPIKA:** Ongea na mimi usiongee na mtu mwengine.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Hata kama watakuwa ni Watanzania lakini si tunalo Shirika la Posta hili Shirika la Posta si liko pale ifanye kazi?

**NAIBU SPIKA:** Sasa, ngoja nilikuwa nataka kuinyoosha vizuri hoja yako. Kwa sababu, umesema hivi tumesomesha watoto wa Kitanzania, sasa nikafikiri labda MaxMalipo siyo Watanzania. Ahsante sana, Mheshimiwa Tabasamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Sylvia Sigula, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Mheshimiwa Dkt. Leonard Madaraka Chamriho, ajiandae.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimwia Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa na mimi kuingia katika taarifa ya nchi hii ya kuchangia bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha Kaka yangu Mwigulu kwa hotuba nzuri sana yenye kuleta matumaini makubwa.

Naomba nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mama yetu mpendwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa anazozifanya na kuona umuhimu wa vijana na kufanya kikao kikubwa na vijana Jijini Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi zangu kwa Serikali kwa kuhusu suala zima hili la bodaboda, kwa kweli kitendo cha kutoa faini ya bodaboda kutoka shilingi 30,000 mpaka kufika shilingi 10,000 vijana tumebari jike sana. Lakini tutakuwa hatujafanya vizuri kama tutaishia tu kupunguza faini hii kutoka shilingi 30,000 kwenda shilingi 10,000 bado kwenye bodaboda changamoto ni kubwa tunafahamu wazi kwamba... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo. Tupunguze sauti, tupunguze sauti. Mheshimiwa Sylvia Sigula.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Tunafahamu kabisa wazi dhamira ya Serikali ni nzuri sana ya kuwatengenezea mazingira vijana ili waweweze kufanya kazi vizuri lakini bado changamoto ni kubwa. Mbali ya kuwa na hii shilingi 10,000 kama faini na tusipoitumia vizuri hii shilingi 10,000 kama faini tutatengeneza tatizo lingine. Nasema hivi kwa sababu moja, matatizo mengi ya bodaboda yanahusiana na suala zima la kuwa hawana leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu leo kijana wa bodaboda ili aweze kupata leseni lazima awe na shilingi 70,000. Kwa hiyo, matatizo mengi na faini nyingi hizi wanapigwa kwa sababu hawana leseni. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali na nimuombe Waziri pamoja na kupunguza hii faini basi tuangalie pia utaratibu huu wa leseni. Kama itampendeza Mheshimiwa Waziri angalau hata iwe shilingi 20,000 kwa mtu mmoja. Kwa sababu, leo haiwezekani kijana wa bodaboda atoe shilingi 70,000 pia na watu wenye magari watoe shilingi 70,000 haiwezekani Mheshimiwa Waziri. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri, Rais wetu mpendwa, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, wakati anaongea na vijana wa Taifa hili kupitia vijana wa Mwanza aliongea na vijana wa bodaboda na katika hotuba yake ya vijana wa bodaboda alisema anatamani kuona vijana wa Taifa hili wanamiliki bodaboda zao wenye. Nasema hivi kwa sababu, mwanzoni bodaboda ilifikiriwa kuwa ni ajira kwa watu ambao hawajasoma lakini naomba nikupe taarifa hii, leo hii asilimia kubwa ya vijana waliomaliza vyuo vikuu leo wanafanya kazi ya kuendesha bodaboda, yote hii ni kwa sababu kuna changamoto kubwa ya ajira, vijana wameamua kujipatia ajira kupitia bodaboda. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ili uingize bodaboda hapa nchini, kumekuwa na kodi nyingi na hizi kodi zinawanyima fursa vijana kumiliki bodaboda zao wenye ndio maana wanatumia bodaboda za watu na kuwaingizia utajiri watu wengine. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nikitaka kuingiza bodaboda kwanza lazima nilipe *import duty* ambayo ni 20 percent pia lazima nitalipa *excise duty* asilimia tano, nitalipa VAT asilimia 18. Ukiangalia tozo zote hizi anayezilipa mtu wa mwisho ni yule mnunuzi, kwa hiyo hii inawafanya vijana wengi wanashindwa kumiliki bodaboda zao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri, tunasema kabisa kwamba, maagizo ya viongozi wakubwa tunasema ni maagizo. Sasa Rais amesema natamani kuona vijana wanamiliki bodaboda zao wenyewe. Nilitarajia kuona mkakati wa Wizara ni namna gani vijana wataenda kumiliki bodaboda zao wenyewe. Hapa naomba nitoe ushauri kidogo tu kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na uhamasishaji wa vijana wengi kwamba wajunge kwenye vikundi na vikundi hivi tumekuwa tukivielekeza kwenye Halmashauri zetu bado tuna Mifuko ya uwezeshaji wa vijana na akina mama chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, niombe Mheshimiwa Waziri kwamba tunaweza tukaratibu vikundi hivi ama kupitia Halmashauri zao au kupitia usajili wao wa vikundi angalau tukaona tukapunguza hizi kodi hasa VAT.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe Mheshimiwa Waziri tunaweza tukaratibu vikundi hivi either kupitia halamashauri zao au kupitia usajili wao wa vikundi. Angalau tukaona tukapunguza hizi kodi hasa VAT. Tukisema kama tutatoa hii asilimia 18 tutakuwa tumewafanyia ahueni vijana wengi, na vijana wataweza kumiliki bodaboda zao wenyewe. Lakini leo ukisema vijana waende benki, tunajua zipo benki zinazotoa mikopo ya bodaboda, wanasema ni riba nafuu lakini Riba hizo sio nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni kijana, nafahamu benki si rafiki kwa vijana wengi kwa sababu hawana hati za nyumba, viwanja wala mitaji kwa hiyo wakifika watakosa vigezo hivyo. Kwa hiyo nilikuwa napenda sana kuishauri Wizara, kwamba eitherwawape mamlaka halmashauri zetu hizi, kama itawezekana waondolewe hii VATwatakapokuwa

wanaagiza bodaboda kwa vikundi ambavyo vimesajiliwa viro chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mchache lakini naunga mkono hoja, ahsante kwa kunipa fursa ya kuingia kwenye *record* ya Taifa hili kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Ahsante sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicodemus Maganga dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nashukuru. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu; kwanza kabisa kwa kuniona wa maana kwa kunipa nafasi ya leo adimu. Zimebaki siku tisa turudi majimboni. Kwa kuwa umenipa msaada mkubwa wa kuweza kuishauri Serikali ninaomba nijikite kuishauri Serikali maana muda hautoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kwa jinsi tulivyopanga hapa bajeti vizuri, kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba pamoja na Naibu Waziri kweli bajeti imekaa vizuri sana. Nimeisoma, ina *page 98* na nimesikiliza michango mingi ya Wabunge karibia yote inafanana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na mawazo tofauti. Kwanza nianze na suala la milioni 500 zilizotolewa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kila jimbo. Neno la Mungu linasema "Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa." Hii milioni 100 ni kilometra moja, milioni 500 ni kilometra moja. Nimeuliza kwenye makampuni yanayouza makatapila; kuna *caterpillar excavator* zinazouzwa na Wachina mpaka milioni 350. Mimi nilikuwa naona kwa mawazo yangu kwenye jimbo langu, kwa kuwa lina matatizo makubwa ya barabara; mngeturuhusu kila Mbunge tukatoa mawazo nikapata *excavator* la milioni 400 au 350 nikabaki na milioni 150 kwa ajili ya kuweka mafuta ningeweza kutengeneza barabara

zaidi ya kilometra 50 na kuendelea na *caterpillar* likabaki. Halafu hilo *caterpillar* si kwamba ni la kwangu, ikiwezekana liandikwe Mama Samia Hassan Suluhu, Rais wetu, ni mtu mwema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine naishauri Serikali, Waheshimiwa Wabunge watu wanataka mabadiliko wako *serious*. Na mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano Mungu amuweke mahali pema peponi; alitunadi kwa nguvu kubwa, na wengine tulishinda hatukuwa na sifa za kushinda; na kuna wengine walishindwa kwenye uchaguzi hawakuongoza katika kura za maoni. Lakini sasa hivi niseme tu nasikitika sana, kuona nchi tena inataka kurudi kwenye upigaji. Kuna watu ndani ya Serikali hawana mapenzi mema na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshauri Mheshimiwa Rais awe na maamuzi magumu kabisa katika hilo, wala asione huruma. Leo nimeshuhudia akiwaapisha Wakuu wa Wilaya na wengine kuwahamisha vituo, kama alivyofanya kwa Mawaziri. Lakini ukweli utabaki kuwa ukweli, watu wale ambao wanatuhumiwa na CAG pamoja na halmashauri zingine ambao wanaonekana kabisa wamekula pesa Serikali ichukue maamuzi magumu, na kwa kufanya hivyo itakuwa na sisi inatusaidia Wabunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa bodaboda Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba bodaboda takriban nchi nzima wanakupongeza sana. Lakini kuna sehemu ya wenye viti wa vijiji pamoja na vitongoji; Wabunge wengi wameongea na mimi naomba nikazie hapo. Hailiingii akilini mtu aliyekuwa ananifungulia mikutano yangu ya Kampeni hana hata shilingi elfu 10 kwenye Taifa ya Tanzania. Mtu huyu ambaye mimi nasimama kumuongoza Kikatiba, kwamba inatakiwa kuwasomea mapato na matumizi wananchi katika michango ya kawaida, hana hata senti 100. Ni suala la kujiuliza haraka haraka bila hata *degree*, unalijua kabisa suala hili si zuri. Kwa maana hiyo ukija hapa ninakuomba ujaribu kuwaingiza hawa watu ili na wao waweze kupata posho. Tunaposema Tanzania ina mali nydingi

angalau na wao *at least* kwa mwezi wawe na hata 100,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *MSD*. Wabunge wengi wanazungumzia suala la afya, na mimi nimekuwa msombofu sana hapa Bungeni. Nikiangalia takwimu za mwaka 2018 kwenye halmashauri yangu Mbogwe zilitengwa milioni 600 na zilikwenda; lakini cha ajabu nawauliza waliokuwa kwenye *system* hizi fedha hazikufika ilhali Serikali mpo na wasaidizi wa Rais mpo.

Mheshimiwa Naibu Spika lakini nimshukuru kaka yangu ambaye ni Naibu Waziri alifanya ziara kwenye hospitali zangu na akaona changamoto zilizopo. Nikuombe radhi sana Mheshimiwa Naibu Waziri juzi kwa kumuuliza swalii la kushtukiza Mheshimiwa Waziri Mkuu na ukaelekeza mamlaka kwamba watanijibu *TAMISEMI* lakini ninahitaji hilo zoezi kwa sababu wananchi wa Mbogwe bado wanaendelea kupata shida, akina mama wanakufa katika harakati za kujifungua, bodaboda wamekuwa wakipata ajali wanakosa vipimo kama X-ray pamoja na mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwaombe watu walio ndani ya Serikali, bajeti hii ni nzuri sana; lakini usiwe mchezo kama wa sarakasi, kama Kanumba na Ray. Tunaweza tukawa tumepitisha bajeti ya kila Idara, na uzuri nimechangia sekta nydingi sana; nimechangia kilimo, bajeti ya madini, na kila ukisoma jinsi Mawaziri mlivyo-*introduce*, kwamba mtafanya nini, iwe hiyo kweli. Lakini isiwe tu kwamba mmetukaririsha kwamba mtawasaidia kwa mfano wachimbaji wadogo halafu kusiwe na kitu, mtawasaidia wakulima kuwe hakuna kila kitu, tutaonekana watu wa ajabu sana. tukiangalia humu ndani tumo wa Chama kimoja; Mheshimiwa Marehemu aliliona hili baada ya Bunge la Mwaka 2015 kuwa na mivutano ambayo haikuwa na sababu; akaona achague watu wa kumsaidia ambao...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, hebu twende vizuri kidogo. Hili Bunge halina chama kimoja viro vyama vingine humu ndani.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kurekebisha tupo vyama vingi pamoja na mchanganyiko lakini wengi wetu tupo Chama Tawala. Kwa maana hiyo mimi nawashauri Waheshimiwa Wabunge, tusije tukamsaliti Marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho naomba nzungumzie kuhusu manung'uniko ya Waheshimiwa Wabunge. Maslahi ya Wabunge yapo kidogo sana; na mimi wakati bado sijaingia humu nilikuwa nafikiria kwamba kuna posho za kutosha. Nimeangalia mabunge mengine kama vile Afrika Kusini pamoja na Kenya na mabunge mengine wanalipa kwa dola. Tusiwaogope wananchi lazima tuwe wakweli tuwaambieni wananchi huku kwenye Ubunge hakuna kitu. Tumekuwa tukitukanwa kwenye mitandao; tumekuwa tukitukwanwa kwenye mitandao, na mimi hii kazi nillilomba kabisa kwa roho yangu moja; na mimi nitasema ukweli daima fitna kwangu mwiko. Fedha inayolipwa posho hapa haitoshi, mishahara haitoshi, mimi ninayeishi na wananchi hakuna kitu kinachoendelea.

Kwa hiyo hilo Serikali illangalie upya ili nasi tufananane na mabunge mengine, tusiwe wajanja wajanja. Ninaujua utapeli wa kila aina lakini sitaki niwe tapeli kwa wananchi, wananchi wajue kwamba wana Mbunge mwenye fedha kumbe hakuna kila kitu. (*Makof/vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo bado siku tisa, nirudi jimboni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa  
Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana mheshimiwa...

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:**...wananchi wanajua Mbunge wao anarudi na fedha. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:**...kengele imeshagonga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na mambo mengine nadhani umesikia kwamba ile milioni 500 matumizi yangeangalia kila Halmashauri na shida zao za barabara. Kwa hiyo huo ni uwekezaji mkubwa jamani, kununua greda siyo masihara.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia lengo la kutoa hamasa na elimu kwa Watanzania kulipa kodi, natoa ushauri kuwa Wizara ibuni mfumo wa mabalozi wa kulipa kodi bila shuruti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kuwa umma ukipata hamasa ya kulipa kodi itakuwa rahisi watu wengi kuona fahari kulipa kodi. Tunataka watu wapate hamasa ya kudai na kutoa risiti. Hii iwe ni kampeni ya nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi najitolea kuwa balozi wa kwanza. Ahsante.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba nianze mchango wangu, kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa muda wake mfupi wa kuongoza nchi yetu baada ya kifo cha Rais wetu wa Awamu ya Tano Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Mheshimiwa Samia ameonesha umahiri mkubwa wa kuliongoza Taifa letu, na hatimaye kutuletea bajeti hii ambayo inakwenda kujibu kero nydingi za wananchi wetu na kuboresha uchumi wa nchi yetu. Mimi binafsi nampongeza sana Mheshimiwa Rais na namwombea kwa Mwenyezi Mungu ampe afya njema na umri mrefu wenye manufaa kwake na kwa Taifa letu.

Lakini pia nimpongezi Mheshimiwa Waziri na watendaji wote katika Wizara hii kwa kuja na bajeti nzuri yenye kuzingatia maoni mengi ya Waheshimiwa Wabunge

walipochangia Wizara mbalimbali za kisekta. Hii inaendelea kuthibitika kuwa Serikali yetu inayoundwa na CCM ni Serikali sikivu, inayozingatia maoni ya wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo yote sasa naishauri Serikali kuendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo hapo juu naomba sasa kuishauri Serikali kuzingatia yafuatayo ili kuboresha utekelezaji wa bajeti hii:-

Kwanza katika Wizara ya Ujenzi, iko miradi ya aina kuu mbili katika ujenzi wa barabara zetu hapa nchini; miradi ya upembusi na usanifu wa kina wa barabara zetu, miradi imekuwa ikiigharimu Serikali fedha nyngi na miradi ya ujenzi wa barabara zillizokamilika kwenye hatua hilo hapo juu.

Katika hatua hii naishauri Serikali kupunguza au kuacha kuendelea na miradi ya upembusi yakinifu hadi pale barabara zote zillizokwishakamilika katika upembusi na usanifu wa kina zitakapofikiwa hatua za ujenzi. Nayasema haya kwa kuwa tunazo barabara nyngi zilishafanyiwa upembusi na usanifu wa kina kwa muda mrefu. Kwa kuwa zinakaa muda mrefu bila kujengwa, na pale tunapokwenda kuzijenga tunalazimika kuzirudia upembusi upya jambo ambalo linaongeza gharama za ujenzi bila sababu, kwa nini tuendelee kufanya upembusi kwenye barabara mpya kabla ya ujenzi wa zile zillizokamilika?

Pili ni kuhusu uhifadhi wa wanyama pori; hapa naomba kuishauri Serikali kuja na mpango mkakati wa kuimarisha hifadhi zinazomilikiwa na jamii zijulikanazo kama WMAs. Hifadhi hizi zinamilikiwa na jamii, lakini Serikali isipokuja na mkakati maalum zinakwenda kufa. Kuimarika kwa hifadhi hizi kungepunguza sana manung'uniko katika jamii hasa zile Halmashuri zinazopakana na hifadhi zetu za Kitaifa. Kuimarika kwa WMAs wananchi wetu wanaenda kuona manufaa ya moja kwa moja uwepo wa wanyama hawa, pale ambapo

mfano *WMAs* watajenga darasa au choo na miradi mingine kama hiyo ambayo inaenda kugusa maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, *WMAs* wasaidiwe kutafuta wawekezaji kwenye vitalu vyao na kuvifanyia matangazo ili kuvutia wawekezaji. Sambamba na hilo niiombe sana Serikali kuharakisha malipo yao ya hizi jumuiya yanatolewa kwa wakati. Hapa napo napendekeza malipo hayo yaende moja kwa moja kwenye jumuiya badala ya kupitia *TAWA* ambako zinachelewa sana kuwafikia walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena *WMAs* zikifanya vizuri zinasaidia sana kupunguza machungu kwa jamii yanayotokana na athari za wanyamapori. Lakini pia ni ukweli usiopingika kuwa uwezo wa kuzitangaza hifadhi hizi zinazomilikiwa na *WMAs* wakiachiwa wenyewe ni mdogo sana.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wa kuchangia kwa kuzungumza katika Bunge lako Tukufu kupitia maandishi narejea na kuendelea kuchangia Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali msisitizo wangu ni juu ya njia na shughuli zinazoweza kutuongezea mapato ya kutekeleza bajeti yetu na kuendeleza Taifa letu kwa ujumla. Fursa ya kuongeza mapato kwa kuuza bidhaa nje zilizoagizwa kutoka nje na kuongezwa thamani hapa au kuuzwa nchi nyingine kama zilivyo maarufu kama *re-export*. Bidhaa ya kwanza ni mafuta jamii ya petroli. Katika historia ya biashara ya mafuta kuna wakati makampuni, watu binafsi na idara za Serikali toka nchi jirani walikuwa wanakuja Dar es Salaam kununua mafuta na kuyasafirisha kwa njia ya malori au na mabehewa ya treni. Matumizi ya mfumo huu ni kuwa kampuni ya Tanzania inapo *re-export* Taifa linafaidika na lile ongezeko katika bei (*mark up*) ambayo huongeza faida ya kampuni husika na hatimaye kutozwa kodi na tozo nyinginezo kwa manufaa ya Taifa. Lakini uwepo wa utaratibu huu ulioratibiwa vizuri huwezesha Taifa

kuwa na hifadhi kubwa ya mafuta bila kuilipia ambayo inapelekea kuwa na mafuta mengi ya kimkakati (*strategic stock*).

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu utawavutia na kuwafunga wateja wa nchi lengwa kwa kuwa na uhakika wa kupata mafuta kwa bei inayojulikana toka kwao, lakini pia uwepo wa *volume* kubwa ya mafuta toka hapa kwenda nchi jirani itaongeza matumizi ya mafuta (*fuel for truck use on safari*) yaliyolipiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nifafanue kidogo dhana ya mafuta yaliyolipiwa, mafuta yanayotumiwa na malori yanayokwenda nje ya nchi (*transit*) au *re-export* shughuli zake huleta pesa za kigeni ambazo huchangia kununua mafuta mengine. Kwa mafuta yanayotumika nchini wingi au ongezeko lake linaweza kuwa na tija pale inapopelekea kutafuta fedha za kigeni kuagiza mafuta mengine. Ikumbukwe kuwa tuna mahitaji ya kununua mafuta kama bidhaa muhimu na mafuta jamii ya petroli ndiyo bidhaa ya kwanza kuchukua fedha zetu adimu za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jinsi ya kuchota fursa hii ni kwanza kujipanga kuusimamia ili kuelpuka watu wasio waadilifu kuitumia vibaya kwa manufaa yao/kuifisadi. Hili zaidi ni jukumu la *TRA* na idara zake wakisaidiwa na vyombo na taasisi nyingine za dola. Utaratibu huu ulikuwepo ila kwa kushindwa kuusimamia basi zikatungwa sheria zilizoua fursa hii. Sasa tunao vijana wengi wenye elimu wanaweza kupewa ujuzi na stadi za kuusimamia sekta hii na kwa faida ya matumizi ya teknolojia tukachangamsha sekta hii na kupata mapato ya Serikali .

Pili ni kuruhusu hifadhi ya mafuta ya forodha iliyozuiliwa (*bonded customs warehouses/terminals*). Kama nilivyodokeza mafuta yaliyoko katika hifadhi za namna hii yanahamasisha kampuni husika kuagiza mafuta mengi kwani hawawajibiki kulipa kodi na tozo mara moja, lakini kwa upande wa nchi *stock* hizi ni kinga ya kiusalama kwani nchi inakuwa na haki ya kwanza kuyatumia inapotokea tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa nyingine inayofanana karibu na hiyo ni hifadhi ya mafuta inayoelea (*floating stock*). Tanzania tunayo fursa ya kufanya biashara hii kwa kuruhusu sekta binafsi kujenga matanki makubwa ya kuhifadhi mafuta nchini kwa lengo la kuuza mafuta hayo popote duniani. Kimsingi mafuta yanayotunzwa katika hifadhi hizi huwa yananyumbulika kufuata bei za soko la dunia. Faida kwa nchi ni kodi na tozo kwa uwekezaji, huduma za bandari na haki ya kuwa mteja wa kwanza. Biashara ya namna hii iliwahi kufanyika kwenye maji ya bahari ya Tanzania kwa kutumia mtindo wa meli mama na mtoto (*mother daughter vessels*). Chini ya utaratibu huo na kutokana na ukosefu wa matenki makubwa na sheria” za nchi yetu, meli kubwa zenye ujazo wa kati ya tani 150,000 mpaka 200,000 hutinga nanga kwenye maji ya Tanzania ambapo hufaulisha mafuta kwenye meli za ujazo wa tani 40,000. Shughuli hii kulingana mwenendo wa bahari ya Hindi inaweza kufanyika Tanzania usawa wa Tanga-Bagamoyo na Zanzibar kwa usawa wote wa chini ya Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafuta ipo fursa ya kuboresha mfumo wa bei elekezi ili kuchota faida kubwa itokanayo na kushuka na kupanda kwa bei za mafuta kwenye soko la dunia (*backwardation - contango*). Busara yake ni rahisi kuelezeka, bei katika soko la dunia inaposhuka na hapa nchini bei ikashuka kwenye vituo vya mafuta nauli au bei ya bidhaa huwa haishuki. Hii ina maana mlaji wa mwisho hafaaidiki mara nyingi na anguko kubwa la bei ya mafuta. Lakini mafuta yanapoanza kupanda na bei elekezi ikaonesha bei ya mafuta kuwa juu kwa kutegemea huo mzigo mpya walaji hafaaidiki endapo kuna *stock* kubwa ya zamani. Lakini soko la Tanzania kulingana na sheria na taratibu zetu hatuna mipango na mikakati ya kuchota na kuhifadhi mafuta yenye bei naifuu katika mazingira ambayo wazi inaonesha kuwa muda si mrefu bei itapanda. Yote haya yanaweza kufanyika kirahisi kwa kuweka sheria na mazingirra ya kuvutia uwekezani wa namna hiyo kuitia sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie fursa nyingine ya *re-export* kwa bidhaa zingine zisizo mafuta jamii ya petroli.

Kwanza nieleze kuwa viwanda vya mafuta ya kupikia na ngano vilivyoko nchi za jirani ikiwemo Rwanda, Burundi na hata Uganda vilijengwa huko baada ya wawekezaji waliokuwa wakitumia viwanda vilivyoko Tanzania kushindwa kuhudumia masoko hayo kutoka kwetu. Yote hayo yalitokana na sheria na usimamizi usiowezesha kufanya biashara ya aina hiyo toka Tanzania. Tathimini ya biashara hii itakuonesha kuwa kuna fursa kubwa sana tukijenga sekta hii kwa lengo la kutengeneza ajira, kupata kodi na kuchangamsha uchumi. Kuna wakati *re-export* kwenda nchi jirani ilifikia dola milioni 840 kwa mwaka lakini kati ya mwaka 2015 mpaka 2020 kiasi cha juu ni dola milioni 340.7 na kiwango cha chini ni dola milioni 143.16 mwaka 2017. Ni imani yangu kuwa kwa kuweka mazingira mazuri *re-export value* inaweza kufikia dola biillioni 1.5 kwa mwaka katika miaka mitatu ijayo. Hii ni sekta ya *re-export*, si mauzo ya bidhaa nje (*export*).

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli nyingine inayoendana na *re-export* na ambayo inaweza kuchangamsha uchumi kwa kutengeneza ajira na kupanua wigo wa walipa kodi ni vituo vya biashara hapa nchini, kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na zile zinazotoka nje ya nchi, kwa mfano, soko la Kariakoo kabla ya kuanguka kutokana na sheria na udhibiti. Ni kweli yalikuwepo mapungufu katika biashara hiyo ambayo pamoja na kuzalisha ajira kwa kiasi kikubwa kulikuwepo mianya ya kukwepa kodi, bidhaa hafifu na bidhaa za bei ndogo zinazoathiri viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa ni kuwa mapungufu yanawenza kurekebishwa na faida za kuwa na masoko kama hayo zikaweza kuchotwa kwa manufaa ya Taifa. Mfano wa wazi ni Kariakoo ya Kampala, Uganda iliyoanzishwa baada ya kudorora kwa Kariakoo mwenye jina. Wafanyabiashara kutoka Malawi, Congo, Zambia na kwetu Tanzania wanunua bidhaa Kariakoo Kampala. Hapa kuna hoja tatu, ajira, kodi na kuchangamsha jamii. Ajira inatangulia kodi lakini mwenye ajira analipa kodi iwe moja kwa moja au *indirect*. Eneo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni uhamasishaji wa mauzo nje (*export*). Kama nilivyoeleza kwenye mchango wangu kwa kuzungumza Tanzania mwaka 2019 tuliiza nje bidhaa zenye thamani ya bilioni 2.9 pesa ya Marekani na 2/3 ikiwa ni dhababu lakini fursa ya mauzo nje (*potential export*) yetu ni bilioni 2.37 pesa ya Marekani bila kuhesabu dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa ni fursa zilizowazi ambazo tunaweza kuzitumia na kuongeza mauzo nje. Nieleze wazi hapa kuwa kama Taifa lazima tutembee na lengo letu la kuuza bidhaa nje kwani pamoja na kuleta pesa za kigeni linatuhakikisha soko la bidhaa zetu na kuleta ustahimilifu wa sekta zetu za uzalishaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bidhaa/mazao 19 niliyoyarejea sikuona nyama au ng'ombe hai, maziwa, mawese, maharage aina ya soya kwa kutaja baadhi. Uchambuzi wa haraka ni labda watakwimu walichukua bidhaa ambazo zina fursa zaidi ya dola milioni 20.8 kwa mwaka. Hoja yangu ni kuwa iweje nchi yenye fursa ya kufuga tushindwe kuzalisha nyama bora na maziwa kutosheleza soko la ndani na kuuza nje? Iweje Uganda na Botswana wafanye vizuri kwenye sekta hizi kuzidi nchi yetu yenye ardhi na uwanda mzuri wa kufuga ng'ombe. Hili ni eneo muhimu la kuwekeza kwani mbali ya fursa ya kuuza nje sekta hizi zinasaidia kujenga uchumi jumuishi jambo muhimu katika Taifa lenye amani na mshikamano. Pia kwa mazao ya shamba kama mawese au mafuta ya mawese ambayo kimsingi yana soko kubwa DR-Congo na tunakuwa na faida ya kuwa karibu na soko kwani yanalinwa mikoa ya Magharibi, ni muhimu tuongeze jitihada za kuhamasisha sekta hii kuliko tunavyofanya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu hapa ni kualika sekta binafsi kushirikiana na wananchi kwanza kwa kuhakikisha wanalima mashamba makubwa kwa uwiano wa familia, lakini mwekezaji anayeweza kujenga kiwanda kikubwa kitakachofanyakazi kwa tija kubwa. China wametupa nafasi ya kuza maharage aina ya soya tani milioni 42 kwa mwaka

kwa bei ya shilingi 3,000 kwa kilo ni takribani mauzo ya shilingi triliuni 126. Kiasi ni kikubwa sana hata ingekuwa ni mauzo ya miaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kuwa kwanza Serikali ihakikishe mkataba huu unalindwa, pili lazima iwepo mipango na mikakati ya kuhudumia soko kwa kukidhi viwango vya soko kwa faida kwa wazalishaji. Tatu, ni kuhakikisha wananchi kwa matabaka yote wanashirikishwa hasa kwa kusaidiwa kuingia kwenye myororo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mazao ya soya ni vizuri tukaelewa kwa ujazo na uzito wake. Tanzania kwa ujumla wake tunazalisha vyakula vya aina zote tani million 19, soya tu ni tani milioni 42; huu ndio ukubwa wa jukumu tulilonalo. Hii ni fursa kubwa na nzito na inahitaji nguvu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kuwa kwa kuza nje (*export & re-export*) kwa kiasi kikubwa tutapata fedha nyingi za kigeni lakini kujenga uhakika wa soko hali itakayochocha sekta za uzalishaji hapa nchini kuzalisha zaidi. Mchakato wa uzalishaji utasaidia kutengeneza ajira, kuzalisha bidhaa, kusaidia kukusanya mapato ya Serikali kwa maendeleo na kuchangamsha uchumi. Pamoja na bajeti hii kama ilivyowasilishwa, tunaweza kufikia mapendekezo haya kwa kutengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji tukirekebisha sheria na taratibu za utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwa kushauri juu ya usimamiaji wa zuio la sukari la asilimia 15 kwenye sukari ya viwandani na hiyo *VAT refund*. Nakubaliana na Serikali kwa kukubali kuondoa hiyo 15% kwenye sukari ya viwandani lakini lazima Serikali iendelee na taratibu za kusimamia sukari hiyo. Hupo uwezekano wa sukari ya mezani kuingizwa na kuuzwa kama sukari ya viwandani. Sukari aina hii iratibiwe kwa kuwa na *customs bonded rooms* kwenye viwanda vikubwa na kwa wawekezaji wadogo iwepo *bonded warehouse* ya ujumla.

Naomba na kushauri wazo la kurudisha kiwango hiki lisifikiriwe kwani madhara yake kwenye sekta ya viwanda hatutakaa tuyamalize makali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Serikali hajatamka juu ya kikwazo kikubwa cha uendeshaji wa viwanda na uwekezaji kwa ujumla. *TRA* wawe wazi kubainisha stahili ya *PMG - VAT revenue* na stahiki ya *CG TRA - VAT expenditure*. Kama awali tunapopokea *VAT* au kuratibu *VAT* ni vema tuje yapi ni mapato ya Serikali na kiasi gani kitarejeshwa kwa mfanyakishara. Vipo viwanda vya Tanzania vimeshindwa kuzalisha na kuuza masoko ya nje kutokana na mapungufu yetu katika kusimamia *VAT refund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali. Kwa dhati ya moyo wangu nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu kipenzi Mama Samia Suluhu Hassan, nampongeza Rais kwa juhudi zake anazozichukua siku hadi siku pamoja na kutupa kipaumbele hasa sisi wakina mama wa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza tena Mama Samia Suluhu Hassan kwa kumuamini na kumteua Dkt.r Philip Mpango kuwa msaidizi wake Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ninampongeza Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge hili kwa kutuendesha vizuri katika shughuli zetu za Bunge.

Nampongeza pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa umahiri wake wa utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku, namuombea kwa Mwenyezi Mungu aangalie uzima wa afya yake na amani katika maisha yake ya kila siku pia nampongeza Waziri wa Fedha – Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchomba na Naibu wake *Engineer Masauni* pamoja na Katibu Mkuu na viongozi wote waandamizi wa Wizara hii ya Fedha na Mipango na pia naipongeza Kamati

ya Kudumu ya Bunge kwa kushirikiana na Wizara kwa kutuleta bajeti ambayo imekidhi kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii imegusa maslahi mapana ya Taifa letu, naamini itawanufaisha Watanzania kwa ujumla, sina budi ya kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake kijumla, lakini naomba kuchangia kwa ufupi kuhusu upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijiji bado hairidhishi. Maji hayana mbadala, maji ni uhai, maji ni maisha kwa viumbe hai vyote, bado viro vijiji ambavyo havina kisima hata kimoja cha maji safi na salama na badala yake hutumia maji ya mapalio, maji ya madimbwi, maji ya mito wanayochangia na Wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina vyanzo vingi vya maji mfano Mkoa wa Morogoro kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama, lakini vyanzo vingi vya maji vimeanzia Mkoa wa Morogoro na kutumika katika baadhi ya mikoa mingine na si kuwasaidia wakazi waliopo vijiji ndani ya Mkoa wa Morogoro; kwa mfano Bwawa la Kidunda liliopo Wilaya ya Morogoro Vijiji nalo lingekuwa msaada mkubwa kwa wanakijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu iweke nguvu katika sekta ya maji ili tuweze kumtua ndoo ya maji mama kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa ufupi niongezee katika upande wa elimu; kuna changamoto kubwa katika upande wa madarasa na madawati, madarasa mengi yamekuwa chakavu na mlundikano wa watoto katika darasa moja linakuwa na wanafunzi zaidi ya 100 na Serikali imeona muitikio mkubwa wa wanafunzi kusoma kutokana na elimu bila malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu naomba kuwe na mkakati maalum kwa watoto wanaohitimu darasa la saba kwenda kidato cha kwanza kuhakikisha wanakuwa na madarasa na si kuanza ujenzi wa madarasa kipindi watoto wanataka kuingia shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja Ahsante.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote kwa hotuba ya bajeti iliyoandaliwa vizuri. Nina imani kubwa juu ya kuwezesha utekelezaji mzuri wa bajeti hii, kwani ninatambua uwezo mkubwa, uthubutu, unyenyekevu na uchapa kazi walionao Waziri na Naibu Waziri. Pia naipongeza sana Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya. Bajeti hii ni nzuri, imegusa maeneo mengi ya kuleta maendeleo na imelenga kutatua changamoto nyingi za wananchi. Ni bajeti ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha, naomba kupendekeza yafuatayo; ulipwaji madeni ya wazabuni ya mwaka 2011 hadi 2016. Kuna wazabuni waliota huduma na vyakula kwenye shule za sekondari kati ya mwaka 2011 hadi kati ya 2016, hawakulipwa. Madeni yalihakikiwa, Hazina ikasema italipa. Wazabuni waliokwenda Hazina baadhi walilipwa. Baadae Serikali ilirudisha madeni haya kwenye Halmashauri. Halmashauri hazikuweza kuyalipa sababu vyanzo vikubwa vya mapato vilijamishiwa *TRA*. Hawa wazabuni wamesubiri, wengine sasa ni miaka kumi wanaidai Serikali, huduma walitoa, lakini Serikali haijawalipa. Madeni yamelala kwenye Halmashauri mbalimbali nchini. Wazabuni hawa wameumia, wamefilisiwa na benki wamefililisika. Naomba na kuiishauri Serikali kuu ilipe madeni haya. Miaka kumi jamani, waonee huruma. Waziri ukija kuhitimisha naomba jibu ni lini watalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoani Kagera wakulima, wastaafuli, wajasiriamali, viikundi vya wanawake na *SACCOS* mbalimbali walikuwa wameweka fedha zao katika Benki ya Wakulima ya *KFCB*. Benki hii ilifungwa na Benki Kuu mwaka 2018. Watu waliokuwa wameweka fedha zao humo, hawana makosa lakini wanateseka sababu fedha hizi zilifungiwa humo. Mheshimiwa Waziri ni lini watu hawa watarudishiwa fedha zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuomba upendeleo maalum (*preferential treatment*) wa kisera, kisheria, kikanuni, kiutaratibu, kikodi ili kuinua uchumi wa Mkao wa Kagera. Mkao wa Kagera uko takribani kilometra 1400 hadi 1500 kutoka Bandari ya Dar es Salaam. Mkao umezungukwa na nchi nyingi kama Rwanda, Burundi, Uganda, na Sudan Kusini na DRC zinafikika kirahisi kutoka Kagera. Nchi hizi zingeweza kuwa soko zuri sana kwa Mkao wa Kagera, lakini kwa sababu wao wana sera nzuri zaidi za kuvutia wawekezaji na biashara, basi kwao wanafanya vizuri kuliko sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya bajeti hii inaonesha kuwa Mkao wa Kagera una wawekezaji kwenye viwanda wachache sana. Gharama kubwa za usafiri zinachangia mkoa kukosa wawekezaji kwenye viwanda na biashara, inapunguza uwezo wa ushindani kwenye masoko. Gharama kubwa za usafirishaji wa wataalam, kufuatilia vibali mbalimbali na usafirishaji wa wataalam na usafirishaji wa bidhaa zilizozalishwa ili zifiki masoko makubwa yaliyo Dar es Salaam, gharama hizi ni kubwa, haziwavutii wawekezaji kwani zinaongeza gharama za uzalishaji. Mfano mfuko mmoja wa simenti unaununa kati ya shilingi 13,000 hadi 14,000 Dar es Salaam, ikifika Kagera mfuko huo huo unauzwa kati ya shilingi 22,000 na 25,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zilizotuzunguka zina sera na utaratibu mzuri zaidi unaowavutia wawekezaji. Nchi jirani zimetambua gharama za usafirishaji kama *Non-Tariff Barrier (NTBs)*, hivyo wameweka utaratibu wawekezaji wanawekewa viwango vidogo vya kikodi. Matokeo yake sasa tunashuhudia wawekezaji wengine wakihama kutoka Tanzania kuhamia nchi jirani. Hata wafanyabiashara Watanzania, wengine wamevutiwa na kuhamishia mitaji yao nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mipakani mfano Mtukula, Rusumo na kadhaika, biashara zinachangamka upande wa Uganda na Rwanda, upande wa Tanzania biashara zinadorora. Sera, sheria na kanuni zao zimerahisishwa sana kiasi wafanyabiashara wanashawishika kufungua

biashara nyingi kwa kasi Uganda kuliko Tanzania. Hata baadhi ya Watanzania wanapeleka biashara zao nchi jirani mfano pale Mtukula.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2019, Mkoa wa Kagera uliwasilisha ombi Serikalini wakiomba mkoa upewe Upendeleo maalum, wawekezaji Mkoa wa Kagera wapewe unafuu wa kikodi ili kufidia gharama kubwa za uzalishaji na uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitolewa upendeleo huu wa kisera, kisheria, kikanuni na kikodi mkoa utashindana sawa na nchi jirani, milango ya uwekezaji na biashara itakuwa imefunguliwa, wawekezaji wataongezeka, uzalishaji kwenye viwanda utaongezeka, biashara za mpakani upande wa Tanzania zitaongezeka, mzunguko wa uchumi katika Mkoa wa Kagera utaongezeka na mapato ya Serikali yataongezeka.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ombi la kuupatia Mkoa wa Kagera upendeleo maalum (*preferential*) liliiletwa Serikalini tangu mwaka 2019 ili kuchochaea uwekezaji wa viwanda na biashara Mkoani Kagera litatekelezwa lini? Naomba jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mchango wa maandishi kama ifuatavyo; kwanza sekta ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na utalii; kwa miaka mingi sekta ya utalii imekuwa na mchango wa takribani 25% katika kuingiza fedha za kigeni, hata hivyo baada ya shida ya *Covid-19* sekta hii imetetereka kwa hali ya juu sana, katika ajira sekta hii kwa ujumla inaajiri takribani Watanzania milioni nne. Baadhi ya nchi na hata mashirika makubwa ya fedha duniani yamekuwa yakitoa *stimulus package* ili walau kukabiliana na janga la *Covid-19*. Sisi Taifa letu bado haliwezi kubeba mzigo wa kuwa na *stimulus package* na ndio maana

hata *TANAPA* imebidi kuisaidia. Kwa sababu hiyo nashauri tusiongeze tozo katika sekta ya utalii, tuache zilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wanyama pori/*TAWA*; naunga mkono suala la kugawa vitalu kwa njia ya mnada, hata hivyo ili tupate fedha lazima tuuze kwa bei rafiki kuliko ilivyo sasa ambapo vitalu vingi vinakosa wapangaji na tunakosa sio fedha tu lakini tunaviweka vitalu katika uhatari wa kukosa kuhifadhiwa kwa sababu masharti ya anayepewa kitalu ni pamoja na uhifadhi. Wenzetu Zimbabwe wana maeneo 40 tu lakini kwa mwaka wanapata *around USD 130 million*, mbali ya kupata fedha kwa kukodisha vitalu kuna faida mbalimbali kama vile ajira kwa *rangers, fuel levy* kutokana na magari yanayotumika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, kwanza Serikali ijiridhishe kuhusu vitalu itabaini kuwa tunakosa fedha kwa sababu ya bei ya kuanzia, hivyo Serikali ipange bei za kuanzia ambazo zitavutia wateja, bei za *USD 80,000* hazijaweza kutusaidia, tushuke walau hata nusu, haina maana tuna vitalu lakini hatuvikodishi, ni kama una nyumba unataka kuipangisha kwa shilingi laki moja kwa mwezi, hupati wapangaji kwa miaka mitatu, wakati ungepangisha kwa nusu ya bei, ungeweza kupata mapato lakini pia nyumba ikikaa bila kuishi mtu inachakaa. Nimetoa mfano wa kawaida kabisa wa *ki-layman* ili walau nieleweke, ninaamini vitalu vya uwindaji vinaweza kutuongezea mapato ya kutosha hata kuvuka bilioni 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni misitu/*TFS*; asilimia 60 ya ardhi ya Mafinga/Mufindi ni misitu, tuna msitu mkubwa wa *Sao Hill*, ni msitu mkubwa Afrika Mashariki na Kati. Hata hivyo wingi wa tozo umeendelea kupunguza wavunaji katika msitu na hivyo kukosresha Serikali mapato, wavunaji wana *opt* kwenda kuvuna miti ya wananchi ambayo haitoshelezi, nashauri *VAT* na *LMDA* ziondoshwe, duniani kote hakuna anayetoza *VAT* kwenye mti. Kwa mfano bei ya soko kwa *cubic meter* moja ni shilingi 320,000 kwa hiyo mvunaji ambaye anaiza 320,000 anaingia ghamama zifuatazo; ili upate *cubic meter* moja ya mbao unahitaji miti ya ujazo wa *cubic meter*

tatu ambapo ni  $3 \times 64,940 = 194,820$  hii *royalty*; kuna VAT 18% shilingi 35,068; kuna *cess* 5% = shilingi 9,741; kuna *LMDA*  $17,000 \times 3 =$  shilingi 51,000 kwa sababu kama nilivyosema ili kupata *cubic meter* moja ya mbao unahitaji *cubic meter* tatu za miti na kuna *TPyaani transit passya* miti  $7000 \times 3 =$  shilingi 21,000. Kwa hiyo jumla ya tozo ni shilingi 311,629. Ukichukua 320,000 ukatoa 311,629 mvunaji anabakiwa na shilingi 8,371. Hapa sijataja gharama nyngine za uendeshaji kama mafuta, vibarua wa kusogea magogo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hii tozo tu ni 97% ndio maana wavunaji wanakimbia kuvuna katika msitu wa Serikali tunakosa fedha lakini pia ni *double taxation* kutoza VAT kwenye mtu, halafu tena kwenye mbao, kadhalika *cess* inatozwa mara mbili, sio tu ni uonevu lakini pia ni kinyume cha sheria lakini pia hotuba inasema Serikali haitaki mapato ya dhuluma, haya pia ni ya dhuluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tozo kwenye mafuta ya kula; ndugu zangu lazima tuwe *honest*, hatuwezi kulinda ambacho hakipo, mwaka wa nne sasa hatujaanza kuzalisha mafuta kutohana na mawese, lakini pia jitihada za kulima alizeti na ufuta hazijaimarika ipasavyo, kuongeza tozo ni kumtesa mwananchi, bei ya mafuta ya imekuwa ikiongezeka mwaka hata mwaka kwa zaidi ya 100%. Hivyo nashauri sana tuitazame hii tozo, tusilinde ambacho hakipo, Wizara ya Kilimo iongoze mbio kuhakikisha suala aliloanzisha Mheshimiwa Waziri Mkuu katika michikichi na alizeti ili tujikwamue kwa vitendo suala la mafuta ya kula, tusilinde ambacho hakipo.

Kuhusu uchukuzi/bandari/*TAZARA*; nashauri, kwa kuwa bandari ni chanzo cha mapato, yapo maeneo tuyaimarishe ili kupunguza muda wa kusafirisha mizigo; *TAZARA* iimarishe ili ifikishe mizigo mpaka Makambako na Mbeya ambapo nchi jirani watakuja kuchukua *cargo* zao Makambako au Mbeya, *tuta-fast track* uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Tunduma malori yanatumia mpaka wiki kuvuka, suala hili linapunguza ufanisi, ndio maana Bandari kama Beira zinakuwa washindani wetu

wakati hawastahili, hivyo maeneo yanayotupa mapato tuyalee, tuweke mageti hata Mbozi, suala kwamba *transit cargo* itarudi nchini, sio sawa labda kama hatuna nia njema kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *fuel levy/vinasaba*; kwa muda wa miezi karibu miwili *TBS* wanaifanya kazi hii, jambo hili ni jambo jema kuvijengea uwezo vyombo vyetu, hata hivyo katika wakati wa mpito yaani *transition period* naomba tuwe makini, *EWURA* wawezeshwe katika kufanya kaguzi kwa kupewa vifaa nya kukagulia ili tusipoteze *fuel levy*, as it is tunapoteza mamillioni kwa sababu mafuta ambayo ni *transit* yanabakizwa nchini, tunapoteza mapato, ushauri wangu Serikali ichukue hatua za haraka na kuthibitisha hilo Serikali ifanyi mahesabu ya *fuel levy* ya mwezi Mei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulinda viwanda nya ndani/ Kiwanda cha Pareto Mafinga; hiki ni kiwanda cha pili duniani na Tanzania ni ya pili kwa kuzalisha pareto baada ya Tasmania-Australia na kwa taarifa tu, pareto ni zaidi ya *data* ya kuulia wadudu kama inavyojulikana, bali ni *final product* ni *component* muhimu katika masuala ya *military*. Sasa Kiwanda cha Pareto Mafinga kimekuwa kikitoa mbegu na huduma za ughani kwa wakulima wa zao la pareto, lakini sasa ikifika wakati wa mavuno, wanatokea walanguzi wanaongeza bei kidogo wanarusua maua ya pareto, kiwanda kinakosa malighafi, ajira zinakuwa hatarini kupotea, Serikali itakosa kodi na kadhalika. Ninaomba sana maelekezo yaliyotolewa na Serikali yaye kwa vitendo ili sio tu kulinda kiwanda hiki lakini pia kusimamia vitu kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabenki ya Serikali *TADB*, *TIB*, *TPB*; ninaandika kama *layman* wa *Banking Industry* lakini kama mfua tilijiwa masuala ya kitaifa, je, benki hizi zinapata faida? Kama hazipati faida ni kwa nini?

Nafahamu jitihada za kuunganisha benki ambazo zimeshaanza na tayari *TIB Corporate* na *TPB*, hata hivyo ninashauri benki hizi zote ziwe benki moja tu ambayo itajihusisha na kilimo/mifugo/uvuvi na uwekezaji, lakini lazima

tukubali kuwa *banking industry* huduma, ni biashara, kama tunataka tupige hatua basi benki hizi zizae faida ili ikopeshe wengine, kwa nini zije benki kutoka nje zipate faida halafu sisi benki zetu Serikali zisipate faida, labda tuamue kuwa ni vyombo vyao kutoa ruzuku.

Mwisho, je Benki ya Kilimo toka imeanza imekuwa na tija kwa kiasi gani? Vinginevyo tutalalamika mtaji mdogo, je, hata huo mtaji mdogo umeleta tija gani hata kama ni kidogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, tutazame mwenendo mzima wa hii benki, vinginevyo itakuwa *political bank of agriculture*, tuwe makini, huu ni uchumi *though* kila kitu ni siasa lakini uchumi usizidiwe na siasa. Naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. MNYAA MAKAME MBARAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kuniwezesha na mimi kutoa mchango wangu kwa maandishi kwenye hoja hii iliyopo mbele yetu ya Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Serikali yetu kwa kuondoa Kodi ya Ongezeko kwenye maeneo mbalimbali kwenye simu janja za mkononi (*smart phones*) HS Code 8517.12.00, vishikwambi (*Tablets*) HS Code 8471.30.00 au 8517.12.00 na modemu (*modems*) HS Code 8517.62.00 au 8517.69.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango alivyosema kwenye kitabu chake cha hotuba ya bajeti (ukurasa wa 29 mpaka 30) lengo kubwa la hatua hii ni kuhamasisha matumizi ya huduma za mawasiliano ili kufikia lengo la asilimia 80 ya watumiaji wa intaneti ifikapo mwaka 2025 kutoka asilimia 46 iliyopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upenyaji (*penetration*) mkubwa wa simu janja, vishikwambi na *modem* ni muhimu

sana kwa sababu zifuatazo; kwanza, wastani wa mapato kwa mtumiaji (*avarage revenue per user (ARPU)*) huongezeka kutokana na matumizi ya *data* kupitia vifaa tajwa hapo juu. Motokeo yake mapato ya makampuni ya simu huongezeka zaidi kutokana na utumiaji mkubwa wa *data*. Makampuni hayo yanaweza kupata faida zaidi na kulipa ushuru zaidi kwa Serikali. Aidha, simu janja na vifaa vingine tajwa hapo juu kwa ujumla hufanya maisha ya watumiaji katika Taifa lolote duniani iwe rahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, upenyaji mkubwa wa simu janja, vishikwambi, na *modem* huhamasisha uanzishwaji biashara mtando, huongeza utoaji wa huduma za jamii kama vile elimu mtandao, matibabu mtando na kadhalika. Kuongezeka biashara mbalimbali kupitia mtandao huongeza ushuru na mapato kwa Serikali. Aidha kuimarika kwa huduma za jamii kutapunguza umaskini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti mbalimbali duniani zinaonesha ya kuwa ongezeko la matumizi ya simu janja na matumizi ya Mkongo wa Mawasiliano kwa asilimia 10 hukuza Pato la Taifa kwa asilimia 1.2, huongeza ubunifu, tija katika maeneo ya kazi na ajira. Kwa hiyo hatua hii ya Serikali ya kuondoa kodi ya ongezeko kwenye vifaa hivyo ni ya kupongezwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa Serikali yetu kwa miaka minge imekuwa ikifanya jitihada za makusudi kupunguza bei ya bando (*gigabit* kwa sekunde (*GB*)) kwa dhamira ya ujumuishaji wa kidijiti na kukuza uchumi wa kidijiti nchini. Kwa bahati mbaya matokeo chanya hasa wananchi wa kipato cha chini na wananchi wa vijijini hayajafikiwa. Ninaendelea kuishauri Serikali yetu sikivu iendelee kupunguza bei ya *bundle* ili wananchi wote wa mijini na vijijini na wenye vipato vyta chini waweze kufaidika na TEHAMA na uchumi wa kidijiti. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iendelee kuwekeza kwenye mindombinu hasa maeneo ya vijijini ambako ndio kwenye Watanzania wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Mwisho ninaunga mkono hoja hii iliopo mbele yetu.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kulijaalia Taifa letu ustawi katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi, kisiasa, kidiplomasia, hali inayotufanya kuwa kelelezo mbele ya mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Watanzania wote kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Sita mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kupokea uongozi wa Taifa letu, hakika tumekuwa kielelezo mbele ya mataifa, nawaasa Watanzania wenzangu tumpe ushirikiano wa dhati na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu amjalie ulinzi, baraka na mafanikio katika kuliongoza Taifa letu Eeh Mungu mjalie baraka zako za milele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Jemadari wa Afrika na Mwana Mapinduzi na Mzalendo wa kweli, Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, viongozi na watendaji wote kwa jinsi tulivyotekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020 kwa kiasi kikubwa. Hakika tumwombee Hayati Mheshimiwa John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Taifa mchango wake tuukumbuke daima, pamoja na viongozi na Watanzania wote waliotangulia mbele za haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kwa Wizara hii ya Fedha kuititia Taarifa ya Hali ya Uchumi yam waka 2021/2022; kwanza Serikali itazame upya mfumo wa kukusanya kodi ya mapato kwenye taasisi za fedha hususan mabenki na mawakala wao kwani mara nyingi unapotoa hela kwenye ATM mbalimbali utaona ujumbe wa maneno kuwa hakuna huduma kwa sasa kwani mfumo huu utaikosesha Serikali kupata mapato yenye uhalisia. Sote tufahamu kuwa upatikanaji wa tozo na kodi

kwenye miamala ya fedha ukidhibitiwa vizuri na Serikali tutapata mapato mazuri kwa kuwa kiwango cha riba na tozo ni mkubwa katika taasisi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia TAMISEMI itazame mpango wa kutoa mafunzo ya Waheshimiwa Madiwani kufahamu majukumu yao katika kusimamia Halmashauri zetu nchini, kukusanya mapato ya ndani na matumizi ya mapato hayo, kushauri na kuhamasisha shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Serikali Kuu kwa azma yake ya kulipa posho za Madiwani kupitia mapato ya Hazina hivyo basi kuna sababu mahususi za kutazama fedha zilizopangwa awali kupata miongozo yake kwa Waraka kutoka TAMISEMI ili mchanganuo wake uwasilishwe kwenye kikao cha Kamati ya Fedha ya mwezi Julai kwa waraka badala ya maelekezo kwa fedha zile nyingi ili sehemu itakayobaki isaidie kuchangia miradi ya maendeleo kwenye kata na vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Serikali iangalie kiwango cha posho ya vikao kwa Waheshimiwa Madiwani kwani kiasi cha shilingi 40,000 kwa Diwani wa Kata kuhudhuria kwa robo mwaka kwa kikao kimoja tu ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono kwa asilimia 100 na naomba kuwasilisha.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango mfupi wa mdomo, napenda nisitizie juu ya uwekezaji kwenye ardhi. Inakisiwa kuwa ifikapo mwaka 2050 dunia itakuwa na watu wapatao bilioni 9.7. Watu wote hawa watahitaji kula, hivyo watahitaji ardhi kwa ajili ya kilimo. Nchi yetu haina umakini wa kutosha namna tunavyowapa wageni ardhi. Wawekezaji wengi wanakuja tunawauzia ardhi kwa maana kuitumia kwa shughuli za kilimo kwa miaka 33, 66 au 99.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kihistoria haina ardhi tupu. Aidha, itakuwa inamiliikiwa na familia, koo fulani au Serikali za vijiji. Mara nyingi wakija hawa wawekezaji tunazichua ardhi hizi kutoka kwa watu wanaohodhi na kuwapa wawekezaji kwa bei ndogo sana na kwa kuwa maeneo ya uwekezaji kwenye ardhi yanazidi kupungua, tusipozingatia tutakuja kujikuta ardhi imekwisha na kundi kubwa vijiji litabaki bila ardhi na hii inaweza kuwa hatari kwa usalama na usitawi wa watu na Taifa lao.

Napendekeza itungwe sheria au miongozo ya kusaidia Watanzania wabaki na ardhi yao ila itambuliwe mahali ilipo, inamiliikiwa na nani na kiasi gani na inafaa kwa kilimo cha mazao gani. Mwekezaji akija tumwambie ardhi ya uwekezaji ipo mfano Kalenga ni eka kadhaa inamiliikiwa na kijji au watu binafsi. Unakaribishwa kuwekeza ila ardhi sio yako ingawa unaruhusiwa kuwekeza mfano kwa miaka 40 lakini tutamiliiki kwa hisa ardhi hiyo wewe mgeni chukua asilimia 80 kwa kuwa unaleta pesa na ujuzi na kijji au mtu binafsi wachukue asilimia 20 ya mazao au faida inayotokana na mazao hayo. Jambo hili niliona muhimu sana, litavijengea uwezo vijiji vyetu na watu wetu, itaimarisha uchumi wa vijiji na watu wake. Nimeangalia muundo wa Dubai (*Dubai Land for Equity*). Alichotakiwa kuwa nacho Mdubai ni ardhi tu iliyopimwa. Wawekezaji walikwenda kutoka Ulaya, Marekani na kwingineko. Iwe hivyo kwenye ardhi yetu kwa faida ya nchi yetu na watu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba leo tena niendelee kuishauri Serikali kwa jambo lake zuri sana la kuweka tozo ya shilingi 100 kwenye mafuta, naomba Serikali iende mbali zaidi kwa kuiwekea wigo fedha hizi ili ziwe kwa ajili ya *TARURA* tu yaani ziwe *ring fenced* kama ilivyo kwa fedha za mafuta hata zile za miamala ya simu nazo zielekezwe moja kwa moja (*RUASA*) maji vijiji na zile za *line* za simu zielekezwe moja kwa moja maji mijini, kuliko ilivyo sasa fedha hizi zote ziko tu hewani hazijawa *ring fenced*, hivyo kufanya rahisi kutumika nje ya makusudio.

**MHE. ABDI HIJA MKASHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanzana namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mahiri katika majukumu yake ya kila siku namuombea kwa Mwenyezi Mungu uhai na uzima katika maisha yake yote na pia nampongeza Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha kwa uwasilishaji wake wa bajeti iliyosheheni Tanzania kwa ujumla.

Mimi napenda kuchangia moja kwa moja kwenye sehemu mbili kama ifuatavyo; mosi napenda kuchangia katika Wizara ya Uvuvi na Mifugo kwa kuwa nchi yetu Mwenyezi Mungu ameibarikia rasilimali ya bahari na maziwa. Mimi naishauri Serikali yangu kuitumia vyema rasilimali hizi tulizonazo kwa kuwanyanya wavuvi wetu wadogo wadogo ili waweze kujikimu kwa pamoja na kulipatia faida Taifa letu kiujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni suala zima la Jeshi letu la Polisi; kiukweli Jeshi letu la Polisi linafanya kazi kubwa mno katika Taifa letu, lakini ni vema Serikali itazame upya suala zima katika stahiki zao kwa vile kipato chao si kikubwa, ni vema waangaliwe upya ili waweze kuonekana na wao. Kwa bahati mbaya huwa wanapatiwa *refreshers course* kwa ajili ya kuwapa utayari wa majukumu yao ya kila siku, lakini huwa wanajigharamia wenyewe. Jambo hili linawapa askari wetu wakati mgumu na hawatokuwa na morali na kama huna morali katika kazi za kila siku hata ufanisi wa majukumu ni lazima yatakuwa madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishauri Serikali ilione na hili ili waweze kuwa na morali ili waweze kufanya vyema kazi zao zaidi, lakini pia na Idara yetu ya Uhamiaji ikumbuke kwamba Tanzania Zanzibar kiujumla ni nchi ambayo ni Visiwa. Visiwa vile vimezungukwa na bahari, sasa huwa kuna bandari bubu nyingi sana. Naishauri Serikali ni vyema inunue boti za kisasa ambazo kwa kushirikiana na Uhamiaji na Jeshi la Polisi ili waweze kufanya doria katika maeneo yetu yaliyotuzunguka kwa lengo zima la kuwasaka wale

wafanyabiashara haramu pamoja na wahamiaji haramu ili kudhibitiwa wakati wanapokuwa katika kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. OTHUMAN HIJA JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Mwaka 2021/2022.

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa namna alivyoanza kuonesha uwezo mkubwa wa kuliongoza Taifa letu. Namuombea kila la kheri katika maisha yake na tatu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwasilisha hotuba hii kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu sera na mikakati ya kuongeza mapato; Mheshimiwa Waziri ametaja hatua kadhaa kama nane hivi ambazo kama tukizisimamia zitatuwezesha kufikia malengo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua hizo bado kuna maeneo ambayo kama Serikali ikiziboresha zinaweza kutuongozea mapato ya ndani. Moja katika sehemu hizo ni sehemu ya bandari bubu. Bandar bubu ni moja kati ya sehemu nyeti sana ambazo kama zikiboreshwaa zinaweza kutuongozea mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika suali hili ni kuiomba Serikali kuziboresha kwa kuzipelekea wafanyakazi wa Mamlaka za Mapato wenye kutambulika na Serikali na wenye ujuzi wa kufanya kazi za ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu Jeshi la Polisi; naipongeza sana Serikali kwa kuwaondoshea askari tatizo la ajira. Tatizo hili ni la muda mrefu sana na lilikuwa linawadhalilisha askari wetu. Lakini hatuba hii imeacha kuzungumzia makazi na vitendea kazi kwa askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya muda wa zaidi ya miaka hamsini bado kuna maeneo ambayo makazi ya askari wetu hayaridhishi, majengo ni mabovu sana ambayo hayastahili kutumika na askari wetu. Ushauri wangu katika jambo hili ni Serikali kulishughulikia kwa nguvu zake zote suala hili la makazi na vitendeya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu wakulima wadogo wadogo; lazima tukubali kuwa katika nchi hii wakulima wetu wanafanya kazi kwa bidii kubwa lakini bado wanakwazwa na mambo kadhaa katika maisha yao ya kikazi. Wanakabiliwa na upatikanaji wa pembejeo kwa kiasi kikubwa sana. Bado mazingira ya utendaji wa kazi zao sio rafiki. Aidha, wakulima wetu wanakabiliwa na uwezo mdogo kifedha. Mabenki yanawapatia mikopo yenye riba kubwa sana ambayo yanawapelekea kufilisika kabisa. Ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kuwatengenezea mazingira mazuri ya kupata mikopo yenye mashart nafuu ili waweze kuijendeleza na kazi zao hizi. Naunga mkono hoja.

**MHE. ABEID R. IGHONDII:** Mheshimiwa Naibu Spika, mambo machache muhimu naomba yazingatiwe kama ifuatavyo; kwanza bajeti ya kilimo iongezwe kwani kiasi cha fedha kilichotengwa kwa sasa hakiwezi kukidhi kuleta mageuzi kwenye kilimo.

Vilevile mpango mkakati wa kuongeza uzalishaji wa alizeti katika mikoa ya Singida, Dodoma na Simiyu uliozinduliwa Singida hivi karibuni na Waziri Mkuu utekelezwe kwa vitendo na uwe endelevu, isiwe ni jambo la mwaka huu kwa sababu ya upungufu wa mafuta, lakini liwe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu posho za Madiwani; naipongeza sana Serikali kwa utaratibu

iliopendekeza wa kuwalipa Madiwani kuititia Serikali Kuu na moja kwa moja kwenye akaunti zao. Ushauri ni kwamba ni vyema kiwango wanacholipwa kiongezeke kutoka shilingi 350,000 hadi shilingi milioni moja au 700,000 kwa mwezi kwani Diwani ndio msimamizi wa miradi yote ya maendeleo inayokwenda kwenye kata yake ambayo ni ya mamilioni ya fedha, kumuacha Diwani akilia njaa huku anasimamia miradi mikubwa ya maendeleo haileti picha nzuri. Anaweza kushawishika kuhujumu au kuingia kwenye upigaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Diwani ndio msimamizi wa wataalam wote kwenye kata yake. Anahitajika awe vizuri kiuchumi ili aweze kuifanya kazi hii kwa ukamilifu. Pia Diwani ndio anaishi na jamii, matatizo yote yanaelekezwa kwake, akiwa na posho ya milioni moja atawea kusaidia jamii na kuisemea ipasavyo Serikali hapo kwenye eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi laki moja kwa Maafisa Tarafa; napongeza sana hatua hii ya Serikali kuwapatia shilingi laki moja Maafisa Tarafa kila mwezi. Hata hivyo kumejitokeza manyanyaso kutoka kwa ma-DAS wakisema kuwa sasa watasitisha kuwapa posho za mafuta ya pikipiki na matengenezo (*OC*) kati ya shilingi 50,000 hadi shilingi 250,000 au mafuta ya petroli lita 50 walizokuwa wanawapatia Maafisa Tarafa hapo awali.

Naomba katika majibu ya Waziri alitolee ufanuzi jambo hili na kukemea kauli na matendo wanayoanza kuoneshwa na ma-DAS dhidi ya Maafisa Tarafa kuwa watasitisha kutoa zile walizokuwa wanawapa. Naomba hii ifahamike na itajwe na Waziri kuwa ni ku-top up ile posho waliyokuwa wanapewa ili kuboresha utendaji kazi wao. Jambo hili limejitokeza kwa Wilaya ya Singida ambapo Maafisa Tarafa wameanza kutishiwa/kuacha kupewa posho/*oc* waliyokuwa wanapewa hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji na jinsi anavyoendelea ku-fit katika nafasi yake.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais mama yetu mpendwa kwa kusikia kilio cha wananchi. Nampongeza pia Waziri wa Fedha na wasaidizi wake kwa kutuletea bajeti nzuri inayokidhi mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natoa pongezi kwa Serikali kusikia kilio cha bodaboda, Madiwani, Watendaji wa Kata na Vijiji. Ushauri wangu kwanza Serikali ipange maeneo ya kutosha ya kilimo na kupunguza au kuondoa migogoro kati ya wakulima na watumiaji wengine wa ardhi (matumizi bora ya ardhi) ili kupunguza migogoro kati ya wafugaji na wakulima ambayo pia imekuwa kikwazo kati ya wafugaji na wakulima katika ustawi wa maendeleo ya sekta ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi tumeona makundi haya mawili kuwa na uhasama mkubwa. Mipango ya matumizi bora ya ardhi yaainishwe kwa mpango wa ramani ili kila mmoja ajue mipaka yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, masoko endelevu ya mazao; wakati tunapitisha bajeti ya Wizara ya Kilimom, Waziri alisema tunataka Bunge hili la Kumi na Mbili liwe la mapinduzi, naishauri Serikali ihakikishe inatafuta masoko ya uhakika ya mazao ya wakulima wetu. Wakulima waruhusiwe kuuza nje ya nchi na masoko mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, bajeti ya Wizara ya Kilimo ya shilingi bilioni 294.1 ni ndogo sana, Serikali ijipange kwa bajeti zijazo kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo angalau ifike asilimia tano ya bajeti yote kwani kutokana na ufinyu maeneo haya huathiriwa na upungufu wa wataalum, zana za kilimo /vyombo vyaya usafiri na OC na kutokuwepo kwa mashamba ya kuzalisha mbegu ndani ya nchi hali ambayo pia itafanya mkulima kupata pembejeo za kilimo hususan mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima wa afya na kuweza kuandika mchango huu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali chini ya uongozi wake Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuleta bajeti hii iliyolenga kuwapa matumaini wananchi wa Tanzania kwa kuondoa baadhi ya changamoto zinazoendelea kuwakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba bila makusanyo ya kodi hatuwezi kufika mbali kimaendeleo wala hatuwezi kutekeleza miradi ya maendeleo tunayopanga. Lazima wananchi wa Tanzania waweze kuwa na uelewa mpana kuhusu uwajibikaji na wigo wa kukubali kukusanya kodi kupitia wafanya biashara wakubwa na wadogo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa sio waaminifu katika kutumia mashine za kielektroniki. Wamekuwa wakisingizia kuwa ni mbovu au kukusanywa na *TRA*. Jambo hili limekuwa likidhoofisha sana ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Tumekuwa na juhudhi kubwa kama wananchi wa Tanzania tunaponunua bidhaa madukani кудai risiti, lakini kwa muda mrefu sasa wafanyabiashara walio wengi wamekuwa hawatoi risiti wanapofanya mauzo. Niiombe sana Serikali, usimamizi iliyoueleza kupitia hotuba hii ya bajeti iwhahishe wafanyabiashara wote waliostahili kutumia mashine za *EFD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yetu kwamba wale wote wanaopaswa kutumia mashine za kielektroniki watatekeleza wajibu wao lakini pia wanaopaswa kusimamia ukwepaji kodi kwa wafanyabiashara hawa wataweza kusimamia ipasavyo. Pia ni mategemeo ya wananchi kwamba vyanzo vipyta vilivyoainishwa kukusanywa kupitia mafuta na miamala ya simu itaweza kukusanya ipasavyo na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopangwa. Wananchi hawana maswali mengi pale wanapoona fedha

yao inayochangwa na kukusanya na kuona kwa uhalisia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo lililokuwa changamoto kubwa kwa wananchi ni suala la tozo kwa bidhaa hata za nyumbani kuendelea kutozwa kodi. Ni furaha ilioje kwa wananchi wa Tanzania kuona bajeti hii imekuja kuondoa kabisa changamoto hii. Ni imani ya wananchi kwamba zile changamoto nyingine zilizobaki zitawezza kufanyiwa kazi hatua kwa hatua. La msingi wananchi tujitahidi kuchangia makusanyo ya kodi ili fedha itayopatikana iwe mfano wa kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopangwa ili bajeti ijayo iweze kutatua changamoto nyingine zilizobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi wananchi wamekuwa wakihoji kuhusu fedha za Jamhuri ya Muungano kuititia Mfuko wa Pamoja wa Fedha. Niwaombe tu wananchi wa Zanzibar kuangalia miradi inayoendelea kutekelezwa kwa upande wa Zanzibar kuititia Mfuko wa Jamhuri ya Muungano na kufuatilia gharama ya fedha zilizotumika kuititia miradi hiyo. Hii nchi ni moja na utekelezaii wa miradi unaendelea vizuri, muhimu tuendelee kulipa kodi kwa manufaa ya Watanzania wote. Tuendelee kusimamia mapato yanayotokana na kodi kwa manufaa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache naunga mkono hoja.

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia natoa pongezi kwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussem Ali Mwinyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kuhusu uvuvi wa bahari kuu. Mnamo mwaka 1980 kilikuwepo chuo kinachofundisha somo la *fisheries*, hili somo ni zuri sana kwa sababu wananchi wetu itapelekea kupata ajira na

kupelekea kupunguza umaskini na kuwezesha viwanda katika uchumi wa bluu. Wananchi wa Tanzania ni wavuvi ambao wamekulia katika mazingira ya uvuvi ipo haja Tanzania kuwa na wataalamu wa uvuvi. Naomba kuishauri Serikali ya Tanzania kushiriki katika uchumi wa bluu kwa kufanya yafuatayo; kwanza kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha kupata vibali vya ajira ili itusaidie kupunguza umaskini kwa namna moja au nyingine. Pia naishauri Serikali iweze kuweka njia ya kuwafundisha vijana wetu na kufufua rasilimali zetu na kutumika. Kwa mfano kuweka ufgajji wa kaa/majongoo/samaki na kadhalika na pia tuweke vizimba kwa wingi vya mazao ya baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunanunua meli za uvuvi lakini hatujajiandaa na wataalamu wa uvuvi wa bluu. Pia kwa sasa naomba kuishauri Serikali kwamba Chuo cha Uvuvi kijengwe Zanzibar kwa sababu Zanzibar imezungukwa na bahari na mikoa yake yote ina pwani na mikoa ya nyanda za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inawasaidiaje vijana ili kuwawezesha na kuwashirikisha katika uchumi wa bluu? Naomba kuiomba Serikali tuweke mazingira mazuri ili kuwezesha wananchi kupata mitaji ili waweze kushiriki katika uchumi wa bluu na pia kupata pesa za kigeni, kupunguza umaskini na kukuza utalii wetu. Ahsante

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa mzima na kuendelea na Bunge lako Tukufu salama.

Nampungeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuleta bajeti hii yenye faida kwa Watanzania, vilevile na Rais wa Zanzibar kwa kuwasilisha bajeti yake yenye muono wa uchumi wa bluu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampungeza Waziri wa Fedha na Naibu wake na watendaji wake wote kwa kazi nzuri waliyofanya kukamilisha bajeti hii yenye mashiko, bajeti

hii imebeba sekta tofauti tofauti na mimi nichangie sekta ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua na inathamini mchango wa sekta ya umma na binafsi katika kukuza pato la Taifa kwa kupunguza kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia tisa hadi asilimia nane. Kodi ya wafanyakazi kwa kiwango kimepunguzwa kutoka asilimia 11 mwaka 2015. Serikali imetenga shilingi bilioni 449 kwa ajili ya kuwapandisha vyeo watumishi 926,619. Natoa hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vyaa kodi, ada na tozo mbalimbali nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kupendekeza na kufanya marekebisho ya vyanzo vyaa kodi hizi ikiwemo tozo na ada ikiwemo tozo na ada zitokanazo chini ya Sheria ya Ajira na usimamizi wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Madiwani kwa kuwa awamu ya tano na ya sita imejenga utaratibu na uzoefu wa kukaa pamoja katika sekta zisizo za Muungano, namuomba Waziri wa Fedha akae na Waziri mwenzake wa Zanzibar haya mambo mazuri yanakwenda kukivusha Chama chetu cha Mapinduzi mwaka 2025, tuhakikishe nayo yanakwenda kufanyika na upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka posho kwa Madiwani wa Tanzania Bara basi tuhakikishe na upande wa Zanzibar yanakwenda kufanyika lakini ni ndogo mno, kwa hivyo ni vyema iongezwe ili waweze kufanya kazi kwa weledi zaidi na kudumisha Muungano wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambazo ameendelea kuzifanya, naipongeza Wizara ya Fedha kwa bajeti nzuri na bila kusahau Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Daniel Sillo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti yetu ni bajeti ambayo itaondoa changamoto nyingi za wananchi wetu. Hakuna Serikali inayotekeleza miradi yake bila ya kulipa kodi, hivyo niwaombe wananchi wenzangu tulipe kodi kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kwenye eneo la miradi ya kimkakati; miradi hii ya kimkakati ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba kila Halmashauri inajitegemea yenye wekiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali wakati wa upembuzi yakinifu wa miradi hiyo ni vyema tukawashirikisha wananchi pamoja na wadau wa maendeleo kwenye maeneo hayo badala ya ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoa mfano Mkao wa Ruvuma, Wilaya ya Songea Mjini kuna mradi mkubwa wa mabasi kule umejengwa wenye umbali wa takribani kilometra 21, kama wananchi wale pamoja na wadau wake wangeshirikishwa mradi ule ungejengwa lakini sio kwa umbali ule. Hivyo niiombe Serikali kufanya ushirikishwaji jamii wakati wa utekelezaji na hiyo ndio dhana ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi viporo; ninaipongeza Serikali kwa kufanya mabadiliko ya Kanuni ya 21 ya Sheria ya Bajeti, Sura Namba 439 ya kuondoa urejeshwaji wa fedha za miradi kila ifikapo tarehe 30 Juni kila mwaka, na hivyo kusababisha fedha zile zitekeleze miradi yake kama ilivyokusudiwa. Niiombe Serikali kuhakikisha kwamba miradi ile iliyopangwa itekelezwe kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, kuimarisha Kitengo chake cha *Monitoring and Evaluation* (Tathmini na Ufutiliaji) kwa kuunda timu ya kikanda na ya kitaifa katika kufanya ufuutiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo, kila robo mwaka ikiwashirikisha Madiwani pamoja na Wabunge wa maeneo

husika kwa kila sekta. Kwa kufanya hivyo tutajua tumetoka wapi, tupo wapi na tunaelekeea wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwisho ni kwenye eneo la ajira; ajira ni changamoto, asilimia 80 ya Wabunge katika kipindi hiki tumeshuhudia wananchi wetu wakitupigia simu za kuomba tuwasaidie kupata ajira. Ninaiomba Serikali yetu iweke uwiano katika utoaji wa ajira kwa kila Mkoa lakini kwa kuzingatia sifa za waombaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba nchi yetu hii ni kubwa sana na hivyo wananchi wake wapo vijijini na Mikoa ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na Mawaziri wote kwa ushirikiano wao leo wameweza kupunguza kodi ya asilimia sita kwenye mkopo ya elimu ya juu, maana wazazi tumepata nafuu kwa msaada huu tuliopewa kwa watoto wetu kutoka kwa huruma na mapenzi ya mama yetu Mama Samia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sisi Wabunge wote tumefarajika sana kuona Madiwani, Maafisa Tarafa na Watendaji wa Kata kwa kupewa posho kila mwezi kuitia kwenye *account* zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la posho kwa watendaji wenzetu limetupa faraja sana sisi Wabunge maana kusema kweli walikuwa na hali ngumu sana ya utendaji wao wa majukumu yao wakati wao ndio wapo na wananchi muda mwingi kuliko sisi Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuwakumbuka wastaa fu kulipwa kwa wakati, kwani wastaa fu wengine wanafariki wakati haki yake hajaipata, anakuja kulipwa mrithi yeye aliyetumikia ajira hajaigusa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kupunguza muda wa mikataba ya Jeshi la Polisi kutoka miaka 12 hadi miaka sita, hii tutafanya askari wetu waendelee kuilinda amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niaishukuru Serikali kwa kuamua sasa tozo ya viza ya wageni wanaoingia Zanzibar ibaki Zanzibar na Tanzania Bara ibaki Bara hii imepunguza kero za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru viongozi wetu wote mama yetu kipenzi Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba na Mawaziri wote kwa kazi nzuri ya kutuogoza na kulitumikia Taifa letu na wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishukuru Serikali kwa kurejesha VAT kwenye bidhaa zinazonunuliwa Tanzania Bara na kutumika Tanzania Zanzibar. Pia naipongeza Serikali kwa kuondoa kero kwa vijana wetu waendesha pikipiki (bodaboda) kwa kupunguza faini ya makosa ya barabarani kutoka shilingi 30,000 hadi shilingi 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Mipango na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kuwasilisha vizuri sana hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali na maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii imeelezea mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyowasilishwa ni nzuri na inalenga kulipeleka Taifa letu hatua moja mbele. Kwa mantiki hiyo, ninaiunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa bajeti hii imeheshimu mawazo ya Wabunge katika michango yao toka Bunge la Kumi na Mbili llianze, isipokuwa kilio cha kuongeza bajeti ya kilimo na mifugo hakikuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii, Serikali imebainisha maeneo muhimu ya kipaumbele kwa mwaka 2021/2022. Kwa upande wa wafanyakazi, ninaipongeza Serikali kwa kupunguza kodi ya mapato ya ajira (*PAYE*) kwa wafanyakazi kutoka asilimia tisa hadi asilimia nane. Hatua hii kwa kiasi imewapunguzia wafanyakazi mzigo mkubwa wa kodi na kuboresha maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuipongeze Serikali kwa kuboresha mazingira ya kazi kwa Madiwani na Watendaji wetu wa Kata. Serikali imeonesha nia njema sana ya kuzijali kada hizi zinazofanya kazi na wananchi katika ngazi ya vitongoji na vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze pia Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 328.2 kwa ajili ya kugharamia Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Zoezi hili ni muhimu sana kwenye kupanga maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika michango mbalimbali, tuliwasikia Wabunge wengi wakilalamikia tozo mbalimbali zilizokuwa zinawaumiza vijana wa Kitanzania waliokopa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Naipongeza Serikali kwa kufuta tozo ya asilimia sita iliyokuwa ikitozwa kwa ajili ya kulinda thamani ya mkopo wa elimu ya juu kwa wanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine liliolalamikiwa na Wabunge ni watumishi kutokupandishwa madaraja kwa kipindi cha miaka mitano na zaidi iliyopita. Ninaipongeza Serikali kwa kutenga jumla ya shilingi bilioni 449 kwa ajili ya kuwapandisha vyeo watumishi 92,619. Hatua hii itawapa motisha na kuboresha maisha ya wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu kumekuwepo na changamoto za muda mrefu za ulipaji wa mafao kwa wastaifu kutokana na ufanisi mdogo wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika kuhudumia wastaifu wetu. Ninaipongeza Serikali kwa kuja na mkakati wa kulipa madeni yanayodaiwa na mifuko kwa kutenga fedha kwenye bajeti na kutumia utaratibu wa kutoa hatifungani maalum isiyo taslimu zitakazoiva kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo ya Waziri hatua hii inakwenda kumaliza kabisa tatizo hilo la wazee wetu kudai haki yao. Katika bajeti hii Serikali imependekeza kuwa kuanzia sasa wanataka kuanza kulipa michango hiyo moja kwa moja kutokea Hazina kwa taasisi zote ambazo watumishi wanalipwa na Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze Wizara kwa nia njema ya kufanya mabadiliko katika Kanuni ya 21 ya Sheria ya Bajeti ili kuondoa changamoto iliyopo ya fedha ambazo hazijatumika hadi tarehe 30 Juni ya kila mwaka kurejeshwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Mabadiliko haya yamekuja wakati muafaka na yatasaidia sana kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika idara mbalimbali za Serikali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Waziri kwa kuja na mapendekezo ya vyanzo vipyta vya mapato. Mimi naunga mkono mapendekezo yake na niwaombe Watanzania wote waelewe kwamba Taifa letu litajengwa na sisi wenyewe. Pendekezo la kulipia kodi ya majengo kupitia matumizi ya umeme (LUKU), tozo za simu na tozo za kutumia miamala ya fedha ni ubunifu mzuri. Hapa Serikali itaongeza idadi ya walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa ilithibitika kuwa kulikuwa na ushiriki kidogo wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Pili. Kwa kiasi kikubwa utekelezaji ulifanywa na taasisi za Serikali. Hii ilitokana na tabia mbaya iliyokuwa imejengeka kwenye sekta binafsi ya kuza

huduma kwa bei kubwa. Kazi hiyo hiyo ilifanyika kwa bei ya chini sana na kwa kiwango kizuri kwa kuzitumia taasisi za Serikali. Katika Mpango wa Tatu, ninaishauri Serikali ishirikishe sekta binafsi kwenye utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaishauri Serikali katika maeneo machache yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaishauri Serikali ishirikishe sekta binafsi kwenye utekelezaji wa miradi ya Serikali iliyopo kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa. Katika hili, sekta binafsi wahamasishwe na kuelekezwa wawe waaminifu kwenye kutoa gharama halisia za utekelezaji kwani wameshajifunza makosa waliyofanya siku za nyuma. Wakishirikishwa kikamilifu, watazalisha ajira, wigo wa walipa kodi utapanuka na mapato yataongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika Bajeti Kuu ya Serikali ya shilingi trillioni 36.33; asilimia 29.3 (trillioni 10.66) zitatumika kulipia Deni la Taifa. Kiasi hiki ni kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali ibuni vyanzo vipyta vya mapato kwani wigo wa kukusanya bado ni finyu sana. Napendekeza ianzishwe tozo mpya kupitia malipo kwenye mita za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, biashara ndogo ndogo zimepanuka sana na wengi huwa hawalipi kodi. Ninaishauri Serikali ibuni mikakati madhubuti ya kukusanya kodi kutoka kwa wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ninaishauri Serikali iendelee na kuboresha mazingira kwa wawekezaji wa ndani na nje. Tukipata wawekezaji wengi, ajira, wigo wa kulipa kodi na mapato ya nchi vitaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Serikali inategemea kukopa shilingi trillioni 7.34 kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi trillioni 4.99 zitakopwa ndani na shilingi

triliuni 2.35 zitakopwa nje. Katika hili Serikali inapochukua mikopo mikubwa kutoka ndani (mabenki yetu), itakuwa inaminya sekta binafsi kukopa na kuzyumbisha. Sekta binafsi zikiyumba, ajira zitakosekana na wigo wa kulipa kodi na mapato kuathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Wabunge wengi waliotoa mawazo katika michango yao, walishauri ufanyike uwekezaji wa kutosha katika sekta za uzalishaji (kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda) na walipendekeza bajeti ya sekta hizi ziangaliwe kwa jicho la pili. Bahati mbaya, Serikali haikuzingatia maoni ya Wabunge wengi. Ninaishauri Serikali kwenye bajeti itakayofuata ya mwaka 2022/2023 iongeze Bajeti ya Kilimo na Mifugo kwani inaaajiri asilimia 65 ya Watanzania.

Mheshimiwa Nailbu Spika, saba, Serikali imelimbikiza madeni mbalimbali ambayo wazabuni wameshatoa huduma. Ninaishauri Serikali ilipe madeni ambayo uhakiki umekamilika. Kwa mfano, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (*NMA/ST*) iliyoko Arusha ina deni (shilingi 6,007,562,000) lililohakikiwa muda mrefu, lakini malipo hayajafanyika. Ninaiomba Serikali isaidie kwenye hili ili shughuli za kukuza hii taasisi zisikwame.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo na ushauri wangu, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mheshimiwa Prof. Joyce Lazaro Ndalichako ajiandae.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia hoja hii ambayo naiunga mkono kwa sababu inakwenda kujibu hoja zote ambazo zimetolewa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetolewa hoja ya uboreshaji wa miundombinu ya kusafiri kwa njia ya maji

ambayo; kama mlivyoshuhudia wengi tayari tumekwisha rekebisha katika Ziwa Victoria na juzi tarehe 15 Juni, 2021 Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan alizindua pale Mwanza meli ya MV Victoria na MV Butiama pamoja na Chelezo, na huo ulikuwa ndio mwanzo. Na katika mwendelezo wake tukavishuhudia tarehe 15 mwezi wa sita...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati mwingine ndiyo maana huwa tunarudia hoja zile zile kila wakti. Na wakati mwingine hata maswali yetu ya nyongeza yanazunguka pale pale. Tuwe na uvumilivu wa kusikiliza wenzenetu wanapochangia. Na sasa mnaona wachangiaji wanaofuata ni upande wa Serikali, sikilizeni michango yao itawasaidia kujua nini cha kuuliza, nini cha kuchangia. Mheshimiwa Dkt. Chamuriho.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naendelea pale pale; katika hoja iliyotolewa ya miundombinu ya maji tulishuhudia tarehe 15 mwezi wa sita Mheshimiwa Rais Wetu Samia Suluhu Hassani alishuhudia utiaji saini wa mikataba mitano ambayo ilikuwa inalenga katika kuboresha usafiri wa maji. Alishuhudia mkataba wa Meli kubwa katika Bahari ya Hindi ambayo ni tani 2,800 ambayo imelenga usafiri kati ya hapa na Comoro. Alishuhudia meli kubwa katika Ziwa Tanganyika ambayo vile vile ina meli yenye uzito wa tani 2,800, alishuhudia utiaji wa saini wa meli kubwa ya abilia 600 katika Ziwa Tanganyika pamoja na uzito wa shehena tani 400. Vile vile alishuhudia utiaji wa saini wa meli mpya ya tani 3,000 katika Ziwa Victoria pamoja na ukarabati wa MV Umoja. Kwa hiyo bajeti hii ambao inakwenda kujibu maswali hayo naiunga mkono kwa sababu hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye Bandari, upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara unaendelea na bajeti hii inakwenda kukamilisha; kwa hiyo unakwenda kutatua matatizo hayo. Katika Bandari ya Dar es Salaam lile gati la RoRo limekamika na magati namba moja hadi saba yamekamilika na sasa hivi tunamalizia pale ile yard ya kuelekea makasha. Hivyo bajeti hii itaimarisha

kuimarisha lango hilo vizuri sana. vile vile lango la kuingilia katika Bandari ya Dar es Salaam linakwenda kupanuliwa, na sasa hivi pale tutaingiza meli kubwa kabisa ambazo zinaweza kubeba hadi makasha 7,000 hadi 8,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bajeti hii tutaagiza mitambo mikubwa ya kupakulia na kupakilia mizigo maalufu kama *SSG Shore to Sea Gantry* ambazo zimeagizwa kwa kutumia na bajeti hii. Katika Bandari ya Tanga vile vile lango la kuingilia pale limechimbwa, ambalo litakamilishwa kwa kuongeza gati mbili kubwa za mita 250, 250 ili tuweze kupokea meli kubwa za mita 300. Vile vile Mtwara tunafanya vivo hivyo tunaongeza magati mawili ambayo tayari yanakamilika na sasa hivi tunaagiza vifaa vya kupakilia mizigo, hivyo bajeti hii inakwenda kutatua hayo matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa reli vile vile tulimshuhudia Rais wetu mpendwa tarehe 14 mwezi wa sita akiweka jiwe la msingi katika Reli ya Standard Gauge kutoka Mwanza hadi Isaka. Kwa hiyo inadhihirisha kwamba bajeti hii ambayo itakwenda kukamilisha kipande hicho inatekeleza mwendelezo wa kazi hizo ambazo tumeziendeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchangiaji vile vile iliongelewa hoja ya *TARURA*, kwamba tuaingalie; na ni kweli katika marejeo ambayo tumeyafanya ya uwiano wa mgawanyo wa fedha za mfuko wa barabara ambao tumebaini kwamba ulifanyika mwezi Disemba, 2020 tumebaini kwamba tatizo kubwa siyo mgao wa fedha bali ni kiasi kidogo cha fedha za mfuko. Tayari mmeona katika bajeti hii hatua zimeanza kuchukuliwa katika kuongeza bajeti hii, ni muhimu tuiunge mkono kwani inakwenda kutatua hayo matatizo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeongelewa miundombinu ya Jangwani pale katika mchango wa bajeti hii. tayari *TANROADS*inafanya pale usanifu wa kina ili tuweze kupata utatuzi wa changamoto hiyo na ambayo katika ukamilifu wake tutaweza kupata utatuzi, kwamba tufanye nini pale ili mafuriko ya pale Jangwani na ile miundombinu

ya Mwendokasi iweze kulindwa na tuweze kuendelea na kutoa huduma pale. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika michango iligusiwa sheria yetu ya barabara ya Namba 13 ya mwaka 2007 ambayo ilikuwa inaongelea kuzuia malori yanayozidi tani 10 kuelekea katika vijiji vyetu ambavyo ililenga kwamba tuiachie. Sheria hiyo imezingatia uwezo wa barabara zetu za kule na kuzilinda hivyo lengo lake ni kulinda miundombinu ya zile barabara hasa madaraja yake. Hivyo, sheria hiyo tutaendelea kuizingatia ili kulinda miundombinu hiyo. Lakini tuendelee kuongeza ulipaji kodi ili tuweze kupata fedha zaidi za kutosha kuweza kuimarisha miundombinu hiyo ili iweze kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ilitolewa rai hapa kwamba kuna ahadi nyingi katika miundombinu ya barabara ya viongozi wa Taifa. Hapa tunarudia kusema tena kwamba hizi ahadi za kitaifa tunazipangia mkakati wa kuzitekeleza. Imetolewa hoja kwamba tuziwekee *database* na hilo ambalo tumelifanya. Kwamba ahadi zote za kitaifa zilizotolewa katika ujenzi wa barabara, vivuko nakadhalika tutazizingatia kulingana na vipaumbele vyake katika bajeti zitakazokuwa zinaendelea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile ilitolewa rai ya kupunguza msongamano wa magari katika babara inayokwenda Tunduma hasa pale Mjini Mbeya katika barabara ya Igawa hadi Tunduma. Hilo nalotunaenda nalo, na kwa sasa hivi tunamalizia ule upembuzi yakinifu wa ile bypass ili itakavyokamilika katika bajeti hii tuanze na utekelezaji wa ujenzi wa barabara ile ambayo inaondoa changamoto hiyo ambayo tunayo pale. Hivyo ni bajeti hii hii ndiyo itakayotatua changamoto hiyo. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna michango ya bajeti hii ambayo ilihusiana na viwanja vya ndege. Kwa mfano ilitolewa rai kuhusu kiwanja cha ndege cha Sumbawanga na vinginevyo. Tayari vile viwanja ambavyo vilikuwa vijengwe kwa ufadhili wa *European Investment Bank*, maongezi

yameshakamiliaka na sasa hivi tunasubiri wakati wowote waweze kutoa fedha ili vile viwanja vinne viweze kujengwa katika bajeti hii. Kwa hiyo tuna kila haja ya kuiunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kisera, bado nia ya Serikali kuunganisha mikoa yote kwa viwanja vyta ndege ipo pale pale hivyo tutaendelea kuviboresha viwanja vyote vyta mikoa na kuvijenga ili viweze kuendelea; na kwa sasa hivi viwanja vyote tunaviboresha katika kiwango cha kuviwekea taa ili viweze kufanya safari za usiku na tuweze kuongeza safari katika miundombinu ya viwanja hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo barabara nyingi ambazo Waheshimiwa Wabunge wameziongelea hapa na zote hizo ambazo tumezipanga katika bajeti hii tunaomba kupewe hiyo fursa ili tuweze kuzitekeleza katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda katika miundombinu ya reli, nikirudia pale, tuna reli ambazo tumepanga kuzifanya upembusi yakinifu ambazo ni Reli ya Tabora hadi Kigoma ambayo vile vile inakwenda kufanyiwa katika bajeti hii. Reli ya Kaliua - Mpanda hadi Karema nazo tutakamilisha kuzifanya upembusi yakinifu. Hivyo tukimaliza huo upembusi yakinifu kazi ambayo itafuata katika reli hizo ni ujenzi, na kazi zote hizo zimepangwa zitekelezwe katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Apika, huo ndio mchango wangu, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Ndalichako, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu ajiandae.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kukubali bajeti nzuri namna hii ije hapa Bungeni. Pia niwapongeze wapishi,

Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu Nchemba na Eng. Hamad Masauni kwa namna ambavyo walipika na hatimaye kutuletea hapa. Lakini pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Kamati ya Bajeti ambao walitoa maoni mazuri sana kuhusiana na bajeti hii; uchambuzi wao kwa kweli umejitoshela nami nawashukuru sana. Lakini niwashukuru pia Wabunge wote waliochangia hata wale ambao hawakuchangia lakini wametoa mawazo yao kwa namna moja ama nyine, lakini hasa wale ambao walichangia sekta ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hoja za Kamati, mojawapo ilikuwa ni Serikali iweke mazingira bora na kuhamasisha wananchi kufuga samaki. Suala hili la ufugaji wa samaki ni suala jipya. Tunakubali kwamba tutaendelea kufanya kazi hilo na Serikali tumejiandaa vizuri. Moja, tumeandaa miongozo mbalimbali inayoongoza suala lenyewe la ufugaji wa samaki, tuna miongozo ya namna ya kufuga au kutunza vifaranga; tuna miongozo ya namna ya kufuga samaki kwenye mabwawa; tunamiongozo ya namna ya kufuga samaki kwenye vizimba; na miongozo mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunajitayarisha vizuri kwa sababu wavuvi wetu hasa wanaotaka kufuga samaki kwenye vizimba wanapata shida hasa kwenye suala la *environmental impact assessment* Pamoja na *NEMC*. Sasa sisi tumesema tutagharamia na tutafanya kama Wizara, *strategic environmental assessment* kwenye maeneo ya upande hasa wa ziwa na bahari na maeneo yanayokubalika, halafu tutawajulisha wanaotaka kufuga samaki ili waweze kufuga samaki kwenye maeneo hayo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala hili la kufuga samaki pia tumesema tuanzishe vituo vipyta viwili, vitakavyowezesha wananchi wetu kujifunza. Tuna vituo vipyta vitano viko kule Lindi, Ruvuma, Mwamapuli pale Igunga, Kingorwila Morogoro na kule Chato na tumesema tunaongeza vituo vyangine viwili kule Mtwara na Dar es Salaam. Hivi vituo viwili vitakuwa ni *special*/kwa ajili ya watu wa mwambao, kwa sababu mfugaji wa samaki kwa vizimba

vyo mwambao na kule ziwani tofauti kidogo, kwa hiyo tumeona tuanzishe vituo viwili. Mwaka wa fedha unaokuja vituo hivyo vitafanya kazi na wananchi walioko kwenye maeneo hayo watakwenda kwenye vituo hivyo ili waweze kujifunza namna ya ufugaji bora wa samaki jinsi ulivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema vile vile tutaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa wafugaji wa samaki wa mabwawa na vizimba na maeneo mengine. Wataalam wetu wapo tayari kwenda na kutoa utaalalm, mafunzo ili kwamba suala hili liweze kueleweka vizuri na wananchi waweze kuchukua hii kama fursa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, suala la kufuga samaki ni suala rahisi sana na vijana amba wako huko wanajaribu kuangalia wafanye kazi gani, wanawea kuanza na hilli kwa sababu hilli ni eneo oevu sana na linaweza kuwapa kipato kizuri cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo Kamati walitushauri walisema Serikali iweke mazingira yatakayowezesha usafirishaji wa mazao ya uvuvi. Tumejitalidi sana kwenye eneo hili, moja ya jitihada tulizofanya ni kupunguza tozo. Tulisema kwenye bajeti yetu tulipokuwa tunasoma hapa, tumeponguzza tozo za aina mbalimbali ambazo tulizitaja kwenye bajeti yetu, sipendi kuzirudia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo tulilizungumza na Kamati, ni Serikali iendelete mapambano dhidi ya uvuvi haramu na kudhibiti utoroshaji wa mazao ya uvuvi, suala hili ni suala endelevu. Naomba Waheshimiwa Wabunge waelewe na wananchi ewelete kwamba, uvuvi haramu haukulaliki kwa namna yoyote ile. Tunaendelea nalo lakini kwa namna ambayo itakuwa ni shirkishi zaidi. Tumezitayarisha halmashauri zetu pamoja Kamati za Ulinzi za Wilaya na za Mikoa, ili zishiriki kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili lilikuwa likichukuliwa kama ni suala la ngazi ya Wizara peke yake, lakini safari hii tunatakata twende pamoja kama Serikali moja.

Kwa hiyo ndio maana mtaanza kuona Wakuu wa Wilaya wanasaka makokolo na Wakuu wa Mikoa wanatafuta wavuvi haramu na kuwapa adhabu kwa mujibu wa sheria. Sasa tunataka Serikali kwa ujumla tulivalie njuga suala hili ili ijulikane kwamba ulinzi wa rasilimali za mazao ya samaki ni wetu sisi wote. (*Makofo*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye masuala ya mifugo. Kamati walitushauri kwamba jitihada zaidi ziongezwe kupambana na magonjwa ya mifugo, hili ni suala ambalo pia ni endelevu, sisi tunaendelea kama Wizara. Moja tunajengea uwezo kituo chetu kinachozaalisha chanji cha *TV*/kipo pale Kibaha, tumetenga kiasi cha shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya kuzalisha chanjo zaidi. Pia Wizara tumetenga kiasi cha shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya kujenga majosho katika maeneo ya wafugaji, hasa maeneo ambayo mifugo yetu mingi ipo. Kwa hiyo, tutajenga majosho kwenye maeneo ya Waheshimiwa Wabunge ili tujaribu kupunguza namna za magonjwa zinazosababishwa na kutoogesha mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tutanunua dawa za kuogesha hiyo mifugo. Tumetenga pesa kiwango fulani na tutafanya ukarabati wa *clinic* zetu mahali popote zilipo, tumetenga kiasi cha pesa kwenye bajeti yetu ili kwamba tuhakikishe angalau tuna *clinic* za mifugo kwenye maeneo yetu kuweza kutibu mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tumesema tutalifanya ni suala linalohusiana na mambo ya ugani. Kamati ilitushauri kwamba tuweke mazingira wezeshaji ya ufanyaji kazi kwa Maafisa Mifugo ili waweze kuzungukia mashamba na mifugo. Tulisema pia kwenye bajeti yetu, kwamba kwenye bajeti hii tumetenga kiasi cha pesa tutanunua pipipiki 300, kwa ajili ya Maafisa Mifugo ili waweze kutembea na kuwafikia wafugaji popote watakapokuwa. Mbali ya kuwanunulia vifaa hivi, pia tutafanya mafunzo rejea kwa ajili ya maafisa hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yaliyozungumzwa na ushauri uliotolewa ni mwinci. Niseme tu kwamba ushauri wote na hoja zilizotolewa tumezichukua tutazijibu kwa

maandishi, ziko nyingi; kuna bajeti ya mifugo na uvuvi ni ndogo tumechukua, naomba tu watupe nafasi kwa bajeti hii tuliopewa waone tunafanya nini kwa mwaka ujao na si sasa hawatakuwa na sababu za kumdati Mheshimiwa Rais kutoongezea bajeti baada ya kufanya kazi ambazo tumepangia mwaka huu watakapotupitishia bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusafirisha na kuuza mazao ya mifugo na samaki bado kweli ni kidogo tunakubali na tunataka tuongeze sasa uzalishaji kwenye sekta hizi zote mbili. Utagundua kwamba kazi zote tulizozitenga kuzifanya zinalenga kuogeza tija na uzalishaji kwenye masuala haya mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ulinzi na usalama kwa wavuvi na wafugaji. Suala hili linaihusu Serikali nzima na tutashirikiana na Kamati za Ulinzi za Wilaya na za Mikoa ili tuhakikishe ya kwamba wavuvi wanapokuwa baharini au wanapokuwa kule ziwani, wako salama na vifaa vyao na vyombo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine la miundombini ya mifugo, nimetaja baadhi. Pia lipo suala la mchango wa uvuvi kwenye pato la Taifa. Nadhani hili litaelezwa kwa kirefu sana na litaongelewa vizuri zaidi naMheshimiwa Waziri au Naibu Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu zao la mwani ambalo linastawi kwenye mwambao wa pwani kuanzia Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Pwani kwenda mpaka Tanga. Suala hili tumelichukua vizuri na sisi kwenye bajeti ijayo tumetenga pesa mahususi kwa ajili ya zao la mwani kuhusiana na uzalishaji wake, soko lake na kuhusiana hasa akinamama wanaozalisha suala hili tuwatafutie vifaa vinavyoweza kuvuna zao hili kwa wingi. Kwa hiyo suala hili pia tumeliwekea maanani sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna suala la Ranchi za Taifa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa nakupa dakika moja, malizia Ranchi za Taifa.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Ranchi za Taifa, tumelichukua na najua Waheshimiwa Wabunge hapo walishauri sana juu suala hili, lakini hata kwenye hoja hii limezungumzwa sana, tumelichukua na tunafanya tathmini, wategemee *transformation* kubwa kwenye Ranchi zetu za Taifa. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, Waziri wa Elimu Sayansi na Technolojia, atafuatiwa na Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi ajiandae.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii ya Serikali ambayo ni bajeti ya Serikali. Kwanza nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii, kwa sababu bajeti hii ya Serikali, ni bajeti ambayo inakwenda kuimarisha Sekta ya Elimu, ni bajeti ambayo inakwenda kutatua changamoto zilizopo katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana na hatua ya Serikali kuongeza vyanzo vya kuboresha barabara vijijini, kwa sababu barabara zinapokuwa mbovu hata Wizara ya Elimu tunapata shida kupeleka mitihani. Kwa hiyo barabara zikiwa nzuri hata Walimu wanapokuwa wanakwenda kwenye shughuli za kufanya kazi mjini kama wana shida au wanaenda kikazi itawarahishia ili kurudi mapema kufundisha. Pia suala la maji na umeme, ni muhimu ili elimu iende vizuri. Kwa hiyo naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa sababu mambo haya yamekwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii pia kwa sababu kwanza imeimarisha hata mikopo, naona hata vijana wangu wapo hapa, mikopo kwa fedha zilizotengwa mwaka 2020/2021ilikuwa ni shilingi bilioni 464, lakini katika bajeti ya Wizara yangu iliyopita zipo bilioni 500, zilizopita ziliikuwa bilioni 464 na mwaka unaokuja ni bilioni 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wakipitisha mapendekezo haya ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameyaleta, tutaweza pia kupata fedha nyingine za nyongeza katika Bodi ya Mikopo. Haya ndiyo yamenifanya niweze kuunga mkono hoja hii na nawasihi Waheshimiwa Wabunge waiunge mkono ili vijana wetu waendelee kusoma. Pia kwa wale ambao hawana uwezo wa kujikimu, basi Serikali iweze kuongeza wigo na tupunguze zile kelele za wanafunzi ambao wanakuwa na sifa wanadahiliwa na wakati mwingine wanakuwa wanakosa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda kuchangia baadhi tu ya maeneo machache ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge katika hoja hii. Kwanza niongelee suala la ujuzi, Waheshimiwa Wabunge wameendelea kusisitiza kwamba elimu yetu iwe kwa vitendo zaidi, ijenge ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikwambie kwamba suala hilo tayari, hata kwenye hotuba ya bajeti yangu nimeshaliweka, lakini ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ameshatoa maelekezo kwa Wizara ya Elimu na tayari tumeanza mapitio, mliuona Mlimani City tarehe 18 Juni, tulikaribisha wadau wa elimu ambao wametupa maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunapokea maoni kwa kuititia njia ya kimtandao *google drive* ambayo mpaka jana mchana tulikuwa na wananchi 1,152 ambao walikuwa wametoa maoni kwa njia ya mtandao. Kwa hiyo tutaeendelea maoni na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutafanya kazi na wasikose kuendelea kutupatia maoni na tutapanga muda mahsusii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tumpanga tuwe na mjadala Dodoma tarehe 26 Jumamosi, lakini Wizara ya Uwekezaji na Ofisi ya Waziri Mkuu tayari wana jambo lao, Kongamano la Vijana. Kwa hiyo tutaangalia kwa sababu yote ni mambo Serikali, hatuwezi tukaweka mambo mawili kwa wakati mmoja ili kuweza kuruhusu ushiriki kikamilifu kwa sababu masuala yote ni muhimu, lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaendelea kuwashirikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine ambalo limezungumziwa kuhusiana na suala la watoto kubaki shulenii wakati wa likizo. Huwa ni msikivu sana na huwa najiuia kumpa Mheshimiwa Mbunge mwenzangu taarifa anapoongea, lakini leo kidogo jinsi liliivoletwa na nikasikia kama mama, nasikia hata kauchungu fulani, Mheshimiwa anavyosema kwamba kuna baadhi ya shule wanawacha watoto shulenii, hakuna mabweni, wanafunzi wanalazwa kwenye sakafu kwenye majani. Hiyo hapana, hiyo sio sawa na Serikali haiwezi kuruhusu jambo kama hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mfumo wa kwenda likizo kwa sababu tunaamini kwamba akili ya binadamu inachoka. Wanafunzi wanahitaji kupumzika, kukaa na familia zao na kufanya shughuli za nyumbani, maana akikaa shulenii tu kila wakati, mazingira pia mengine wanakuwa hawawezi kuyafanya. Nikitoa mfano wa wanafunzi wa kidato cha nne, wamefungua shule January, 13. Wataanza mitihani yao ya kumaliza kidato cha nne, tarehe 14 mwezi Novemba. Sasa mtoto yupo tangu January unamwambia mwezi Juni asiende nyumbani akae shulenii mpaka Disemba ndio anamaliza mitihani tarehe 13 Desemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama Serikali tunaona kwamba likizo kwa wanafunzi ni muhimu. Kwa sababu suala la mjadala wa elimu lipo mezani, tumeshafungua pazia, tunapokea maoni ya wadau na hili suala la likizo ya wanafunzi ambao wapo kwenye mitihani, tulipitie ili tuone kama kweli tumefika mahali ambapo tunaona kwamba Serikali itoe waraka ili ifute hizo likizo. Kwa

sasa tunatekeleza nyaraka ambazo zipo na nyaraka ambazo zipo ndio zinavyoelekeza, wanafunzi wapate na muda wa kupumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba, utaratibu pia unaowekwa na shule ambazo zinawabakiza watoto shulenii unakuwa pia mwingine siyo sawa, kwa sababu inakuwa kama ni dharura, wazazi inakuwa kamata kamata, lazima walete hela na mzazi asipoleta mtoto inakuwa ni shida. Sasa kipindi cha likizo ni kipindi cha kupumzika, isiwe ni lazima kwa mzazi ambaye labda anaenda likizo anataka mtoto wake aende naye, anaambiwa lazima abaki shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuzikumbusha shule za Serikali, Serikali inatoa elimu bila malipo, sasa hili la kuwabakisha wanafunzi wakati wa likizo limekuwa ni uchochoro wa kuongeza gharama. Gharama zinazotozwa wakati wa likizo zinaanzia Sh.5,000 mpaka Sh.250,000 kwa mwezi mmoja. Kwa hiyo sasa ni namna ambavyo gharama za elimu zinarudishwa kwa njia nyiningi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe Maafisa Elimu wa Mikoa wote na Maafisa Elimu Wilaya kuzingatia waraka wa elimu namba tatu wa mwaka 2016, ambapo umeelekeza bayana kwamba Serikali inatoa elimu bila malipo na kama kuna ulazima wa kuwachangisha wanafunzi michango ya aina yoyote, Waraka Na.3 wa mwaka 2016 unaelekeza utaratibu unaopaswa kufuatwa. Kwa hiyo wazingatie utaratibu huo, vinginevyo Maafisa Elimu, kwa sababu sehemu tumefuatilia sehemu nyngi shule zinafungwa kwa maelekezo ya Afisa Elimu, Waziri wa TAMISEMI ambaye ndiye anasimamia shule hana taarifa, Waziri wa Elimu hana taarifa, kwa hivyo Maafisa Elimu acheni kupoka mamlaka ya kuweka sera.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyngi za Serikali zimeanza huu mtindo, hata madarasa mengine yasiyokuwa ya mitihani wanaambiwa wasiende shule. Leo nimepata malalamiko kwa mfano Kagera, kuna shule moja, mpaka wanafunzi wa elimu ya awali wanaambiwa wasiende likizo.

Hiyo hapana, inakuwa *too much* sio tu masuala ya mitihani, yaani wanasema mafunzo rekebishi na kila mwanafunzi anayekwenda shule hata huyo mwanafunzi wa elimu wa awali, anatakiwa alipe. Kwa hiyo ukiliftafakari kwa undani, kuna baadhi ya shule, Serikali inatoa elimu bila malipo, lakini wao wameamua kurudisha gharama kwa kivuli cha kwamba wanaandaa wanafunzi. Tumetunga mtaala wetu, tunaamini kwamba siku 194 za masomo zinatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu ng'ombe hanenepeshwi siku ya mnada, mwanafunzi amekuwa shulenii miaka saba, darasa la kwanza, la pili kwa nini nguvu anayotumia mwanafunzi akiwa kwenye darasa la mitihani wasitumie miaka yote mwanafunzi anapokuwa shulenii? Kama hakuandaliwa vizuri kwa miaka saba jinsi mitaala yetu ilivyoadaliwa, haiwezekani kwa mwaka mmoja ukamshindilia mtoto, mambo ambayo alipaswa kusoma kwa miaka saba, huyu mtoto akawenza kuelewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kuwashindilia watoto mwaka wa mwisho, unataka mambo ambayo walitakiwa kuwafundisha miaka saba, ayasome kwa mwaka mmoja, wengine ndio maana wakiingia kwenye vyumba vya mitihani wanwakuwa wamechanganikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, naomba sana Waheshimiwa Wabunge, Serikali imelipokea suala hili na kwa sababu linaonekana ni tatizo tuna malalamiko mengi sana kutoka kwa wazazi. Shule binafsi nyingine zina utaratibu mzuri tangu kwenye *joining instruction* wanakuwa wameonesha na inakuwa ni sehemu ya ada zao, lakini kuna shule nyingine zinakuwa zinawashtukiza wazazi tu dakika ya mwisho mwanafunzi anatakiwa kuja, inakuwa kama dharura kwamba hawatakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nadhani suala hili kama Serikali kwa sababu tumeshaiona hiyo changamoto, Waheshimiwa Wabunge tunapokea maoni kuhusiana na mitaala. Hata hivyo, suala hili lenyewe, tutalichukua na

kwenda kulifanyia kazi na hasa hizi shule za Serikali, tutakwenda kufanya ukaguzi kwa sababu kuna shule za msingi kwenda mwanafunzi kusoma wiki tatu anatakiwa alipe Sh. 85,000/= shule ya Serikali. Hii sio sawa, msimamo wa Serikali kutoa elimu bila malipo upo pale pale, tutaendelea kutoa elimu bila malipo bila ya kuingiza gharama kwa kutumia kivuli kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu ya juu, ni wahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba bajeti hii inakwenda kuimarisha miundombinu katika elimu ya juu, inakwenda kuhakikisha kwamba tunaongeza idadi ya wanafunzi ambao wanajunga na elimu ya juu kwa sababu kutokana na elimu bila malipo, ongezeko la wanafunzi Shule za Msingi na Sekondari ni kubwa. Kwa hiyo, tunaandaa mazingira sasa ya kuwapokea watakapokwenda Vyuo Vikuu. Kwa hiyo, tutakuwa na ujenzi wa miundombinu, kutakuwa na kutoa ufadhili wa wahadhiri wetu ili waweze kupata shahada za uzamivu na tuweze kuandaa walimu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tutaimarisha sana mafunzo kwa vitendo. Hapa ni endeleo kuwasishi Wakuu wa Vyuo, Taasisi za Elimu ya Juu kuweka ushirikiano mzuri na sekta binafsi pamoja na viwanda ili kuweza kupata sehemu za kufanya mafunzo kwa wanafunzi wetu wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii kwa sababu hakika inakwenda kuimarisha elimu yetu. Nashukuru sana kwa nafasi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nadhani umeeleza hapo kwamba kama Serikali mnapokea mawazo kipindi hiki kwa ajili ya mitaala. Ila ukiacha hayo yaliyopitiliza ya shule sijui ya awali, ama madarasa yasiyo na mitihani, nadhani hoja mojawapo iliyotolewa ni baadhi ya shule kutokuwa na walimu wa masomo fulani. Kwa hiyo, wakawa wanahitaji pengine kuwaweka wanafunzi sehemu ili walimu hao ambao hawana kipindi cha kawaida waweze sasa kuwafundisha wawe tayari kwa ajili ya mitihani.

Kwa hiyo, nadhani ni jambo ambalo inabidi mitazame katika kipindi hiki chote, kwa sababu hoja yako ya kunenepesha ng'ombe wakati wa mnada ni kweli, lakini, sasa kusoma tunafahamu, wengine lazima watumie msuli sana, wengine kidogo na pia kwa ajili ya kuondoa ule utofauti unaokuwepo sana kati ya ufaulu wa shule za sekondari za Serikali na za binafsi. Kwa sababu tukizikataza shule za sekondari za Serikali halafu shule za binafsi zikaendelea na utaratibu wake, ule utofauti bado utaendelea kuwa mkubwa. Kwa hiyo, nafikiri ni jambo la kulitazama kama ambavyo umesema kwamba mtakuwa mnaliangalia. (*Makof!*)

Pia hizi ajira ambazo zimetangazwa, nadhani zitapunguza ule uzito kwenye hizi shule, kwa sababu tunaweza tukafika mahali sasa walimu wakaona sasa ah, kwani akifeli mimi nina adhabu gani? Mimi bado niko shulenii. Kwa hiyo, tujaribu kuziangalia pande zote mbili ili watoto wetu wafanye vizuri. Tunataka watoto wetu wafaulu.

Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI atafuatiwa na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalam wote kwa kuandaa bajeti nzuri ambayo kwa kweli inakwenda kutatua changamoto katika maeneo yetu katika ngazi za Vitongoji, Vijiji, Kata, Halmashauri na Wilaya. Kwa hiyo, katika hatua hii nasema naunga mkono hoja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri ambaa mmetupatia katika maeneo mbalimbali ikiwemo kuboresha elimu msingi na sekondari, kuboresha huduma za afya ya msingi katika zahanati, vituo vya afya na Hospitali za

Halmashauri. Ushauri mzuri mmetupatia kwa ajili ya kuboresha barabara za vijiji na mijini kupitia *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumepokea ushauri wenu Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuimarisha Utawala Bora ikiwemo usimamizi wa rasilimali fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Waheshimiwa Wabunge, tunawashukuru sana na tunawaahidi kwamba tutafanya kazi ushauri wenu na tutatoa taarifa kupitia kwenu kupitia Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu mambo makubwa matatu au manne. Jambo la kwanza, Waheshimiwa Wabunge tumepokea ushauri wenu. Kwanza tunapokea pongezi kwa Serikali kupitia Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan ya kuamua kubeba mzigo wa posho za kila mwezi za Madiwani kulipwa na Serikali Kuu. Pia tumepokea maoni yenu kwamba sasa kile ambacho kitaokolewa kiende kikalipe fedha au posho kwa Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linatakiwa kufanya uchambuzi, lakini tumeona mahesabu ya haraka haraka, tunaweza tukapata *savings*. Mheshimiwa *Comrade* Mkuchika katika Halmashauri yake ya Mji wa Newala wana Madiwani 22. Kwa hiyo, Madiwani wa Kata ni 16 na wengine ni wa Viti Maalum. Kwa hiyo, kama wangalipa Halmashauri, ni kama shilingi milioni 7.3. Kwa sababu Serikali inabeba huu mzigo; na kwa sababu pia tumeelekeza ile shilingi 100,000 angalau ikalipe posho za watendaji wa Kata, kwa hiyo, ukitoa shilingi milioni 7.3 na shilingi milioni 1.6, Halmashauri itabakiwa au ita-save shilingi milioni 5.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, inawezekana kabisa kuwapa hata hela kidogo; shilingi 20,000 ya kuweza kuwasaidia. Kwa hiyo, hili Waheshimiwa Wabunge tumelipokea na tutalifanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu miradi ya kimkakati inayotekelizwa katika Halmashauri zetu hususan masoko

yamejengwa au stendi ambayo hayaleti tija au yamekuwa ni kero katika baadhi ya Halmashauri. Tumepata ushauri kutoka kwenye Kamati ya Bajeti inayoongozwa na *Comrade Sillo*; tumepata ushauri kutoka Kamati ya TAMISEMI inayoongozwa na *Comrade Polepole*. Kwa hiyo, tutafanya mapitio ya utekelezaji wa miradi yote ya kimkakati. Waheshimiwa Wabunge mtashiriki kuamua miradi hii katika majimbo yenu iende ikatatue kero gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Watanzania hawataki soko la ghorofa, wanataka *simple* soko. Kuna *roofing*, chini kuna *floor* nzuri, lakini pia ina maeneo mazuri. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, haya tutayashirikisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni *TARURA*. Tunawapongeza na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kueleza kilio chenu kuhusu ubovu wa miundombinu ya barabara katika majimbo yenu na Halmashauri zenu. Ni kweli, *TARURA* imeanzishwa chini ya Sheria Na. 13 ya 2007 na *TARURA* inafanya kazi kwa mujibu wa sheria ndani ya Tanzania Bara. Kwa hiyo, mtandao ambao *TARURA* unahudumia ni kama zenye urefu wa kilometra 100,008.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna utafiti, barabara za lami ni asilimia 2.1, barabara za changarawe ni asilimia 25 na barabara za udongo ni asilimia 72. Kwa hiyo, kwa kweli kilio cha ubovu wa barabara ni kikubwa. Kulikuwa na mvua, kwa hiyo, pia imefanya barabara zetu nyingi hazipitiki na ukiangalia hali ya barabara ni asilimia 23 tu ya barabara zetu kwa mujibu wa Taarifa ambazo ninazo ndiyo ziko katika hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumesikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge. Namshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Fedha, kwamba sambamba na fedha ambayo tunaipata kuititia Mfuko wa Barabara Mheshimiwa Waziri Chamuriho ameeleza, kuna fedha angalau Hazina walitutengea kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya

barabara. Ndiyo maana katika ile dhamira ya Mheshimiwa Rais Samia ya kuwashirikisha Wabunge, tukasema badala ya kuwaachia wataalam waamue fedha hizi ziende wapi, tukaona kila Mbunge tutende haki na usawa kwa kila jimbo, shilingi milioni 500. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze, ninaposema kila jimbo, ni jimbo ndani ya Tanzania Bara kwa sababu *TARURA* kwa mujibu wa sheria inafanya kazi ndani ya Tanzania Bara. Kwa hiyo, naomba niweke vizuri hili. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge shilingi milioni 500 siyo nyingi lakini tunaamini inaweza kuleta mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kesho Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ana mambo mazuri zaidi anakuja nayo. Mapendekezo yetu Waheshimiwa Wabunge, kwenye nyongeza hili ambayo tutapata kutoka Hazina, Wabunge wa Dar es Salaam mnisamehe, mtapata *DMDP II*. Kwa hiyo, hatutawaingiza kwenye fedha itakayoongeza, kwenye hela ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kuna miji 45 tunategemea itapata fedha kupitia mradi wa *TACT/Cs*. Kwa hiyo, tutawoandoa pia kwenye fedha hizi amba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu atatupa. Kwa hiyo, Wabunge tunaamini badala ya shilingi milioni 500 mnawenza mkajikuta mnaondoka hata na 2B. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namsafishia njia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. Kwa hiyo, mambo mazuri tutayasikia kesho. Wabunge wa Dar es Salaam *DMDP II*, mambo mazuri; Wabunge wa Majiji 45, Mheshimiwa Naibu Spika, nawe ni mnufaika. Mambo pia yanakuja vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne ni la kuboresha miundombinu ya elimu msingi na sekondari. Waheshimiwa Wabunge tumpokea ushauri wenu lakini kubwa zile shilingi milioni 600 tunawaomba sana, tunataka shule iliyokamilika, yenye madarasa nane, yenye vyumba vyaya maabara vitatu. Yenye nyumba mbili za walimu; *two in one* na yenye vyoo.

Kwa hiyo, mnaposema tuwagawie kidogo kidogo, Waheshimiwa Wabunge tunaomba sana, hebu tufanye kitu *complete* kipendeze katika majimbo yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwapa siri nyingine, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kesho anakuja na mambo mazuri zaidi. Tutatoa fedha za kujenga madarasa haya mawili mawili, manne manne katika shule zenu zaidi ya 10 au nne katika majimbo yenu. Kwa hiyo, haya tunawaomba sana, shilingi milioni 600 hii ikatumike kufanya kazi iliyokusudiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dada yangu Mheshimiwa Prof. Ndalichako tunafanya kazi nzuri na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. Tuna *network*, tuachieni, tutawatafutia fedha chini ya Rais Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kujenga miundombinu ya elimu, miundombinu ya afya na pia miundombinu ya afya katika Halmashauri zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona hili nilitolee ufanuzi. Kwa hiyo, tunaomba shilingi milioni 600 ile msiende kuikata kidogo kidogo. Nami nimeshawaambia watu wangu, kama tunampa Mbunge kwenda kuongeza madarasa, lisiwe chini ya madarasa mawili. Kwa hiyo, kila Mbunge kama atapata, angalau madarasa mawili, matatu au manne kwa ajili ya shule za msingi na sekondari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulisisitiza samahani sana Waheshimiwa Wabunge; sambamba na fedha ambazo tutazitoa kutoka Serikali Kuu nataka nikiri katika miezi miwili ambayo nimekuwa Waziri wa TAMISEMI, kuna ubadhirifu au matumizi mabaya ya fedha za Serikali katika Halmashauri zetu. Fedha zinapigwa ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge. Baadhi ya Halmashauri hawajali. Tukiwabana Halmashauri; nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, nasi sote ni Wajumbe wa Kamati za Fedha; wewe uliza, nataka kuona asilimia yangu 40 ambayo itaenda kutatua kero za ndugu yangu pale Jimbo la Tandahimba, kaka yangu. Kwa hiyo, mnatakiwa mkikaa, usikubali tu wakiwaambia ukarabati, sijui kumalizia, ndiyo

wanapiga fedha. Mwulize umekarabati kitu gani? Umekarabati msingi? Umepiga rangi? Umeweke bati? Umeweke dari? Au umeweke *floor chini?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge bila kupepesa macho, tunazo fedha siyo nyingi, lakini zinaweza kwenda kutatua kero za wananchi wetu katika elimu na afya. Pia kuna Halmashauri zinapata zaidi ya shilingi bilioni 500. Waheshimiwa Wabunge, siyo vibaya kuweka bilioni moja kwenda kupiga kilometa mbili za lami katika Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu Mheshimiwa Tarimba nadhani anafahamu, Kinondoni wanapata shilingi bilioni 33, wanatakiwa kupeleka kwenye maendeleo shilingi bilioni 19 kwa mwaka mmoja. Mheshimiwa Gwajima, ninyi sio masikini, yaani mna uwezo wa kupiga sekondari mbili za ghorofa kila mwaka za shilingi bilioni mbili mbili. Mna uwezo wa kupiga vituo vya afya viwili vya ghorofa kila mwaka, shilingi bilioni mbili mbili; kwa Mheshimiwa Gwajima na Kinondoni. Nawaomba sana tushiriki kuwasimamia Halmashauri zetu. Nasi tutajitahidi kuwapitia Waweka Hazina wa Halmashauri wote. Mama akishamaliza kuteua Wakurugenzi, tunaenda kufanya mapitio ya Waweka Hazina wote, lakini pia tunaenda kufanya mapitio ya Maafisa Mipango wote. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kengele ya pili. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na Mwenyezi Mungu awabariki. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Sasa ningeweza kumpa nusu saa, lakini inavyoonekana atamaliza makofi ya kesho ya Mheshimiwa

Dkt. Mwigulu, naye amesema hataki kuongea mengi leo. Kwa hiyo, pale ndiyo amemaliza aliyotaka kusema. (*Makofi/Kicheko*)

Ahsante sana Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu kwa taarifa nzuri zinazotia moyo Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wawakilishi wa Wananchi. Kwa hiyo, tunaamini huko nje wananchi nao wanafurahi kama wawakilishi wao wanavyofurahi.

Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa muda huu niliopewa kuchangia hoja hii kuu ya Wizara ya Fedha. Kabla sijasema yangu machache nami niseme nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu kwa kazi nyingi, kwa muda mfupi usiozidi siku 100 ambao tumeshuhudia. Tumeshuhudia maelekezo, tumeshuhudia kazi, tumeshuhudia na mfumo mpya wa utendaji wa kazi na tumeshuhudia na kasi mpya ya utendaji wa kazi. Kwa hiyo, nami nampongeza sana, angalau katika siku hizi ambazo hazizidi 100 ambazo amekaa madarakani wananchi tumepeata matumaini makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepeata matumaini na mengi Waheshimiwa Wabunge mnayaona hata humu kuitia Bungeni. Yapo mambo mapya ambayo tulikuwa hatujashuhudia, mnayaona. Haya makofi mengi ya Mheshimiwa Waziri Ummy ni matumaini mapya ambayo yamekuja na utaratibu mpya. Bajeti ni ile ile, pesa ni zile zile, lakini huu ni ubunifu mpya wa namna ya kusimamia na matumizi mazuri. Kwa hiyo, haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita katika siku zisizozidi 100. Sasa fikiria tukifika mpaka 2025, Mheshimiwa Ummy atasema maneno mangapi huyu? Tunajua yako mengi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunampongeza. Kwetu sisi tulioko wote, maana ni Wabunge wote tuna

matumaini makubwa kutokana na mageuzi makubwa anayoyafanya. Nami nimepewa shilingi milioni 500 zile barabara, nimeelekeza zitumike kwenye barabara zangu. Haya ni mapinduzi makubwa kwamba sasa na Wabunge tunashiriki katika kupanga miradi ya maendeleo. Yaani tunashiriki kupeleka pesa na kusimamia pesa tuliyopeleka wenyewe kwa maelekezo ya barabara na miradi tunayoitaka. Tumeulizwa hapa habari ya shule tunazotaka zipelekewe pesa, Wabunge wote tumechagua shule. Ni mapinduzi makubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda sana kupongeza haya, yatatupa ule usimamizi wa karibu ambao tulikuwa tumepewaa kwenye Katiba, sasa tunapewaa kiuhalisia kwamba kuna upangaji wa bajeti unaokwenda kwenye milango ya Serikali na mwininge upande wa jimbo tunakwenda kusimamia. Kwa hiyo, napongeza sana juhudii hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wizara ya Ardhi ni Sekta wezeshi. Katika miradi yote inayopangwa humu ndani, yote inatekelezwa kwenye ardhi. Kazi kubwa na maelekezo makubwa tuliyopewa na Mheshimiwa Rais ni kupunguza urasimu katika upatikanaji wa ardhi katika kutekeleza yote yanayopangwa hapa hasa ya uwekezaji. Tumeshuhudia katika kipindi hiki cha siku zisizopungua 100 Mheshimiwa Rais kwa kutumia madaraka ya kisheria aliyopewa ameweza kufuta mashamba yasiyopungua 11 yenyekarini ya zaidi ya 24,119. Mashamba haya yamefutwa kwa sababu yalikuwa hayaendelezwi vizuri. Haya mashamba yako kila mahali, hata Waheshimiwa Wabunge mlipokuwa mnachangia sehemu nyingine, mnayaita mashamba pori. Kwa hiyo, ni fursa Waheshimiwa Wabunge, kama kuna mashamba kama haya watu wanamiliki sehemu mbalimbali lakini mnayaona kwa macho hayaendelezwi, tuambizane kutoka huko huko ili tuchukue hatua za kisheria tuyafute ili waweze kupewa watu wengine wenye uwezo wa kuyaendeleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mashamba haya ameelekeza sehemu wagawiwe wananchi ambao hawana

ardhi ya kutosha na sehemu tumehifadhi kwa ajili ya uwekezaji. Pia tulikuwa na mashamba yenyekari 45,788 ambayo yalifutwa siku nyingi lakini maelekezo ya namna ya kutumia yalikuwa yatoke kwa Mheshimiwa Rais na yalikuwa hayajatolewa. Mama ametoa maamuzi kwamba mashamba haya angalau ekari 33,672 kati ya ekari 45,000 wagawiwe wananchi wayatumie na sehemu iliyobaki ya ekari 15,000 ziwekwe kwa ajili ya uwekezaji kuititia taasisi ambazo zinasimamia uwekezaji za EPZA na TIC, kulima mashamba ya katani, kujenga viwanda na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumeshuhudia katika kipindi hiki cha siku zisizozidi 100 uwekezaji maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji yamekuwa makubwa sana. mpaka tarehe 01 mwezi wa sita ofisi yangu imeshapokea maombi 305 ya watu wawekezaji mbalimbali wanaokuja kutaka ardhi kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali. Na kati ya hayo, kama nilivyosema juzi, sasa tumeanza kukaa Kamati ya Kitaifa ya Ugawajji wa Ardhi inakutana kila wiki kwa hiyo, katika maombi 305, mia tatu na tatu yameshapewa majibu na wawekezaji wameshapewa ardhi ya uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji huu tunakwenda kushuhudia Morogoro kuna uwekezaji mkubwa wa kiwanda cha sukari. Kigoma kuna watu wameomba kwa ajili ya viwanda vya sukari, lakini Kilwa kule kuna kampuni kubwa zinakuja kulima mihogo, lakini yanaweka viwanda vya kuchakata mihogo kwa soko la China kwa ajili ya kununua vilevile mihogo inayolimwa katika Mikoa ya Kusini, lakini hapa Kibaha tumeshuhudia kampuni zimeanza kuomba sasa maeneo ya *industrial park*. Iko kampuni moja ambayo imepewa ekari 1,000 na imeahidi itawekeza viwanda 73 katika hiyo *industrial park*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hayani mambo yanayotokea ndani ya siku zisizozidi 100 kwa hiyo, uwekezaji nao unaenda kwa kasi. Na sisi kama sekta wezeshi tunaahidi mbele yenu Bungeni hapa, tunamuahidi Mheshimiwa Rais kwamba, tutatimiza wajibu wetu, tutaondoa urasimu na

kuhakikisha uwekezaji unakuwa wa tija katika nchi hii, hasa katika matumizi ya ardhi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ardhi hii imetengwa mikoa yote. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wakuu wa Miko ana Wakuu wa Wilaya wametenga ardhi za kutosha na halmashauri, kama mamlaka za upangaji ziko huko. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia wawekezaji wote Tanzania ni salama kwa uwekezaji na ardhi ya kuwekeza ipo. Mtu yejote ambaye anafikiri nataka kuwekeza, kujenga majengo, kujenga viwanda, ardhi ipo; kokote kule kama wakikusumbua tuonane huko wizarani sisi tunajua ardhi ilipo mahali popote katika nchi hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho, ndani ya Bunge hili tumeshuhudia Waheshimiwa Wabunge mjisema gharama za umillikishaji ni kubwa na wengi mlikuwa mnaitaja tozo ya *premium*. Kama walivyosema Wabunge wengine, inaelekeea Mheshimiwa Rais huwa anasikiliza kule, leo tumemsikia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ametangaza hapa kwamba toso ya asilimia mbili na nusu kwa kila anayemiliki ardhi kwa mara ya kwanza ya thamani ya ardhi sasa imepunguzwa na inakuwa 0.5. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake nini? Hawa wote wawekezaji ambao tumewapa ardhi zaidi ya 303 wangepaswa kulipa asilimia 2.5 ya thamani ya ardhi na hii si kodi ni tozo. Na wote hawa kila anayemiliki kiwanja, hata urasimishaji wakipata *invoice* wanamfuata Waziri awapunguzie, nilikuwa nawapunguzia, lakini je, mtu wa Kigoma atamuona Waziri? Je, mtu wa Kilosa kule atakuja kwa waziri?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo Mheshimiwa Rais ameleta tiba kwamba, wote wanaomiliki ardhi kwa mara ya kwanza wamilikishwe kwa tozo ya 0.5 yaani nusu ya asilimia moja. Kwa hiyo, hii itaongeza ari ya uwekezaji, lakini na wananchi masikini ambao wanataka kumiliki ardhi zao kwa kupata hati, hasa katika zoezi la urasimishaji. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini nampongeza

sana rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwa hotuba yake nzuri sana ambayo ameisoma hapa ambayo imewezesha tozo hii kupunguzwa kutoka asilimia 2.5. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi nilivyosikia mazungumzo ya Waheshimiwa Wabunge wengi naona tozo hii mmeikubali kwamba, ipungue. Na pengine tunavyoendelea inaweza ikafutwa kabisa kwa sababu, hii sio kodi ni tozo. Kodi za msingi za umilikaji zipo na mtu akimiliki ardhi kwa mara ya kwanza maana yake anakuwa mlipa kodi wa kila mwaka kwa miaka 99. Kwa hiyo, ni vizuri mtu amiliki kwa gharama ndogo kwa sababu bado anatupa japo kidogo kidogo, lakini kwa miaka 99. Hawa ni walipa kodi wa kudumu wa uhakika, yaani akinunua shati maana yake atalilipia kodi kwa miaka 99, akipewa hati miliki maana yake huyo anaingia kwenye daftari la ulipa kodi la Serikali kwa miaka 99. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huu ni mwanzo mzuri. Nafikiri tukiona inaenda vizuri mwaka huu tunaamini hata mapato yatokanayo na kodi ya ardhi yataongezeka kwa sababu, leo tuna viwanja laki tisa ambavyo tumevipima, lakini watu hawajachukua hati kutokana na tozo hiyo. Kwa michoro ya *survey* ambayo inaonesha viwanja mbalimbali vilivyopimwa nchi hii kwa urasimishaji na viwanja na mashamba tunayo michoro ya viwanja elfu tisa ambavyo vimepimwa, lakini hatujatoa hati. Watu wanasita kuchukua hati kwa sababu tozo hii ilikuwa kubwa kuliko kodi ya asili ambayo imetungwa na Sheria ya Bunge. Kwa hiyo, tunahisi baada ya kuondoshwa hii *premium then* tunaamini kwamba, wananchi watamiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wananchi Waheshimiwa Wabunge wamewasemea na Mheshimiwa Rais amesikia ameondoa hii kodi. Kwa hiyo, hakuna kizuizi chochote sasa kisingizio cha kuweza kumilikishwa kwa sababu, gharama kubwa ya umilikishaji imeondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelekea na sisi kama Wizara, kama ambavyo wameanza kodi ya majengo kwenda

ki-*electronic*, na sisi tumejipanga kuja ki-*electronic* vilevile. Tunaangalia uwezekano pengine mwakani tutakuja na bajeti tofauti, tunaangalia namna nzuri zaidi ya ukusanyaji wa kodi ya ardhi pengine kwa kuunganisha na majengo, lakini tutajipanga vizuri. Na sisi tunaunga mkono hili la ukusanyaji tujaribu ukusanyaji huu wa kutumia bili za umeme, lakini na sisi kwenye kodi ya ardhi kwa sababu, majengo yako kwenye ardhi na taariza zote tunazo kwa hiyo, na sisi tunajipanga ki-*electronic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tumefunga mfumo mpya ambao umetengenezwa na vijana wa kitanzania. Mwezi ujao tutaanza kutoa Hati za *Electronic* hapa Dodoma. Mfumo huo utatuwezesha sisi kutokutumia mabavu sana kufuatilia kodi ya kila mwaka kwa sababu, ndani ya mfumo ule tuna namba za simu, tuna taarifa za kila mmiliki wa ardhi. Ikifika siku ya kulipa kodi *message* itakujia kwenye sim una kukuomba ulipe kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mfumo ambao umetengenezwa na wataalamu wa Wizara na utaanza kutumika. Wale wote ambao watachukua hapa Dodoma hati kuanzia tarehe 01 mwezi wa saba wataanza kupata hati za *electronic*. Na pengine tutaachana na hii tabia ya kufukuzana kwa sababu, kila mwananchi atakumbushwa siku ya kulipa kodi. Tunataka tufanye jambo hili nchi nzima, ili tupunguze kasi ya kukamatana na kufukuzana kwa ajili ya ukusanyaji wa kodi, turahishe, lakini tupate mapato ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakushukuru sana kwa muda ulionipa, lakini nataka nirudie kuunga mkono kwa nguvu zangu zote hotuba hii ya Wizara ya Fedha kama walivyofanya wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais, lakini kuwapongeza sana wenzetu Mawaziri wa Wizara ya Fedha na watendaji wote wa Wizara ya Fedha. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumebakiza mchangiaji mmoja ambaye yeye atachangia kesho, kwa

maana ya Naibu Waziri wa Fedha, kabla ya mwenye hoja yake hajahitimisha.

Waheshimiwa Wabunge nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wote kwa michango yenu ya muhimu kabisa ya kuishauri Serikali hap ana pale katika mipango yake ya mwaka 2021/2022. Mmetoa michango mingi nani dhahiri michango hii Serikali inasikiliza kama ambavyo waliskiliza mawazo ya Kamati na sasa imelisikiliza Bunge zima linasemaje. Naamini mambo mengi ambayo mmeyachangia Waheshimiwa Wabunge siku ya kesho pengine mtayasikia baadhi nani ahata yale ambayo hamtakuwa mmeyasikia naamini mipango inayokuja huko mbele itakuwa imeyachukua hayo pia.

Kwa hiyo, mmetoa mic hango mizuri yenyewe mashiko ya msingi kabisa ambayo inaisaidia Taifa letu kusonga mbele na inaisaidia Serikali kujipanga kwa namna ya kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi, lakini pia kuwahudumia wananchi kwa yale ambayo tumejipanga kwa miaka mitano. Kwa hiyo, niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa haya mabadiliko anayoyafanya hapa na pale ambayo yanatusaidia Waheshimiwa Wabunge kufanya kazi yetu kwa ufanisi zaidi kuliko wakati mwininge.

Waheshimiwa Wabunge yako matangazo hapa machache:-

Kwanza tangazo la wageni; tunao wageni 172 wa Mheshimiwa Abdul Aziz Abood ambaa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kutoka Mkoani Morogoro wanaosoma kozi ya maendeleo, mipango, ama kupanga na usimamizi (*Development Planning and Management*) pamoja na Kozi ya Maendeleo Vijijini (*Rural Development*) wakiongozwa na Prof. David Mhando. Karibuni sana wageni wetu kutoka Morogoro na kwa kweli mnasoma kozi ya msingi kabisa hii itatusaidia maana humu ndani tunajadili mipango,

tunajadili usimamizi, tunajadili maendeleo, naamini leo mmejifunza mambo mazuri, karibuni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni 183 wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambao ni wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Shule ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino Tanzania cha Jijini Mwanza wakiongozwa na Mkufunzi Jackson Katabaro. Karibuni sana, jamani hawa ni wanasheria wajao baadaye na mnaona wameanza kujipanga kabisa kuanzia mwaka wa kwanza wameshajua kuvalia suti vizuri na tai na mambo mazuri namna hiyo. (*Makof*)

Sawa, sasa wamepiga makofi na mimi nawasamehe kwa sababu, ningekuwa bado nafundisha wangekuwa ni wanafunzi wangu. Sasa mnawenza kukaa, asanteni sana na karibuni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge lipo tangazo lingine, tangazo muhimu linatoka kwa Katibu wa Bunge; anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, siku ya kesho, Jumanne, tarehe 22 Juni, 2021, Waheshimiwa Wabunge magari yenu ile sehemu mnayoegesha ya mbele ya zahanati ya Bunge siku ya kesho magari hayataruhusiwa kuegeshwila hilo eneo kwa sababu kuna kazi maalum ya ukarabati kwenye hilo eneo. Kwa hiyo, mnaombwa Waheshimiwa Wabunge muweke magari yenu sehemu nyingine zote isipokuwa sehemu hiyo ya mbele ya zahanati.

Waheshimiwa Wabunge liko jambo lingine hapa, niliwaambia nina matangazo mengi kidogo; Mheshimiwa Gati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mara, alipata ajali jana, lakini kwa ujumla anaendelea vizuri, anaendelea kupata huduma Hospitali ya Benjamin Mkapa. Kwenye ajali hiyo alikuwepo pia na mumewe naye anaendelea vizuri. Taarifa rasmi itatolewa kesho na Mheshimiwa Spika.

Tangazo lingine na la mwisho Waheshimiwa Wabunge, mnakumbushwa kwa sababu, siku ya kesho, siku

ya tarehe 22, yale yote ambayo tumekuwa tukiyajadili wakati wa bajeti za kisekta na sasa bajeti kuu ya Serikali kesho ndio tunapiga kura ya uamuzi. Na kura hii hupigwa kura ya wazi na kila mmoja anapiga kura ye ye peke yake binafsi kwa kusimama sehemu yake na kusema, kama ye ye anasema Ndiyo au Hapana. Huwa linaitwa jina moja baada ya lingine, sasa kuweka msisitizo mpaka Waziri Mkuu huwa anatakiwa kuitika jina lake kama Mbunge.

Sasa Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Spika, alishatangaza kwamba, kila Mbunge kesho awepo. Na sasa mnakumbushwa kesho Mbunge ambaye hatakuwepo kuitika nadhani mtakuwa mmeshaelezwu hayo mambo mengine ambayo huwa yanafuata baada ya hapo, yanakuwa sio shughuli ya Bunge usije ukaanza kumtafuta Spika kwamba, sikuwepo siku ya kuitika kura ukiwa umeitwa kwenye chama chako. Kwa hiyo, kura itapigwa kesho na kwa kawalda watu wamezoea kura hupigwa mchana, kesho kura itapigwa asubuhi, kura itapigwa asubuhi.

Hili ni tangazo ambalo utazame kitu cha jirani yako kama Mbunge hayupo mme taarifa. Asipokuwepo saa ya kuitika hakuna muda mwingine wa kuitika.

Waheshimiwa Wabunge naamini hilo limeelewaka. Na mimi nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa hilo siku ya kesho.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, Saa Tatu Kamili asubuhi.

*(Saa 01.35 Usiku Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumanne,  
Tarehe 22 Juni, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*